Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA KUMI

**Kikao Cha Nne -Tarehe 1 Februari, 2008**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samwel J. Sitta -Spika) Alisoma Dua*

**Mwongozo wa Spika**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika**,** katika Bunge hili ulitoa mwongozo juu ya Wabunge ambao wanahitaji kupata nyaraka Serikalini, kwamba pamoja na kwamba ipo sheria Wabunge wanaoataka nyaraka ni lazima waandike barua kwa Katibu wa Bunge. Mnamo mwezi Septemba mimi nilifanya hivyo na tarehe 4 Septemba, Katibu wa Bunge alimwandikia Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha akimwambia kwamba nipatiwe nyaraka ninazozihitaji zinazohusu Alex Stuart. Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha akamwandikia Katibu wa Bunge akimwambia kwamba nyaraka hizo zipo Benki Kuu na kwamba aziombe huko.

Mheshimiwa Spika, tarehe 8 Katibu wa Bunge alimwandikia Gavana wa Benki Kuu ili ampatie nyaraka hizo. Hadi leo sijapata nyaraka hizo. Katiba ya Bunge inaturuhusu kuihoji Serikali, sheria ya *Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act* inaturuhusu tupate nyaraka. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Bunge hili alisema kwamba Serikali haina tatizo la kutoa nyaraka, na wewe mwenyewe ulitoa mwongozo juu ya namna gani ya kupata nyaraka na mpaka leo nyaraka ninazozidai zimewagharimu Watanzania si chini ya shilingi bilioni 70/-. Ningeomba kupata mwongozo wako ni utaratibu gani sasa tuutumie baada ya Katiba sheria kutokuheshimiwa. Baada ya Maagizo ya Waziri Mkuu na mwongozo wako kutoheshimiwa je, tutumie utaratibu gani sasa? Naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tulikwishatoa maelekezo na tuliweka utaratibu wa Wabunge kupata nyaraka kwa utaratibu ambao ulielekeza. Nasikitika kwa kilichotokea kuhusu Benki Kuu lakini nina hakika kuwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed anajua mgogoro uliokuwepo Benki Kuu na Gavana kuwa Mgonjwa kwa muda mrefu. Naomba mtuachie tulifuatilie tujue ni nini kilichotokea lakini Wabunge watapata nyaraka kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Ofisi ya Spika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani baada ya kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni kutoa kauli ambayo ni ya dhati naiona, sina tena ya kuendelea kutoa mwongozo wowote, ahsante sana.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 43

### Historia ya jengo la Bunge la Tanzania

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. JANETH B. KAHAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa historia ya Bunge letu inaanzia mwaka 1926 wakati huo likiitwa *Legislative Council* (*LEGCO*), lakini jina hilo lilibadilika na kuwa *The National Assembly* baada ya nchi yetu kupata uhuru:-

Je, Bunge hilo la (*LEGCO)* lilikuwa likitumia ukumbi uliokuwa unaitwaje, na ukumbi huo uko sehemu gani Jijini Dar es Salaam na sasa unatumika kwa shughuli zipi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth B. Kahama , Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli historia ya Bunge la Tanzania imeanza mwaka 1926 wakati huo nchi yetu ikiwa chini ya himaya ya wakoloni wa Kiingereza. Wakati huo Bunge lilikuwa linajulikana kama Baraza la Kutunga Sheria (*Legislative Council – LEGCO*). Kiongozi wake alikuwa Gavana aliyetawala dola hadi uhuru. Baada ya kupata uhuru mwaka 1961 jina *LEGCO* lilibadilishwa kuwa *The National Assembly* na kuongozwa na Mheshimiwa Spika.

Kuanzia mwaka 1926 hadi 1945, Baraza la Kutunga Sheria halikuwa na ukumbi maalumu wa kufanyia vikao vyake kama ilivyo sasa. Sehemu mbalimbali zilitumika ikiwa ni pamoja na ukumbi wa *Arnatouglou*, ukumbi huu uko Wilaya ya Ilala eneo la Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam. Aidha, *LEGCO* lilitumia pia jengo ambalo sasa linaitwa *Freemasons Hall* lililopo karibu na ubalozi wa Zambia likitazamana na hoteli ya Kilimanjaro- barabara ya *Ocean Road* na jumba la makumbusho ya Taifa, mtaa wa Shabaan Robert, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ukumbi wa *Anatouglou* unatumika kwa mikutano ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Ukumbi wa *Freemasons* unatumiwa na Taasisi binafsi inayoitwa *Freemasons*. Ukumbi wa Karimjee umetumiwa na Baraza la Kutunga

Sheria tangu mwaka 1945 hadi tulipopata uhuru, hivi sasa unatumiwa kwa mikutano ya Jiji la Dar es Salaam na Meya wa Jiji anatumia sehemu ya majengo ya ukumbi huu kwa ajili ya ofisi yake.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa majengo hayo ni kumbukumbu muhimu sana katika nchi yetu kwa kizazi hiki kipya; je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka historia hii kwa ajili ya kumbukumbu ili vizazi vyetu vijue tulianzia wapi kutoa maelekezo ya Bunge hili katika nyumba zipi na zikawekewa hadhi ya kitaifa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, kama ifuatavyo:-

Ni kweli majengo ya kihistoria kama haya yaliyotumiwa kwa ajili ya shughuli za Baraza la Kutunga Sheria na pia Bunge letu ni vema yakawekewa kumbukumbu. Lakini kama tulivyokwisha ambiwa hapo mwanzo, hayo majengo hayakuwa ya Serikali, kwa hali hiyo si sahihi kusema kwamba tuyawekee kumbukumbu. Kwa sababu kama yalikuwa yanaazimwa kwa ajili ajili ya shughuli hizo hatuna mamlaka nayo. Anatouglou ni mali ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwa hiyo, wao ndiyo wenye mamlaka ama kuyatoa hayo majengo kwa ajili ya shughuli za kumbukumbu.

**MHE. SULEIMAN OMAR KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa historia haina Serikali, haina mtu binafsi, je, serikali yetu haioni kwamba kuna umuhimu wa kuyatafuta maeneo yote, hata kama sasa hivi maeneo hayo si ya Serikali ili kulinda historia yetu katika nchi hii?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kumchaya kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa kuna umuhimu wa nchi yetu kuweka historia ya kuendelea kutafuta maeneo ambayo yalikuwa ni ya kihistoria lakini bado hatujayaweka katika kumbukumbu zetu. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia kwamba tutazingatia ushauri wao wa kuyatafuta maeneo yaliyokuwa ya kihistoria na kuyaweka katika kumbukumbu zetu na kuyatambua kutokana na mchango wa majengo hayo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu jibu la kwanza lilikuwa lina utata kidogo, sasa umeweka vizuri.

Na. 44

**Ahadi za kuboresha mji wa Kibaha**

**MHE. RAMADHANI A. MANENO ( K.n.y. MHE. DR. ZAINAB A. GAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaahidi wananchi wa Jimbo la Kibaha kuwa litakuwa na viwanda vingi na kuwa makao makuu ya Mkoa yatakayokuwa na barabara nzuri; na kwa kuwa mpaka sasa hayo yote hayajatekelezwa, na hata Waziri Mkuu alipotembelea Kibaha alikuta bado kuna mapori mengi; je, utekelezaji wa ahadi hizo utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Serikali iliamua Mji wa Kibaha kuwa Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani kwani tayari kulikwishakuwa na huduma muhimu ikiwa ni pamoja na miundombinu kama vile huduma ya maji safi na salama, barabara kuu ya Morogoro- Dar es Salaam, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na juhudi mbalimbali katika kuendeleza mji wa Kibaha, katika juhudi hizo maeneo yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na kuboresha huduma mbalimbali juu ya matumizi ya ardhi kama vile makazi, makazi na biashara, taasisi, viwanda, huduma za umma n.k. Katika kukamilisha mipango hiyo zipo juhudi za makusudi kabisa ambazo Serikali kupitia Halmashauri inazifanya, juhudi hizi ni pamoja na:-

(1) Kuboresha mpango wa matumizi ya ardhi ikiwa ni pamoja na kubadilisha matumizi kwa kufuta baadhi ya viwanja na badala yake eneo hilo litumike kama kitovu cha Mji wa Kibaha.

(2) Kutenga eneo la Zengereni lililokuwa shamba la Halmashauri kuwa eneo kwa ajili ya matumizi ya viwanda badala ya vile vilivyofutwa kwa matumizi ya kitovu cha Mji.

(3) Kuandaliwa kwa mpango wa matumizi ya ardhi katika eneo la Shirika la Elimu Kibaha, jambo ambalo litaondoa mapori katika mji wa Kibaha.

(4) Kupimwa kwa viwanja 21 vya Taasisi katika eneo la Mkoa (msitu) ambapo hadi hivi sasa Taasisi kumi na moja (11) zimegawiwa na kulipia tayari kwa uendelezaji wa ujenzi wa Taasisi hizo.

(5) Kuwepo na mpango wa kuzifanyizia matengenezo barabara za kibaha Mjini zenye urefu wa kilomita 4 kwa kiwango cha lami. Matengenezo hayo ni pamoja na barabara za waenda kwa miguu, magari na kuweka taa za barabarani. Barabara

zilizopewa kipaumbele katika matengenezo hayo ni zile za Mjini kuanzia Maili Moja, Stendi hadi Mkoani, Magereza hadi Sheli, Magereza hadi nyumbani kwa Mkuu wa Wilaya ya Kibaha na Mkoani hadi Ikulu ndogo ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, zenye urefu wa kilomita Nne (4).

(6) Aidha, kupitia mfuko wa barabara kwa mwaka 2007/08, Halmashauri ya Mji wa Kibaha imetenga kiasi cha shilingi milioni 398 na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha imetenga kiasi cha shilingi milioni 368.5 kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, zote hizi ni jitihada za Serikali katika kuboresha Miundombinu na ahadi hizo zinaendelea kutekelezwa kwa awamu kulingana na bajeti ya Serikali.

**MHE.RAMADHAN A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwenye swali la msingi jambo kubwa ambalo alikuwa ameliuliza Mheshimiwa Dr. Zainab Gama ni ahadi ya Rais wakati akiwa kwenye kampeni juu ya uwezekano wa kupata viwanda na kustawisha Mji wa Kibaha uendane sambamba na miji mingine kama ilivyo Makao Makuu ya Mkoa. Swali langu la nyongeza ni kwamba je, mpaka sasa ni wawekezaji wangapi wameshaonesha nia ya kuwekeza viwanda katika Mkoa wa Pwani Mjini Kibaha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maneno kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba sasa hivi tupo katika mipango ya kuupangilia Mji wa Kibaha na tumekwishapima sehemu mbalimbali kwa ajili ya uendelezaji wa Mji huo na sehemu za viwanda pia zimekwisha pimwa. Suala la wawekezaji wangapi ambao wamekwishaonesha nia ya kuwekeza katika sehemu za Kibaha hilo linahitaji takwimu, naomba niende kwenye mamlaka husika ili niweze kupata takwimu sahihi niweze kumjibu kwa ufasaha zaidi.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, haya ndiyo majibu ya ukweli kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kutoa majibu ya nyongeza ya swali la Mheshimiwa Ramadhani Maneno, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kufuatia ahadi alizotoa Rais wakati wa uchaguzi, Wizara mbalimbali tumekuwa tukizifuatalia na katika sekta zetu kuangalia tutatekeleza vipi. Wizara ya Ardhi imechukulia suala hilo na kufuatana na sera yetu ya makazi tumetoa takriban shilingi milioni 400/- ili kuendeleza Mji wa Kibaha.

Mheshimiwa Spika, tumejitahidi kuwasaidia katika *strategic plan* au mkakati wa kupanga mji huo vikiwemo viwanda katika Mkoa mzima wa Pwani. Pamoja na hayo shilingi milioni 400/- tumewaagiza wapime maeneo ya viwanda, maeneo ya makazi, na huduma za Jamii na tayari wamekwisha anza kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, nilitaka kuongezea tu kwamba ahadi za Rais zinatekelezwa na siyo Kibaha tu ni Mkoa mzima wa Pwani, Bagamoyo na Mkuranga . (*Makofi*)

Na. 45

**Ratiba za mikutano ya Wilaya na Mikoa kuzingatia ratiba ya vikao vya Bunge**

**MHE. FUYA G. KIMBITA (K.n.y. MHE. MBAROUK K. MWANDORO)** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi Waheshimiwa Wabunge wametoa rai na Serikali imekubali na kutoa ahadi Bungeni kwamba ratiba za mikutano mbalimbali ya Serikali katika ngazi za Mikoa na Wilaya zitapangwa kwa kuzingatia ratiba ya Bunge ili Waheshimiwa Wabunge wapate fursa ya kuhudhuria na kuchangia katika vikao hivyo muhimu bila kulazimika kuondoka Bungeni mara kwa mara; na kwa kuwa bado utaratibu huo hauzingatiwi:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa Wabunge kutohudhuria vikao hivyo wanakosa fursa muhimu ya kutoa miongozo na kuhakiki udhaifu unaostahili;

(b) Je, ni lini Serikali itachukua hatua thabiti za kuhakikisha uzingatiaji wa agizo hilo muhimu ili Wabunge waweze kuhudhuria vikao vyote vya Serikali na Bunge.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uendeshaji na usimamizi wa shughuli na vikao vya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya au za Miji) huongozwa na kufanyika kwa kuzingatia Sheria za Serikali za Mitaa Namba 7 na 8 za mwaka 1982 na Kanuni, Taratibu na miongozo mbalimbali iliyowekwa na Halmashauri husika, Kanuni, Taratibu na miongozo hiyo huidhinishwa rasmi na mamlaka zilizowekwa kisheria ambapo mamlaka mojawapo ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Viongozi wa mamlaka za Serikali za Mitaa yaani Waheshimiwa Madiwani na Wabunge kupitia vikao vyao mbalimbali vya Kamati na Mabaraza ya Madiwani ndiyo wanaofanya uamuzi kuhusu shughuli za mamlaka zao.

Mheshimiwa Spika, vikao vya ngazi ya Mkoa ambavyo Waheshimiwa Wabunge ni wajumbe, hufanyika kwa kuzingatia Sheria za Tawala za Mikoa, Na. 19 za mwaka 1997. Vikao vya kimkoa ambavyo Waheshimiwa Wabunge ni wajumbe ni Kamati ya Ushauri ya Mkoa inayofanya vikao vyake vya kawaida mara mbili kwa mwaka na vikao vya Bodi ya Biashara ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zinao utaratibu wa kuandaa na kuidhinisha ratiba ya mwaka ya vikao vya Kamati zote na mabaraza ya Madiwani. Mkutano wa kwanza wa kawaida ndiyo unaojadili na kuidhinisha ratiba ya vikao vya Kamati na Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri, ambapo Waheshimiwa Wabuge ni Wajumbe. Kwa upande wa ngazi ya Mkoa, Wajumbe hufahamishwa mapema kabla ya kufanyika kikao na hupewa ajenda za kikao. Utaratibu wa sasa wa kuandaa, kuidhinisha na kufanyika kwa vikao hivi unawapa nafasi Waheshimiwa Wabunge kushiriki kikamilifu na wanapokuwa na udhuru basi wanapata fursa ya kutoa hoja na kuchangia agenda za vikao kwa maandishi.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na utaratibu huu wa ushirikishwaji wa Waheshimiwa Wabunge katika uandaaji wa ratiba za vikao vya Halmashauri na vile vya ngazi ya Mkoa na kwa kuwa vikao vya Bunge navyo huendeshwa kwa mujibu wa sheria na Kanuni za Bunge, kwa sasa Serikali haioni sababu ya kuzielekeza halmashauri kutoendesha vikao vyake hadi wabunge wanapokuwepo kwenye majimbo. Hata hivyo, Ofisi yangu imekwishawasiliana na Ofisi ya Bunge na kupata rasimu ya ratiba ya vikao vya Bunge kwa mwaka 2008. Tayari tumewasiliana na Halmashauri zote nchini kwa barua yenye Kumbukumbu Na. BA229/402/01 ya tarehe 2/10/2007 na kuzielekeza kuandaa ratiba za vikao vya halmashauri kwa kuhusisha ratiba ya vikao vya Bunge ili kupunguza migongano.

Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba agizo hili litatekelezwa isipokuwa wakati wa Bunge la Bajeti ambalo huchukua muda mrefu inabidi utaratibu uangaliwe upya ili kuzifanya Halmashauri zisisimamishe baadhi ya shughuli za Serikali za Mitaa, ni kwa njia ya vikao *(committee System*).

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu ambayo yametoa jibu kwa swali la msingi.

Naomba niulize swali moja dogo la nyongeza na kwa sababu ni Wizara hiyo hiyo, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza nini kuhusu Ofisi za Wabunge ambazo hazipati ile huduma ambayo tumekwishaipitisha kwenye Bajeti zetu. Nimeunganisha tu kwa sababu Wizara ni hiyo hiyo moja kwa sababu bado baadhi ya Makatibu Tawala hawahudumii ofisi zetu?

**SPIKA:** Swali hilo ni jipya, ni vizuri tu uliandikie ili liweze kujibiwa siku za usoni.

Na. 46

**Maandishi ya kukataza rushwa kwenye milango ya ofisi za Serikali**

**MHE. JACKSON M. MAKWETA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika ofisi nyingi za makao makuu ya Wizara, Mikoa na Wilaya yapo maandishi kwenye milango ya Ofisi hizo yanayosema: "Hatupokei Rushwa", "Rushwa ni adui wa haki," "Usitoe rushwa," au *"You are entering a corruption free zone,"* n.k:-

(a) Je, maandishi hayo kwenye milango yanazuia vipi utoaji na upokeaji rushwa, kama si kuwadhalilisha watumishi walio kwenye ofisi hizo na majengo yake?

(b) Kama kuandika maandishi hayo siyo sharti la kupata misaada je, Serikali inaweza kuagiza yaondolewe mara moja ili kutunza heshima ya Taifa letu?

(c) Kama ni lazima kwa maandishi hayo, basi mtumishi avalishwe beji shingoni yenye maandishi hayo; na ni wapi mahali pengine duniani mtindo huo umeondoa rushwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a) b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matangazo au maandishi yanayowekwa kwenye milango ya Ofisi za Serikali yanayosema hatupokei rushwa au *you are entering a corruption free zone*, yanalenga katika kuelimisha, kukumbusha na kuhamasisha jamii kuhusu ubaya na madhara ya rushwa. Kwa hiyo, madhumuni makubwa ya matangazo ya aina hii ni kugusa hisia za mtoa huduma na mpokeaji wa huduma ili awapo katika maeneo hayo asiwe na fikira ya kudai kushawishi au kupokea rushwa, ama kutoa au kushawishi kutoa rushwa. Kwa hiyo, matangazo haya hayalengi katika kuwadhalilisha Watumishi au ofisi za Serikali. Uchapishaji na ubandikaji wa matangazo hayo katika milango au kuta za ofisi za Serikali, hauna uhusiano wowote na maombi ya misaada ya kutoka kwa wafadhili na wala si sharti la kupatiwa misaada. Kwa hiyo, Serikali haina sababu ya kufikiria kuyaondoa kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya rushwa yanahitaji pia utashi na utayari wa kisaikolojia, hivyo matangazo haya yanalenga kubadili mitazamo ya watumishi

pamoja na wananchi kuhusu kuacha kushiriki vitendo vya rushwa. Maandishi hayo ni muhimu na kwa kuwa hayawalengi Watumishi peke yao si vema watumishi pekee kuvalishwa beji shingoni. Badala yake Watumishi wanavaa vitambulisho ili waweze kutambuliwa na wapewa huduma.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya nchi kama vile Hong Kong na Chile zimefanikiwa kwa kiasi fulani kupunguza vitendo vya rushwa kwa kutumia matangazo na maandishi ya aina mbalimbali yanayolenga kuhamasisha jamii kuhusu madhara ya rushwa. Kwa hiyo, ubandikaji wa matangazo ya maandishi kwenye kuta za ofisi pamoja na maeneo mbalimbali ni njia mojawapo ya kuhamasisha vita dhidi ya rushwa.

**MHE. JACKSON M. MAKWETA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kama lengo ni hilo ambalo Mheshimiwa Waziri anasema kisaikolojia ni kujaribu kuwazuia wapokeaji na watoaji rushwa, ingawa sipendelei, kwa nini wasingeweka yale maandishi ndani ya ofisi ya yule Mtumishi kusudi anapoingia awe anayasoma ndani ya ile ofisi na si nje?

(b) Jambo la pili Mheshimiwa Spika, ni kwamba saikolojia ya mambo haya unavyoyahubiri ndivyo unavyoyatangaza. Kuna wakati shirika fulani hapa Tanzania lilikuwa linatangaza ukitaka likupe bidhaa zenye risiti basi ulipe shilingi 100,000/=, bila risiti lipa shilingi 90,000/=. Mheshimiwa Shelukindo akichangia Bungeni hoja mbalimbali alikosoa kwamba njaa hii mnatangaza wenyewe; je, si vizuri mkaacha? Walipoacha inasemekana hata ile shughuli mbaya imefungwa. Nadhani hata katika hili tunatangaza badala ya kuzuia, je, haoni ubaya huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Makwetta maswali yake mawili ya nyongeza kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kuhusu maandishi kuwa nje au ndani hakuna tatizo kubwa kwa sababu mtumishi hata maandishi yakiwa nje huwa anayatambua na kama hoja ni maandishi pia yawe ndani tutafanya hivyo. Hili la kuhubiri mapambano haya nadhani si vema sana kuchukulia mapambano dhidi ya rushwa kwa urahisi namna hiyo. Rushwa katika Taifa ni tatizo kubwa, wengi tunaichukulia rushwa kama saratani katika mwili wa binadamu. Serikali au Taifa lolote linalokumbatia rushwa kwa hakika linajichimbia kaburi lake, hivi mapambano haya tuyachukulie kwa uzito wake kama ambavyo Serikali kwa sasa inachukulia kwa uzito huo.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. kwa kuwa tafsiri nyingine ya mabango hayo yanayowekwa nje ya majengo ni kuonesha kwamba watumishi wanaofanya kazi katika ofisi hizi hawapokei rushwa ndani ya ofisi hizo na inawezekana wakapokea nje ya ofisi halafu wakaja kufanya kazi bila rushwa ndani; je, kuna kipengele chochote katika sheria yoyote ya rushwa

kinachompatia adhabu ya ziada mtu anayepokea rushwa ndani ya jengo kwa sababu anadanganya Umma? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Kwimba, swali lake kama ifuatavyo:-

Kwa hakika mabango yale lengo lake ni kutoa tahadhari na kuelimisha. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile hayana maana nyingine.

**MHE. MARTHA M. MLATA**: Mheshimiwa Spika, pamoja na matangazo hayo ambayo yako ofisini Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba rushwa ni mahali popote pale, iwe vijijini, mitaani au majumbani. Je, ana mkakati gani katika kuwaelimisha wananchi ambao wako vijijini ambao wao ndiyo waathirika wakubwa kwa janga hili la rushwa? Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Napenda kukubaliana naye kwamba rushwa hasa katika nchi yetu imeenea sana na ndiyo maana mtandao wetu wa kupambana na rushwa umefika mpaka Wilayani. Mikakati yetu ya kupambana na rushwa inajulikana. Kwanza, ni kuelimisha na katika eneo hili kama inavyojulikana kwa sasa kuna Kamati za maadili katika kila Wizara na Idara za Serikali na tunatarajia kufikisha Kamati hizi za maadili *(Integrate Committees)* katika ngazi za Halmashauri na Kamati hizi zinatakiwa zitoe taarifa ya hali ya maadili na hali ya rushwa katika Halmashauri na idara mbalimbali katika ofisi yangu. Lakini pia kwa upande wa mapambano yenyewe, kama nilivyosema mtandao wetu umepanuka kutoka Makao Makuu, Mkoani hadi Wilayani. Bila shaka matokeo yake yanaonekana.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nitaongea na Kamati yako ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuwaeleza jinsi ambavyo kwa muda mfupi uliopita tangu sheria mpya ya kupambana na rushwa itungwe tulivyoingia kati na kuweza kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 1.8 ndani ya Halmashauri zetu katika miezi mitatu tu ya sheria hii yaani kati ya Julai na Septemba, 2007. (*Makofi*)

Na. 47

**TAKUKURU kupatiwa vitendea kazi**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa TAKUKURU ni idara mpya na ambayo kama itafanya kazi yake kikamilifu itakuwa ni mkombozi wa wanyonge hasa wanaodaiwa rushwa:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali haijaipatia Idara hiyo vitendea kazi vya kutosha ili kazi wanayoifanya ifanyike kwa ufanisi?

(b) Je, ni lini Serikali itatembelea mikoani na hasa Mkoa wa Rukwa wilayani Nkasi ili kuona mazingira yasiyoridhisha ya vitendea kazi vya TAKUKURU?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa heshima napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuimarisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, ili iweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi, Serikali imekuwa ikitenga fedha za kununua vitendea kazi, kwa kadri ya uwezo wake kifedha. Kwa mfano, katika mwaka 2007/2008, TAKUKURU imepatiwa vifaa vya msingi katika Ofisi za Mikoa na Wilaya zote Tanzania Bara. Vifaa hivyo ni pamoja na magari, samani za ofisi, mashine za nukushi, simu na huduma ya intaneti. Vifaa hivi bado havitoshelezi mahitaji lakini angalau Wilaya na Mikoa yote imepata vifaa vichache na Serikali katika mwaka ujao wa fedha 2008/2009 itawaongezea vifaa hivyo kadri ya uwezo wa Bajeti ya Serikali utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Viongozi wa Serikali wamefanya ziara mikoani na hata Mkoa wa Rukwa umetembelewa pia na hususan Wilaya ya Nkasi. Kwa sasa hali ya vitendea kazi vilivyopo hasa katika Mkoa wa Rukwa ni ya kuridhisha. Kwa mfano, Ofisi ya TAKUKURU Mkoani Rukwa ina jengo linalomilikiwa na TAKUKURU yenyewe na lina nafasi ya kutosha.

Ofisi yetu pia Wilayani Nkasi, ofisi zote hazina gari, kompyuta, samani, simu, mashine za nukushi na huduma za intaneti isipokuwa Ofisi ya Wilaya. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa maboresho yanayoendelea yatawezesha TAKUKURU kupata vifaa vingi ne vya kutosha kwa kila Mkoa na Wilaya awamu kwa awamu kutegemeana na mapato ya Serikali.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa taasisi zingine zinazofanana na TAKUKURU kama vile Usalama wa Taifa, Polisi na wengineo, huwa wana majengo ambayo yako tofauti na ofisi za *RC* pamoja na Mkuu wa Wilaya; na kwa kuwa TAKUKURU inafanya kazi muhimu sana inayofanana na idara kama hizo.

(a) Je, kuna utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba hawakai katika majengo ya RC au kwa Wakuu wa Wilaya bali wajengewe ofisi zao tofauti kabisa kama ilivyo kwenye idara hizo nilizozitaja?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, hajawahi kufika Rukwa na hususan Nkasi ili kuona vitendea kazi vilivyopo pale Wilayani na aende kule Mpanda pia Sumbawanga; je, ni lini Mheshimiwa Waziri atautembelea Mkoa wa Rukwa ili kusudi aone vitendea kazi alivyovitaja kama vitafanya kazi sawa sawa au vipi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu rafiki yangu Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi maswali yake kama ifuatavyo:-

Kwa kweli kuna utaratibu wa kuzitenganisha ofisi za TAKUKURU katika Wilaya na Mikoa yote nchini. Ni Wilaya na Mikoa michache sana ambayo kwa sasa Ofisi ya TAKUKURU ipo ama katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Kwa mwaka huu tunajenga ofisi mpya Mkoa wa Lindi, tunakamilisha ujenzi Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Iringa pia tunajenga Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Maswa. Tutaendelea hivyo hivyo kadri tutakavyopata uwezo kutoka Serikalini. Namuahidi Mheshimiwa Ponsiano kwamba nitafanya ziara siyo tu Sumbawanga, Mpanda na Nkasi pengine tutafika hata ziwani kule Kalema, Kasanga na kwingine ambako tunatarajia kufungua ofisi ndogo. Ahsante.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali lifuatalo:-

Mnamo mwishoni mwa mwaka jana tulisikia kule Arusha Wabunge wenzetu walikamatwa na TAKUKURU wakidai walikuwa wanatoa rushwa. Mpaka sasa hivi sijasikia maendeleo ya kesi hiyo. Je, Serikali haioni kutokuendelea na kesi hiyo kwa haraka ni kutowatendea haki Wabunge hao pamoja na wananchi wao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, suala hili lipo mahakamani na kwa mujibu wa Kanuni zetu hatuwezi kulijadili hapa. Kwa hiyo, tunaendelea, tunahamia Wizara ya Miundombinu.

Na. 48

**Miundombinu ya Mabasi yaendayo Kasi Jijini Dar es Salaam**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:

Kwa kuwa Serikali ipo mbioni kuandaa miundombinu kwa ajili ya mabasi yaendeayo kasi katika jiji la Dar es Salaam; na kwa kuwa Serikali kwa upande mwingine inazungumzia juu ya udhibiti wa mwendo wa kasi kwa mabasi yanayokwenda mikoani kwa kufunga vidhibiti mwendo (*speed governor*) na tumeambiwa kuwa hatua hiyo

itasaidia kupunguza ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikipoteza maisha ya Watanzania kwa wengi:-

Je, Serikali haioni kuwa kutenganisha miundombinu ya mabasi yaendayo kwa kasi huenda kukaongeza ajali zaidi kwani mara nyingi tunaelekezwa kuwa mwendo wa kasi unaua?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Serikali iko mbioni kuandaa miundombinu kwa ajili ya mabasi yaendeyo haraka katika jiji la Dar es Salaam sanjari na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005-2010, ibara ya 45, Kifungu Kidogo Na. (h). Jiji la Dar es Salaam limeupa mradi huu jina la *Dar Rapid Transit* (*DART)*. Wakala wa uendeshaji *(DART Agency)* wa mfumo huu umekwishaundwa kwa mujibu wa sheria kwa Tangazo la Serikali Na. 120 la tarehe 25 Mei, 2007.

Mheshimiwa Spika, dhana ya mabasi yaendayo haraka inahusiana na usafiri unaoenda kwa wakati tofauti na dhana ya kwenda kasi. Kwa kweli hii ni *bus rapid transit* siyo *bus speed transit.* Unaokwenda haraka na siyo unaokwenda kasi. Usafiri huu utamwezesha mwananchi kufika kwenye kituo anakotaka kwa wakati na kwa uhakika ukilinganisha na mfumo wa sasa wa Daladala.

Aidha, utenganishwaji wa miundombinu ya mabasi unalenga katika kuwezesha mabasi haya yaweze kusafiri kwa wakati uliopangwa bila kuzongana na usafiri wa aina nyingine. Usanifu wa mradi huu unalenga kuwa na mabasi yatakayosafiri kwa mwendo wa k.m. 22 kwa saa. Miundombinu yake inazingatia watumiaji wote wa barabara, kwa maana ya kuwa waenda kwa miguu, baiskeli na magari ya kawaida yatakuwa na njia zao tofauti. Vilevile patakuwa na vivuko salama katika kila kituo cha basi kwa ajili ya abiria.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, miundombinu hii italenga katika kuhakikisha usalama wa watu na utenganishwaji wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka. Haulengi kuongeza ajali bali utapunguza sana ajali kwa kuwa mfumo mzima unasanifiwa kitaalamu ukizingatia usalama wa watu wa aina zote.

Na. 49

**Ukarabati wa Barabara Wilaya ya Ngara**

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara nyingi katika wilaya ya Ngara ni za udongo na hazipitiki kabisa hasa wakati wa mvua, mfano barabara ya kutoka Murugarama kupitia Juluigwa,

Rulenge, Keza, Kumubuga mpaka Mizani, na barabara kutoka Kabanga kupitia Mabawe, Muruvygira, Mukikomero, Kasange, Ntobeye mpaka Rusumo Feri:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukarabati Barabara hizi na kuzitengeneza kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Feedham Filipo Banyikwa, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Mizani (Nayakahura) kupitia Kumubuga – Keza – Rulenge – Murugarama hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Ngara yenye urefu wa kilometa 105 ni ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia wakala wa Barabara, Mkoa wa Kagera.

Kilometa 85 kutoka Mizani –Kumubuga – Keza – Rulenge – Murugarama ni za changarawe na kilometa 20 toka Murugarama hadi Ngara Mjini ni ya kiwango cha lami. Barabara ya kutoka Kabanga – Mabawe – Mukikomero – Muruvygira – Kasange – Ntobeye mpaka Rusumo Feri ni ya Wilaya na inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

Barabara ya Murugarama kupitia Rulenge, Keza, Kumubuga hadi Mizani imekuwa ikifanyiwa matengenezo kila mwaka. Katika mwaka wa fedha 2000/2001 barabara hii ilifanyiwa matengenezo makubwa kwa kiwango cha changarawe cha gharama ya shilingi 221.5 milioni chini ya ufadhili wa pamoja wa Serikali ya Uholanzi na Serikali ya Tanzania. Aidha, Wizara yangu imeendelea kuifanyia matengenezo ya kawaida barabara hii kila mwaka ambapo jumla ya shilingi 184.03 milioni zimetumika kugharamia matengenezo hayo kati ya mwaka 2001/2002 hadi 2006/2007 na kuiwezesha kupitika wakati wote.

Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara yangu imetenga jumla ya shilingi 335.6 milioni kwa ajili ya kugharamia matengenezo mbalimbali katika barabara hii, kazi ambazo zimeanza kutekelezwa kuanzia Septemba, 2007 na zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kutokana na ufinyu wa bajeti, bali itaendela kuifanyia matengenezo ya kawaida na muhimu kadri itakavyohitajika ili iendelee kupitika wakati wote.

Kuhusu barabara ya kutoka Kabanga – Mabawe – Mukikomero – Muruvygira – Kagange – Ntobeye mapaka Rusumo Feri, namshauri Mheshimiwa Mbunge, awasiliane na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Ngara, ili kupata mikakati ya ukarabati na ujenzi wa barabara za Wilaya katika Wilaya ya Ngara ikiwemo barabara hiyo, ambapo kwa mwaka 2007/2008 Mfuko wa Barabara umetenga shilingi milioni 407.28 kwa ajili ya kukarabati na kutengeneza barabara za Wilaya katika Wilaya hiyo ya Ngara.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara zilizoko Ngara zinafanana kabisa na barabara za Jimbo la Mbinga Magharibi; na kwa kuwa Jimbo la Mbinga Magharibi lina barabara moja kubwa kutoka Kaskazini kwenda Kusini na barabara hiyo sasa haipitiki kwa sababu madaraja mengi yamevunjika; je, Serikali inaweza kuniazima Helkopta nitembelee jimbo langu? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Capteni Komba, kama ifuatavyo:-

Kwa hali halisi barabara nyingi ambazo zinahudumiwa na *TANROADS* katika nchi nzima zinapitika vizuri na hasa baada ya Serikali kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kukarabati barabara hizi, zile za dharura ambazo tumeweka kwenye bajeti, nyingi zinapitika. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kutumia helkopta kutembelea Jimbo. Hata katika ziara ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya hivi karibuni, amejionea mwenyewe jinsi barabara za Wilaya ya Mbinga zinavyopitika na si kweli kwamba zinahitaji helkopta kupita. Hata Waziri wangu ametoka huko barabara zinapitika wala sio kwa helkopta. (*Makofi*)

**SPIKA:** Siku nyingi hajauliza swali msaidieni hapo.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naomba kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa barabara hii ya kutoka Kabanga kupitia Mavawe, Muluvygira, Mkikomelo, Kasange, Mtobe mpaka Lusumo ni barabara ya kiulinzi kwa maana inaambaa kwenye mpaka wa nchi yetu na Burundi na Ruanda; Je, haoni kwamba inastahili kuchukuliwa na *TANROADS* kama barabara ya mkoa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Ombi lake tumechukua na litaangaliwa wakati tunapitia kanuni ambazo zinaendelea kutengenezwa ili kuona kama kweli barabara hiyo inakidhi vigezo vilivyowekwa na sheria mpya ya barabara ili tuipandishe hadhi. (*Makofi*)

Na. 50

**Matumizi ya Kiswahili katika Elimu**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa shule kadhaa za kimataifa nchini ambazo hazitumii Kiswahili katka kutoa elimu hazitaki kusikia mwanafunzi yeyote akizungumza Kiswahili; je, Serikali ina ushauri gani kwa wazazi/Watanzania ambao wana watoto wanaosoma katika shule hizo ambazo zinaififisha lugha ya taifa letu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zipo shule 17 za kimataifa *(International Schools)* ambazo zimesajiliwa hapa nchini. Shule hizo zimekubaliwa Kimataifa kupewa leseni ya kufundisha kwa kutumia mtaala wa kimataifa, na hufanya mitihani inayoandaliwa kwa kuzingatia mitaala hiyo. Katika shule hizo Kiswahili ni somo la hiari. Shule za kimataifa zilianzishwa ili kuwasaidia wanafunzi wa kimataifa ambao wazazi wao wapo nchini kwa shughuli mbalimbali kama vile wafanyakazi wa mashirika ya kimataifa na mabalozi. Aidha, zipo shule nyingine ambazo si za kimataifa lakini hutumia lugha ya Kiingereza katika kufundisha. Shule hizo zinatumia mitaala ya Kitanzania ambapo Kiswahili ni mojawapo ya masomo yanayofundishwa. Kutoruhusu kuzungumza Kiswahili katika shule hizo ni utaratibu unaotumika ili kuwasaidia wanafunzi kuielewa lugha na kuitumia vizuri lugha inayotumika kufundishia darasani.

Mheshimiwa Spika, nawashauri wazazi wanaowapeleka watoto wao kusoma katika shule za aina hii wawapatie fursa ya kujifunza Kiswahili wakiwa nje ya mazingira ya shule. Aidha, wawaruhusu kushiriki shughuli nyingine za kiutamaduni kama vile ngoma, nyimbo, mashairi, ngojera kwa lugha ya Kiswahili.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa Majibu yake mazuri. Lakini nina swali moja. Kwa kuwa amesema kwamba zipo shule 17 ambazo zinatambuliwa kama shule za kimataifa; lakini pia akasema kwamba kuna shule nyingine ambazo siyo za kimataifa ila zinatumia mtalaa wa Kingereza; je, atakuwa tayari sasa kutupa orodha hiyo ili na sisi tuzijue shule hizo kwa manufaa yetu, lakini pia na Watanzania wengine?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, shule ambazo zimepata kibali ni kama ifuatavyo:-

*International* Arusha ambayo iko Mkoa wa Arusha, *St. Constantine* Mkoa wa Arusha, *St. George* – Arusha, *International School of Tanganyika*, Dar es Salaam, *St. Mary*, Tabata, Loleti iko Mkoa wa Dar es Salaam, *Heaven of Peace* iko Mkoa wa Dar es Salaam, *ESACS* ipo Mkoa wa Dar es Salaam, *Academic International* ipo Mkoa wa Dar es Salaam, Kwanza *International* ipo Dar es Salaam, *St. Mary, Mbezi Beach* iko Mkoa wa Dar es Salaam, Canon Adrew Mwaka iko Mkoa wa Dodoma, *Iringa International* iko Mkoa wa Iringa, *International School of* Moshi iko Mkoa wa Kilimanjaro, *Morogoro International School* iko Morogoro, Isamilo iko Mkoa wa Mwanza, *Tanga International* ambayo iko Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, pengine ningependa tu niongeze ziada na niwatoe hofu wananchi. Naomba katika kukitukuza Kiswahili nimnukuu Rais wa Awamu ya Pili,

Mzee Ali Hassan Mwinyi, katika moja ya nasaha zake wakati akizindua Baraza la Kiswahili alisema, "Kiswahili ni hazina kwetu, ni vema Watanzania tukaona fahari kuwa nacho". Akashauri kuwa kifundishwe kwa ufasaha na kitumike vema. Aidha, alisema Kingereza ni lugha inayoboresha mawasiliano na mahusiano kitaifa na chenyewe kifundishwe kwa juhudi kubwa. Vinginevyo tutapoteza mawasiliano na wenzetu duniani." Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa jibu zuri sana linalodhihirisha maandalizi mazuri na naamini kwamba Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii anakulea vizuri sana. (*Makofi/Kicheko)*

Na. 51

**Tatizo la Mpunga Pori**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa mpunga pori umekuwa ni tatizo kubwa kwa wakulima wa mpunga hapa nchini ambapo mavuno ya mpunga halisi yanaweza kupungua kwa asilimia 70; je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima wa mpunga kuondokana na tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Hemed, Mbunge wa Chambani, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mpunga pori umekuwa ni tatizo kubwa kwa wakulima wa mpunga hapa nchini. Tatizo hili limo pia katika nchi nyingine za Afrika, Asia, Amerika ya Kusini na Visiwa vya Caribbean. Mpunga Pori una uwezo mkubwa wa kufyonza virutubisho ukilinganisha na uwezo wa mpunga wenyewe na hivyo kuathiri ukuaji wake na hatimaye kusababisha upungufu wa mavuno ya mpunga kwa kiwango kikubwa. Upungufu wa mavuno ya mpunga huweza kufikia asilimia 70 au zaidi ya kiwango cha uzalishaji kutegemea uwingi wa mpunga pori ulioota pamoja na mpunga shambani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya utafiti uliofanyika katika mabonde ya mpunga ya Kilombero, Dakawa, Kyela na Ruvu, kuhusu tatizo la mpunga pori, Serikali imechuikua hatua mbalimbali kwa lengo la kuwasaidia wakulima, wakiwemo wakulima wa mpunga wanaokabiliana na tatizo hilo la mpunga pori. Hatua hizo ni:-

(i) Kuendelea kuwashauri wakulima kupanda mbegu safi zisizochanganyika na mbegu za mpunga pori kulingana na maelekezo ya kitaalamu.

(ii) Kuwashauri wakulima kusafisha mashamba mapema kabla ya muda wa kupanda.

(iii) Kuwashauri wakulima kuchavanga majaruba ya mpunga mapema kwa kutumia matrekta ya mkono kabla ya kupandikiza miche ya mpunga; na

(iv) Kuwashauri wakulima kutumia uatilifu aina ya *Glyphosate (Round-up)* kabla ya kupanda, kulingana na maelekezo ya kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wakulima wakiwemo wakulima wa mpunga kuhusu mbinu za kudhibiti mazao mbalimbali na mpunga ukiwemo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Kwa kuwa lengo au dhamira ya Wizara na Serikali ni kuongeza tija katika kilimo; na kwa kuwa tatizo hili la mpunga pori linapunguzwa kwa kiasi kikubwa tija iliyokusudiwa; na kwa kuwa Halmashauri za Wilaya hazionekani kuwa na dhamira sahihi ya kuvisaidia vituo vya utafiti kama vile TPLI iliyoko Kaskazini, Arusha ambacho ni mojawapo ya kituo kinachofanya kazi ya utafiti wa mpunga pori; je, Wizara ina mkakati gani madhubuti wa kuona kuwa vituo hivi ambavyo hatimaye vitakuja na jibu sahihi vinawezeshwa, hali kadhalika watafiti wanawezeshwa ili waweze kufanya kazi zao barabara?

La pili, tatizo hili haliwezi kuwa tatizo la Tanzania peke yake duniani kama Mheshimiwa Waziri alivyosema; je, anao ufahamu wa nchi ambayo ina tatizo kama hili na imefanikiwaje kuondoa tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kama ifuatavyo:-

(a) Kama nilivyosema katika jibu langu la awali kuwa Serikali inatoa elimu kutokana na matokeo ya utafiti yaliyofanyika Kilombero na maeneo mengine pamoja na Arusha kwenye vituo vyetu vya utafiti. Inatoa elimu kwa wakulima kusudi waweze kutekeleza zile njia ambazo zitasaidia kupunguza kuendelea kwa mpunga pori. Labda niseme kwamba kuna aina mbili za mpunga pori, ya kwanza inasambaa kwa mbegu, ya pili inasambaa kwa mizizi yake. Sasa lazima wakulima waelewe kwamba wanavyolima pia kuna gharama ambazo wanatakiwa waingie. Serikali haiwezi ikatoa dawa kwa ajili ya

kuua mpunga pori lakini inachoweza ni kutoa elimu. Vile vile inawezesha mwaka hadi mwaka katika bajeti yake inaongeza fedha za kuimarisha vituo hivi vya utafiti.

(b) Katika nchi ambazo zimeshapata tatizo hili nilisema ni pamoja na Amerika ya Kusini yaani maeneo ya Amerika ya Kusini na Carebbean. Sasa wanafanyaje, njia ya kwanza ni kuhakikisha kwamba wanapalilia kwa kutumia mikono ama kwa kutumia majembe madogo ambayo hayawezi yakang'oa mpunga. Lakini hiyo kazi inachukua muda mrefu sana na ni gharama kubwa. Lakini ya pili, kama nilivyosema awali kuna dawa inaitwa *round up.* Dawa hii inaua mpaka kwenye mizizi, wanatakiwa watumie dawa hii kabla hawajapanda ule mpunga. Hii itasaidia na kwa Tanzania bei ya lita moja ya *round up* ni shilingi 12 hadi 15 kwa lita. Katika hekta moja zinatumika lita nne. Kwa maana hiyo shilingi 50 mpaka shilingi 60 zinatosha kuua magugu ya hekta moja ambayo inatoa magunia 60 hadi 75. Kwa hiyo, mkulima awe tayari kugharamia kama anataka apate mavuno mengi.

Na. 52

**Ruzuku ya Pembejeo kwa wakulima**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imepania kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kama mahindi kwa kutoa ruzuku kwenye pembejeo kwa wakulima hususan wa Nyanda za Juu Kusini:-

(a) Je, ruzuku kiasi gani ilitolewa kwa ajili ya kilimo cha mahindi mwaka 2005/2006 na 20006/2007 katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini?

(b) Je, ni faida kiasi gani ilitokana na ruzuku hiyo kwa Serikali na wakulima wa zao hilo wa Nyanda za Juu Kusini katika misimu hiyo miwili?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilianza kutoa ruzuku ya mbolea katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yaani Ruvuma, Iringa, Mbeya na Rukwa katika mwaka wa 2003/2004 kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo hususan mahindi. Mpango huo umeendelea kutekelezwa ambapo katika mwaka 2005/2006, ruzuku ya shilingi 4,903,224,375.00 sawa na asilimia 72 ya fedha za ruzuku zilizotengwa ilitolewa katika mikoa hiyo. Ruzuku hiyo ilitosheleza usambazaji wa jumla ya tani 38,645 ya mbolea ambazo zilisambazwa kama ifuatavyo:- tani 8,900 Mkoani wa Ruvuma, 14,275 Mbeya, 2,380 Rukwa na 13,090

Mkoani Iringa. Katika mgawo wa Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Ludewa ilipata ya tani 2,129.

Katika mwaka wa 2006/2007, Mikoa hiyo ilipewa mbolea yenye ruzuku ya tani 64,875 yenye jumla ya fidia ya ruzuku ya shilingi 9,139,321,000.00 (sawa na asilimia 69 ya fedha zilizotengwa). Kiasi hicho cha mbolea kilikuwa sawa na asilimia 59.689 ya mbolea iliyosambazwa nchi nzima. Mchanganuo wa mgawo kwa kila Mkoa ulikuwa Ruvuma tani 17,734; Mbeya 18,251; Rukwa 5,310 na Iringa 23,580. Wilaya ya Ludewa ilipata tani 3,341.

Aidha, katika mwaka wa 2006/2007, Serikali ilianza kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbegu bora ambapo mikoa hiyo ilipangiwa jumla ya tani 769,253 za mahindi sawa na asilimia 26 ya nchi nzima. Mchanganuo wa kila mkoa ulikuwa tani 205.8, Ruvuma, 203 Mbeya, 139.8 Rukwa na Iringa tani 220.7.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa upatikanaji wa mbolea ya ruzuku, matumizi ya mbolea katika mikoa hiyo yameongezeka kutoka tani 76,349.2 katika mwaka 2005/2006 hadi 98,834 katika mwaka wa 2006/2007. Ongezeko la matumizi ya mbolea limechangia katika ongezeko la tija ya mahindi kutoka tani 1.3 kwa hekta katika mwaka 2005/2006 hadi 1.4 kwa hekta katika mwaka 2006/2007. Aidha, uzalishaji wa zao la mahindi katika mikoa hiyo umeongezeka kutoka tani 3,423,000 msimu wa 2005/2006 hadi tani tani 3,659,000 msimu wa 2006/2007 na hivyo mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa katika upatikanaji wa chakula hapa nchini.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Nashukuru Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa Serikali inatumia fedha nyingi sana ambazo ni za walipakodi ambao ni maskini sana kwa ajili ya kufidia gharama za pembejeo kwa wakulima hao na kisha Serikali huwaachia wafanyabiashara ndiyo wanunue sehemu kubwa ya mazao hayo kwa bei ndogo sana, kwa kweli kwa bei ya kutupwa, napenda kuuzliza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa nini Serikali inawakamua maskini walipa kodi na kuwatajirisha wafanya biashara badala ya kuwapa faida hiyo wakulima wenyewe au kujipatia Serikali yenyewe faida?

(b) Kwa nini Serikali isilete Muswada Bungeni ili *SGR* waweze kufanya biashara ya nafaka badala ya kununua na kuhifadhi mazao kidogo sana, *kiduchu*, ukilinganisha na gharama kubwa sana ambayo Serikali inaingia katika kufidia gharama hizo? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, niseme tu Serikali haikamui wananchi, wananchi sharti watoe kodi kwa ajili ya shughuli mbalimbali kwa mujibu wa sheria, kwa ajili ya maendeleo, na maendeleo ya kilimo yakiwemo. Vilevile ili kuweza kupunguza tatizo hili la masoko, kwa maana ya wafanya biashara wakubwa kununua mazao haya, niseme tuko kwenye soko huria, lakini pia wananchi na wakulima wanaweza wakatumia soko hilo kwa kuanzisha vyama vya ushirika na *SACCOS* ambazo

zinaweza kuuza yale mazao yao kwa bei nzuri mahali ambapo wanaweza wakanunua. Wakulima wakawauzia *SACCOS*, *SACCOS* nazo zikaweza kuuza hata kwa wafanya biashara kama tulivyofanya kwenye zao la pamba na zao la korosho kwa msimu huu.

Pili, suala hili la kwamba *SGR* ifanye biashara, sasa hivi *SGR* kama ilivyo haifanyi biashara kwa sababu ni kwa ajili ya kuhifadhi chakula cha akiba, chakula cha dharura kwa miezi mitatu ambapo ni tani 150,000 kila mwaka. Lakini suala hili tumelisikia, kukiwa na haja ya kufanya hivyo nadhani Serikali inaweza ikaleta kwa manufaa ya wananchi. *(Makofi)*

Na. 53

**Matatizo ya Maji Jimbo la Ubungo**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Kata ya Goba na Mtaa wa Msewe na Kata ya Ubungo kuna matatizo makubwa na sugu ya maji na miradi iliyojengwa kwa misaada ya wahisani ni mzigo mkubwa kwa wanancjhi wa maeneo hayo kutokana na ghareama za kuendesha miradi hiyo na kwa kuwa, ni sehemu ndogo sana za maeneo h ayo zinapata maji:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba wananchji wa Goba na Msewe, wanapta maji ya kutosha na kwa bei nafuu?

(a) Kwa kuwa eneo la Kimara ambako yapo matangi ya maji linakabiliwa na ukosefu wa maji. Je, hali hiyo inasababishwa na nini na Serikali inachukua hatua gasni kurekesbnisha hali hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpoango gani wa kutumia maji ambayo yanasadikika yapo ardhini chini ya Mkoa wa Dar es Salaam?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maeneo ya Goba na Msewe ni miongoni mwa maeneo yaliyo kwenye ukanda wa juu wa Jiji la Dar es Salaam ambayo hupata maji kutoka mtambo ya Ruvu Juu. Mtandao uliopo kwenye maeneo haya ni wa siku nyingi na umechakaa. Uchache wa maji yanayosukumwa kutoka Ruvu Juu hufanya maji yasambazwe kwa mgawo. Kwa kupunguza tatizo hili kwenye maeneo haya ipo miradi miwili ambayo hutumia nguvu za pampu za umeme kutoa maji kwenye ukanda wa chini hadi Goba na Msewe.

Miradi hii huendeshwa na kamati za maji za wananchi wenyewe. DAWASCO huuza maji kwa Kamati hizi kwa kiwango cha shilingi 725 kwa lita 1000 sawa na shilingi 14.50 kwa ndoo ya lita 20 au shilingi 145 kwa pipa la lita 200. Hata hivyo, Kamati za

maji nazo huuzia maji wananchi kwa bei ya shilingi 20 kwa ndoo ya lita 20 ili kufidia gharama za uendeshaji kama vile matengenezo na kuwalipa wahudumu wa mradi. Bei hii ndiyo inayotumika kwenye miradi ya maji kwa jamii Dar es Salaam. Katika matukio kadhaa Kamati zimekosa uwaji bikaji na hivyo kupandisha bei kiholela. Ninamuomba basi Mheshimiwa Mbunge ahamasishe Kamati za Maji katika Jimbo lake zisimamie vizuri huduma hii ili iweze kutolewa kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, ili wananchi wa Goba na Msewe waweze kupata maji ya kutosha na kwa bei nafuu Serikali kupitia *DAWASA* itekeleze mradi wa maboresho ya miundombinu ya usambazaji maji katika maeneo ya Ubungo Kibo na Msewe. Hatua iliyofikiwa sasa ni kuwa usanifu utayarishaji wa makabrasha ya zabuni umekamilika. Kibali cha kuitisha zabuni kwa ajili ya ujenzi kimetolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB).* Hivyo, zabuni itatangazwa hivi karibuni. Aidha, kutekelezwa kwa mradi huu kutaongeza idadi ya vioski vilivyopo katika maeneo haya hivyo kurahisisha upatikaqnaji wa maji kwa wananchi katika maeneo husika.

(b) Mheshimiwa Spika, tatizo la maji kwenye eneo la Kimara linasababishwa na uwezo mdogo wa mtambo wa Ruvu Juu kama nilivyoeleza awali. Aidha, upotevu wa maji kwa kuvuja unaotokana na uchakavu wa mitandao wa bomba pamoja na ongezeko la matumizi ya maji kuanzia eneo la Kimara mpaka Mlandizi. Ili kutatua tatizo hili, Wizara yangu kupitia *DAWASA* imekamilisha kazi ya usanifu kwa ajili ya kuboresha mfumo wa usambazaji maji katika maeneo yote yaliyo kandokando ya bomba kuu kutoka mtambo wa Ruvu Juu hadi Kimara. Kazi ya ulazaji mabomba katika maeneo ya Temboni, Golani, Changanyikeni, Mbezi na Goba itafanyika. Hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa mradi huu katika maeneo haya ni kwamba ripoti ya tathmini ya kumpata Mkandarasi imepelekwa *ADB* kupata kibali ili kazi iweze kuanza katika mwaka huu wa 2007/2008. Utekelezaji wa mradi huu pia utasaidia kupunguza uvujaji wa maji na kuboresha usambazaji wa maji ili yawafikie wananchi walio wengi katika maeneo yao.

(c) Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa awali uliofanywa na *DAWASA* umebaini kuwa kuna maji chini ya ardhi yanayofaa kwa matumizi ya binadamu. Maeneo hayo ni Kimbiji (Kigamboni) na Mpera (Mkuranga). Kisima kingine kilichochimbwa eneo la Mpiji kilionyeasha kutokuwa na maji yenye ubora unaostahili kwa matumizi ya bindamu. *DAWASA* inakamilisha sasa taratibu za kumpatra Mhandisi Mshauri wa kufanya uchunguzi wa kina ili kuhakiki wingi wa maji katika mwamba wa Kimbiji, chini ya ufadhili wa Serikali ya Norway. Kazi hii inatarajiwa kuanza mapema katika mwaka wa fedha 2008/2009. Aidha, Mhandisi Mshauri *AAW Consulting Engineers* anakamilisha usanifu wa mradi wa kutumia visima vya Kimbiji kwa ajili ya matumizi ya wakazi wa Dar es Salaam. Kazi ya usanifu inatarajiwa kukamilika Aprili huu 2008. Mradi huu ukikamilika Jiji la Dar es Salaam litakuwa limepata chanzo kingine kwa kutumia maji chini ya ardhi.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Waziri kwa majibu yake mazuri. Na pia nimshukuru Naibu Waziri kwa kutembelea maeneo ya Jimbo la Ubungo kuona hali ya maji mwishoni mwa mwaka jana. Tatizo ni kwamba wananchi wanalipia maji, wanalipia umeme, wanalipia upotevu wa maji na kwa

hiyo maji yanapofika Goba na Msewe yanakuwa na bei kubwa kuliko hiyo ambayo tumeambiwa. Ninachoomba ni Wizara ikubali DAWASCO wachukue miradi hii Kamati za Maji zifanye usambazaji. Je, Waziri atakubaliana na mimi juu ya hili?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Sera ya Maji inataka wananchi wenyewe wachangie gharama ya kuendesha miradi ya maji na kwa wananchi wa Ubungo ambao wameshafanya kazi hii kwa kiasi kikubwa nawapa pongezi. Lakini hili analolisema Mheshimiwa Mbunge nalipokea. Tutakachokifanya tutafanya uchunguzi wa Kamati za Maji zinaridhisha kiasi gani kwa gharama ya kuchota maji katika viosk hivi kwa wananchi. Gharama ambayo inategemewa na Wizara ambayo inaripoti nayo ni sh.20 kwa ndogo moja ya lita 20. Wizara itafanya uchunguzi ili iweze kuzisaidia Kamati hizi na itakapoonekana kwamba ni lazima basi Serikali itachukua hatua zinazohusika.

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ya kutupa moyo kwamba tutaendelea kupata maji. Lakini nina swali dogo tu kwamba je, haya maji machafu ya kununuka yanayozagaa kwenye mji wa Dar es Salaam kuna ufumbuzi gani wa kuweza kuyaondoa mpaka leo hii?

**SPIKA:** Kwa taarifa huyu siyo Naibu Waziri. Huyu ndiye Waziri mwenyewe, Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi huo. Tatizo hilo tumeshalifahamu na Mamlaka husika DAWASCO wanalifuatilia kwa karibu tutegemee hivi karibuni tutakuwa na ufumbuzi wa tatizo hilo.

Na. 54

**Miradi ya Ufadhili wa Maji Misungwi**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi Bungeni katika bajeti ya mwaka 2007/2008 kuwa suala la maji Wilayani Misungwi limo katika mpango wa kufadhiliwa na MCC *(Millenium Challenge Corporation)* pamoja na hayo pia Serikali ilitenga Tsh. milioni 400 kukamilsha baadhi ya upembuzi yakinifu na maandalizi mengine muhimu:-

(a) Je, kati ya kiasi cha Tshs. 400 milioni zilizotengwa zimetumika ngapi kwa kazi ile na zimebaki ngapi?

(b) Je, wafadhili wa *MCC* wako katika hatua gani ya utekelezaji wa mradi huo?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi kwa ajili ya maji kwa wananchi wa Misungwi wanaoteseka na tatizo hilo?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Jimbo la Misungwi, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 410 kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008 kwa ajili ya mradi wa maji ya Mji wa Misungwi. Kwa bahati mbaya sana fedha ya programu ya maji zimechelewa kutolewa hivyo kuchelewa kupelekwa Misungwi. Hata hivyo, Wizara yangu sasa imeshatoa shilingi milioni 231 ambazo ni fedha za robo mbili ya mwaka 2007/2008 na taratibu ya kuzituma fedha katika Halmashauri zinakamilishwa. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Ununuzi wa pampuni 1 (yenye uwezo wa kusukuma maji mita za ujazo 16.7 kwa saa).

(ii) Ununuzi wa mabomba yenye vipenyo mbalimbali.

(iii) Ukarabati wa chujio (*Treatment Plant).*

(iv) Ukarabati wa matanki 2.

(v) Ujenzi wa Ofisi.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi wa maji katika mji mdogo wa Misungwi ulikuwa katika mpango wa kufadhiliwa na *Millenium Challenge Corparation (MCC)* katika uboreshaji wa miundombinu ya maji safi baada ya upembuzi yakinifu chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(AfD)* ambao kukamilika. Hata hivyo, *MCC* waliamua kujitoa kugharamia mradi wa maji wa Mji wa Misungwi kutokana na kupunguzwa kwa bajeti iliyokuwa imepangwa awali na MCC. Hata hivyo, Serikali imeamua kutekeleza mradi huu kwa kutumia fedha zake kupitia Programu ya Sekta ya Maji *(WSDP).*

c) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati ya makusudi ya kuwapataia maji wananchi wa Misungwi ambayo ni kuendelea kutenga fedha kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji – *Water Sector Development Programme (WSDP)* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji safi toka Ziwa Victoria umbali wa kilometa 12 ambao unakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 15. Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu wa kina na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni zinafanywa. Hadidu za Rejea *(Terms of Reference)* hivi sasa zinatayarishwa.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kutokana na majibu ya Waziri nina imani kabisa wananchi wa Misungwi wamechanganyikiwa kutokana na majibu ambayo yamewanyima raha hasa ukizingatia kwamba Mheshimiwa Rais alipotembelea Misungwi na akahutubia wananchi wengi wa Misungwi aliwaahidi kuwa MCC

ingeliweza kufadhili mradi wao na akaainisha vijiji ambavyo vingeweza kufaidika na pesa hizo. Na kwa vile MCC hawakuihusisha Misungwi, kuna mbadala gani unaoendana na ahadi ya Mheshimiwa Rais ili kupunguza matatizo ya wananchi wa Misungwi. Hilo swali la kwanza.

La pili, kwa kuwa mradi wa Kahama na Shinyanga unaotoa maji Ziwa Victoria umegharimu karibu bilioni 200 za Kitanzania ambazo ni za walipa kodi wa Tanzania ni kwa nini Serikali isitoe hizo bilioni 15 kwa wananchi wa Misungwi wanaoteseka ili nao wakaweza kufaidi matunda ya uhuru? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ahadi za Mheshimiwa Rais ni maelekezo kwa Serikali hii na ahadi hizo zitatekelezwa pamoja na ahadi ambazo zimetolewa katika Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi. Tumeahidi kwamba miji mikuu yote ya Wilaya itaboreshewa miundombinu yao ya maji katika kipindi hiki cha Awamu ya Nne ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

*MCC* tumewaomba msaada kwa bahati mbaya MCC hawakukubali kugharamia mradi huu wa Misungwi na wala siyo Misungwi peke yake tumeomba miradi miji saba ikiwemo Misungwi, Bunda, Tarime, Geita, Bukoba, Bariadi na Morogoro. Iliyoidhinishiwa ni Morogoro peke yake katika hiyo miji saba. Kwa hivyo hatuna namna yoyote ile ya kuilazimisha MCC au Serikali ya Merekani kutupa pesa. Wametathmini mradi wa Misungwi wametueleza kwamba mradi huu hata ukikamilika hautoweza kujiendesha kibiashara na kufauatana na vigezo vyetu hatoufadhili mradi huu. Ukijiendesha kibiashara, usipojiendesha kibiashara Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kwamba mji wa Misungwi unapata maji. Na mpango mbadala tumeichukua Misungwi tumeiweka katika programu ya Sekta ya Maji na mwaka huu tumeitengea milioni 410 kama miji mingine. Tutaendelea kufanya hivyo mpaka wananchi wa Misungwi wote wawe wamepata maji. *(Makofi)*

Swali la pili, tumegharamia Kahama/Shinyanga kwa fedha nyingi za Watanzania wenyewe. Jumla ya bilioni 225, kazi hiyo tutaendelea kuifuatilia kuhakikisha pia wananchi wa maeneo mengine ambao wako katika hali ngumu ya maji Misungwi na Wilaya zingine wanapata maji kama vile ambavyo Kahama na Shinyanga na vijiji 54 ambavyo vinaambatana kwenye mradi huo vitapatiwa maji, na tutazindua mradi huo ndani ya mwezi wa Februari mwaka huu. *(Makofi)*

Na. 55

**Kuboresha kambi ya wazee Langoni**

**MHE. GRACE S. KIWELU** aliuliza:-

Je, ni hatua gani zinazochukuliwa kwa Serikali kuboresha hali ya uhaba wa watumishi, kukarabati nyumba za wazee, kujenga uzio na bwalo la chakula pamoja na kuweka usafiri wa uhakika katika kambi ya wazee Langoni iliyopo Kata ya Mji Mpya, Manispaa ya Moshi Mkoani Kilimanjaro ?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba nisahihishe kidogo kwa faida ya kumbukumbu kwamba jina sahihi la makazi yaliyopo Moshi Mkoani Kilimanjaro ni Njoro na siyo Langoni kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua kwamba katika jamii yapo makundi ya watu ambao uwezo wao wa kujikimu umepungua au haupo kabisa ilipitishwa Sheria Na. 3 ya matunzo kwa watu wasiojiweza ya mwaka 1982 inayotoa nafasi kwa watu wasio na uwezo wa kujikimu kutunzwa na Serikali. Kwa utaratibu huo Serikali inatoa matunzo kwa wasiojiweza katika makazi 17 ikisaidiwa na wakala za hiari zinazoendesha makazi 24. Makazi hayo kwa ujumla inahudumia wastani wa wasiojiweza 4,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika makazi takriban yote ikiwa ni pamoja na Njoro. Hali hii inasababishwa na kustishwa kwa muda mrefu kwa taratibu za ajira hivyo kusababisha kushindwa kuziba nafasi zilizokuwa zikiachwa wazi na watumishi wanaostaafu kuacha kazi au kufariki.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kushughulikia tatizo hili la upungufu wa watumishi kwa mujibu wa taratibu na kanuni zinazotawala ajira. Nia ya Wizara ni kupeleka watumishi wapya na wa kutosha katika makazi ya Njoro na kwingineko kadiri itakavyokuwa ikipata kibali cha kuajiri kutoka ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia inatambua hali mbaya ya majengo katika makazi yanayotunza wasiojiweza ikiwa ni pamoja na makazi ya Njoro. Kuanzia mwaka wa fedha wa 2006/2007 Wizara imeanza kutenga fedha za ukarabati wa Makazi pamoja na vyuo vya mafunzo ya kazi kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007 Bunge lako tukufu liliidhinisha fedha kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Kolandoto na Shinyanga. Mwaka 2007/2008 Bunge lako limeidhinisha fedha kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Sukamahela yaliyopo Manyoni, Vituo vya watu wenye ulemavu vya Singida, Mtapika (Masasi), Luanzari (Tabora), Mbeya na Shule ya Maadilisho, Irambo (Mbeya).

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakusudia kukarabati majengo ya makazi ya Njoro yaliyopo Mkoani Kilimanjaro katika mwaka wa fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia inatambua umuhimu wa kuvipatia vyombo vya usafiri vituo na taasisi zote zinazotoa huduma kwa watu wenye ulemavu, wazee na watu wasiojiweza. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara itaendelea kuhakikisha huduma zote

muhimu ikiwa usafiri na ukarabati wa majengo ya makao ya wazee na vituo vingine vya ustawi wa jamii zinaboreshwa.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wazee ni muhimu sana katika Taifa letu na katika kambi hizo walizo wazee hao wanayo matatizo mengi sana kama vile ya matibabu na chakula. Je, Serikali inasema nini ili kutimiza wajibu kwa wazee wetu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII**: Ni kweli kwamba katika makambi kunakuwa na tatizo la chakula na matibabu. Lakini kama nilivyozungumza katika jibu langu la msingi, nimesema kwamba Wizara inajitahidi kwa sababu makambi haya ni mengi na inajitahidi kutoa pesa kwa kadiri ya uwezo unapopatikana. Napenda nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba huduma ya chakula na matibabu ni jukumu la Wizara kweli na fedha inatengwa na kuweza kuona kwamba matibabu na chakula kinapatikana.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile naomba niseme kwamba pamoja na kutoa huduma za msingi kwa watu wasio na uwezo, napenda ifahamike kwamba maisha au matunzo katika makazi yana madhara yafuatayo:-

Kwanza yanadumaza upeo wa mtu kutenda kazi na vilevile yanaendeleza upweke lakini yanapunguza pia uhuru binafsi na yanaweka mipaka ambayo haipo katika maisha ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na madhara haya Wizara yangu kupitia sera ya Taifa ya wazee iliyopitishwa Septemba, 2002 imeelekeza kwamba matunzo kwenye makazi litakuwa kimbilio la mwisho baada ya kushindikana njia mbadala za matunzo. Hivyo matunzo timilifu yanapaswa kutolewa kwenye jamii na familia ndiyo yenye jukumu la msingi la kutoa matunzo kwa watu wasiojiweza.

**SPIKA:** Meryce, swali la nyongeza, sijapata taarifa kama umebadili jina. Kwa hiyo, nitakuita Meryce Mussa Emmanuel kama ilivyo kwenye rekodi zetu.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Asante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa swali alilouliza Mheshimiwa Grace Kiwelu, linafanana na tatizo lililoko katika kituo cha wazee cha Magugu, Babati Vijijini. Na kwa kuwa tumefika pale Kamati ya Huduma za Jamii, tumejionea huduma dhaifu iliyoko pale, chakula, majengo na uchakavu wa maeneo na mazingira machafu yanayowakabili.

Je, Serikali inasemaje juu ya kushughulikia tatizo lililopo katika eneo la Magugu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Meryce Emmanuel, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa Kambi ya wazee kule Magugu iko katika hali mbaya. Ni kweli Waheshimiwa wabunge wa Kamati ya Huduma za Jamii wametembelea na mimi nimeshawahi kutembelea pale, lakini Mheshimiwa Spika ni kwamba tulishatoa maelekezo yale mambo ambayo yanaweza kufanyika katika Halmashauri ya Babati waendelee kufanya. Lakini na sisi kama Wizara ya Afya kama ninavyosema tunatenga pesa kila inapofikia mwaka kuweza kuona kwamba haya makambi 14 yanaweza kukarabatiwa kama nilivyojibu katika swali langu la msingi. Kwa hiyo, ninamhakikishia kabisa kwamba tutalichukulia kwa uzito wake na tutahahakikisha kwamba haya makambi tutayahudumia kadiri ya uwezo utakavyoruhusu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunahamia sasa Wizara ya Fedha. Ni kweli muda wa kawaida wa maswali umefika lakini mtakumbuka tulianza na hoja ya Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, imetuchukua pamoja na majibu kama dakika 10 hivi. Kwa hiyo, hizo nitazifidia kwa kuingia kwenye haya maswali ya Wizara ya Fedha. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dakta Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu. Kwa niaba yake linaulizwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed.

Na. 56

**Tanzania na Fedha za *Debt Conversion Scheme - BoT***

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED (K.n.y. DR. WILBROAD P. SLAA)** aliuliza**:-**

Kwa kuwa Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ya tarehe 30 Juni, 2005/2006 inaonesha kuwa Tanzania imezuiliwa kutumia zaidi ya shilingi bilioni mbili kutoka kwenye mfuko wa "*Debt Conversion Scheme*" ulioko Benki Kuu kwa sababu waliochukua fedha kutoka kwenye mfuko huo hawajarejesha:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo?

(b) Kama jibu kwenye sehemu (a) ni 'ndiyo'; je, waliochukua fedha hizo ni akina nani kwa majina na ni kiasi gani cha fedha kila mmoja alichukua?

(c) Je, hadi Disemba, 2007 ni wangapi kati yao wamelipa na ni kiasi gani kila mmoja amelipa, na iwapo hawajalipa Serikali imechukua hatua gani ili Taifa lisiendelee kupoteza manufaa ya mfuko huo kwa ajili ya watu wachache?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAPHA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wilbroad Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ya tarehe 30 Juni, 2005/2006 haioneshi popote kuwa Tanzania imezuiliwa kutumia zaidi ya shilingi bilioni 2 kutoka kwenye mfuko wa *Debt Conversion Scheme* ulioko *BoT* kwa sababu waliochukua fedha kwenye mfuko huo hawajarejesha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika ukurasa wa 10, aya ya 2 ya ripoti hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inasema, na na-nukuu: *"We noted that the NBC External Payment Arrears Deposit (TZS) Account closed with a balance of TZS 2,288,418,463.41 as at 30th June, 2006 and total payment of TZS 4,227,632,787.60 were made during the year. On the other hand the total EPA loss in exchange – NBC was TZS 131,725,294,000"*. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Serikali ilitoa tamko tarehe 29 Januari, 2008, katika mkutano huu wa Bunge, suala hili limekwisha shughulikiwa chini ya *"special audit"* ya akaunti ya *EPA* iliyoko Benki Kuu. Hivyo, ni muhimu kuvuta subira na kuona matokeo ya utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu suala hilo. Vilevile juzi ulitoa mwongozo kwamba kwa vile Mheshimiwa Lucy Maenga, aliomba kwamba hesabu za Benki Kuu zijadiliwe ndani ya Bunge hili, nina imani suala hili linaweza likajibiwa vizuri zaidi wakati tunazungumzia hesabu hizo za Benki Kuu.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Asante sana Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa akaunti hii ilihusu madeni ambayo watu mbalimbali walikopa; je, Serikali itakuwa tayari kuleta orodha ya majina ya hao ambao wali-*default payment* ya hii *external payment* ya bilioni *2* na zaidi? Pili, kwa kuwa taarifa inayofanyiwa kazi na Tume aliyounda Rais haihusiani kabisa na Kanuni za Bunge, kwamba Kanuni za Bunge hazizuwii jambo ambalo linafanyiwa uchunguzi lakini inazuwia jambo ambalo liko Mahakamani; je, taarifa hiyo italetwa wakati huku tukiendelea na kazi nyingine za kushughulikia masuala hayo?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, suala hili tulilijadili awali na niliahidi kwamba nitatoa majibu baadaye. Kwa hiyo, mashauriano yanaendelea na litashughulikiwa likizingatia haki ya Kikatiba ya Bunge. Asante. Nadhani tuendelee Mheshimiwa Zitto, sidhani kama kuna zaidi ya hayo, basi tumemaliza hapo. Swali la mwisho kwa Wizara ya Fedha na swali la mwisho la leo Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando. Unapendeza sana katika vazi rasmi la Bunge la hivi sasa. Hongera sana!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Asante Mheshimiwa Spika, kwa pongezi hizo na pia kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali langu hili. Sasa naomba Swali langu Na. 57 lipatiwe majibu sahihi.

Na.57

**Mfuko wa Serikali**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa kuwa Katiba ya nchi imtoa fursa ya kuwa na Mfuko Mkuu wa Serikali na kwa kuwa hali ya makusanyo ya mapato kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni madogo sana kwa sasa:-

(a) Je, ni lini makusanyo ya mapato yatakusanywa pamoja kwenye mfuko mmoja na baadaye kutoa fungu kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambalo litakuwa kubwa kuliko ilivyo sasa ili uweze kusaidia maendeleo?

(b) Kwa mujibu wa taarifa za *TRA*, kwa sasa hali ya makusanyo ya mapato ikoje kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani katika kipindi cha kuanzia Julai – Novemba, 2007.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAPHA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika Tume ya pamoja ya Fedha ambayo ni chombo cha Muungano ilishaundwa na inatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Ibara ya 134 ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kazi ya kwanza ni kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na; au yahusuyo utekelezaji wa mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili mchango na mgawo wa kila mojawapo ya Serikali hizi.

(ii) Kazi ya pili ni kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha za Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Tume hiyo iliwasilisha mapendekezo yake kwa Serikali zote mbili juu ya vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano kupitia akaunti ya pamoja ya fedha ambayo ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mchakato wa kujadili mapendekezo hayo na kufikia makubaliano baina ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unaendelea. Utekelezaji wa mapendekezo hayo utaanza mara tu baada ya kufikia makubaliano.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, 2007, Mamlaka ya Mapato Tanzania yamejitahidi kukusanya mapato ya Serikali kulingana na Bajeti yake

kwa pande zote mbili Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Katika kipindi hicho makusanyo yalikuwa kama ifuatavyo:-

Moja, Tanzania Bara. Mwezi Julai *TRA* ilikusanya shilingi 248,426,000,000, mwezi wa nane shilingi 262,271,000,000, mwezi Septemba, shilingi 320,568,000,000. Mwezi Desemba shilingi 669,388,000,000 na Novemba, shilingi 269,389,000,000. Jumla ya makusanyo ilikuwa ni shilingi 1,370,043,000,000.

Pili, kwa upande wa Tanzania Visiwani, *TRA* iliweza kukusanya kwa mwezi Julai, shilingi 3,109,000,000, mwezi Agosti shilingi 3,206,000,000, mwezi Septemba, shilingi 3,634,000,000, mwezi Oktoba, shilingi 2,508,000,000 na mwezi Novemba shilingi bilioni 2,990,000,000. Jumla kwa upande wa Tanzania Visiwani ilikuwa ni shilingi 14,449,000,000.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa swali nililouliza linahusu matakwa ya Kikatiba, na kwa sababu katika majibu yake hajataka kusema waziwazi hili suala la mapato kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu ni tayari au mazungumzo yanafanywa na Tume ya Fedha; ningependa alieleze hili Bunge.

Pili, suala la mgawo ambao anasema unazungumziwa na hiyo Tume, mgawo ambao mara nyingi Bunge hili linaelezwa ni ule unaotokana na mikopo na misaada. Lakini hivi ni lini Bunge hili litaelezwa mgawo halisi katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Upande wa Zanzibar na Upande wa Jamhuri ya Muungano ukoje, utaletwa lini hapa Bungeni?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAPHA M. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kikatiba kuna chombo kinaitwa *Joint Finance Committee*. Chombo hiki kimeundwa, chombo hiki kinafanya kazi, nimezieleza katika jibu langu la msingi. Chombo hiki kimetoa mapendekezo kwa Serikali zote mbili. Serikali ya Tanzania Visiwani na Serikali ya Muungano wa Tanzania. Baraza la Mawaziri la Zanzibar limekwishaizungumzia. Sasa hivi Baraza la Mawaziri wa Serikali ya Muungano linakaribia kuizungumzia. Siwezi nikasema chochote kabla Baraza la Mawaziri halijatoa kauli.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kuwaambia Wabunge tu, ni kwamba mapendekezo ya Tume ni *very comprehensive.* Wameizingatia Katiba, wametembea nchi kadhaa zenye Serikali aina ya Tanzania, Serikali ya Muungano, Serikali ya *Federation*. Wamekuja na kitu ambacho wanafikiri ni muafaka kwa muungano wa aina yetu. Kwa hiyo, itakapokuwa tayari nina hakika italetwa Bungeni kwa taratibu za kawaida.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali ya leo yamekwisha. Matangazo, kwanza wageni. Tunao humu Ukumbini katika *gallery* ya kawaida vijana sita waliomaliza kidato cha nne mwaka jana kutoka shule za mikoa mbalimbali, wamekuja kuangalia shughuli za Bunge. Joseph Augustino, Iyunga, Mbeya. Yuko wapi? Wametoka hawa. Bakari Said, Ilboru. Nadhani hawa hawapo pamoja na

Fatma Jamali, Catherine Kileche na Herieth Manase. Pia tunao waandishi wa habari 15 kutoka Mkoa wa Ruvuma, wakiongozwa na ndugu Nyumayo. Ni wageni wa Wabunge wote wa Mkoa wa Ruvuma. Waandishi kutoka Ruvuma? Wale pale! Karibuni sana! Karibuni sana!

Wapo wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Makinda, na Mbunge wa Njombe Kaskazini, Mheshimiwa Jackson Makweta na pia Mbungwe wa Njombe Magharibi, Mheshimiwa Yono Kevela, nao ni Bahati Gersoni Msigwa, yule pale! Karibu sana Ndugu Msigwa. Upendo Godwin Mzovela, yule pale na Sixbert Mlowe! Hawa hawakuelezwa ni nani? Wametajwa vyeo tu, mmoja ni Mwenyekiti, mwingine Makamu Mwenyekiti, mwingine ni Katibu. Inawezekana! Aah! Basi nisiseme lolote.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Ester Nyawazwa, anaitwa Mzee Ali, anatoka bariadi. Mzee Ali? Loh! Leo wageni wetu hawana subira hata kidogo hawa. Wageni wengine Bungeni leo ni wageni wa Mheshimiwa Halima Omari Kimbau, Viti Maalum. Wageni tisa wakiwemo wanawake watano wanaume wanne. Ni vijana wa Kikundi cha Taarabu kutoka Mafia. Jina la kikundi, *Samsuri Culture Group*, wale pale wanatupungia mikono! Kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge, kikundi hiki mahiri kitafanya onesho katika ukumbi wa *Royal Village*, hapa Dodoma siku ya Jumamosi, kesho. Hawakutaja muda lakini nadhani ni dhahiri itakuwa ni jioni. Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa. Kuhusu vikao, Mheshimiwa William Shelukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara mfanye mkutano leo saa saba mchana katika ukumbi Na. 231. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Katibu wa Kamati ya Wabunge wa *CCM*, ameomba leo saa 7.30 mara baada ya kusitishwa kwa shughuli za Bunge asubuhi, kutakuwa na kikao cha wabunge wote wa *CCM* katika ukumbi wa Pius Msekwa. Kikao hiki ni cha dharura, mnaombwa Wabunge wote wa *CCM* kuhudhuria. Vilevile Katibu huyo wa Kamati ya Wabunge wa *CCM*, anaarifu kwamba kutakuwa na mkutano wa Waheshimiwa Wabunge wote wa *CCM* siku ya Jumanne tarehe 5 Februari, mara baada ya kuahirisha kikao cha Bunge. Loh! Sasa hii shida hii, sijui jioni? Mara baada ya kuahirishwa, nadhani ana maana kusitishwa ile saa 7.30 tena. Nadhani hivyo. Mheshimiwa Jenista? Katibu Msaidizi.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kikao hicho kitafanyika mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge za asubuhi siku hiyo ya Jumanne wiki ijayo.

**SPIKA:** Asante sana, kwa hiyo, Jumanne tarehe 5 Februari, Wabunge wote wa *CCM*, ukumbi wa Pius Msekwa saa 7.30 mchana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe taarifa kwamba kesho saa mbili asubuhi, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge, atazindua mkakati wa pili wa Taifa wa kudhibiti *UKIMWI* 2008/2012. Mtafahamu kwamba mkakati wa kwanza umeishia hivi sasa. Sasa tunaingia kwenye mkakati wa pili na unazinduliwa katika viwanja vya Nyerere *Square* kesho saa mbili asubuhi. Saa tatu asubuhi, afadhali kidogo! Saa mbili ilikuwa kidogo mtihani. Kwa hiyo, tangazo hili limeboreshwa sasa. Saa tatu

asubuhi kesho na ni Nyerere *Square,* Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. Nina hakika itakuwa ni fursa nzuri ya kukaa na wananchi na kujumuika nao ili kuzindua kwa kishindo awamu ya pili ya mradi ambao umefanikiwa sana, kudhibiti *UKIMWI.* Mtakuta kwenye *pigeon hall* kadi hizi, mfano huu. Huo ndio mwaliko wa ghafla hivyo karibuni sana. Pia Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, akiwa ni Mwenyekiti wetu wa *TAPAC,* amesisitiza tangazo hilohilo. Kule katika eneo la uwanja wetu wa maonesho katika jengo la utawala, yapo maonesho ya gazeti la Habari Leo.

Waheshimiwa Wabunge mnapopita pale basi basi vizuri kutembelea maonesho hayo, yanaendelea hivi sasa. Waheshimiwa Wabunge, kesho! Loh! Mambo yanagongana, sijui Waziri wa Fedha, hii semina labda ianze sijui saa nne au saa tano? Tufanye saa tano eeh? Asante sana.

Semina ya Wizara ya Fedha, kuhusu *The Financial Leasing Bill*, saa tano asubuhi ukumbi wa Pius Msekwa. Ni muhimu sana Waheshimiwa, kwa sababu Muswada huu tutaukabili baadaye. Sasa vizuri kujielimisha kuhusu maudhui ya *Financial Leasing* na maana yake ili kushiriki vizuri. Kwa hiyo, ni kesho saa tano asubuhi baada ya kuwa tumeshiriki katika uzinduzi wa awamu ya pili ya mradi wa *UKIMWI.*

Semina tena Jumapili, saa tano asubuhi tarehe 3 hapo hapo ukumbi wa Pius Msekwa, itakayohusu Miswada ya Sheria za Umeme na Biashara ya Mafuta. Miswada mingine tena miwili ambayo mizito sana, ina mambo mengi yanagusa wananchi na hisia zao na maisha yao. Tunakuombeni sana Waheshimiwa Wabunge, saa tano asubuhi siku ya Jumapili tarehe tatu, Miswada ya Sheria ya Umeme na Biashara ya Mafuta, hiyo ni semina ya pili. Leo kwenye orodha ya shughuli mtaona kuna Miswada miwili. Kuna ule ambao tulikuwa tunaendelea nao, wa Sheria ya kuzuia na kudhibiti virusi vya UKIMWI nchini. Unatazamiwa kukamilika, mara baada ya huo tutauzingatia Muswada wa Sheria ya Utalii wa mwaka 2007.

Ningeomba Waheshimiwa Wabunge wote ambao wangependa kuchangia katika Muswada wa Utalii wa 2007 waanze kuleta Mezani maombi ya kuchangia ili tujipange vizuri tuweze kuwatambua wakati tutakapoanza.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwaarifu rasmi kwamba siku ya Jumatatu nitakwenda Dar-es-Salaam kwa ajili ya safari ya Marekani. Nimealikwa na Bunge, Baraza la Wawakilishi (*House of Representatives).* Ziara yenyewe sio utalii, ingekuwa utalii wala nisingekwenda kwa sababu wakati huu sio wakati wa kufanya utalii. Lakini tunajenga mahusiano na Mabunge ambayo yana taratibu nzuri za demokrasia. Na kuna mipango ambayo tulikwishaianza kwa kuwasiliana na Nancy Pelosi kule Washington *DC,* ya kujaribu kujenga uwezo (*capacity building)* kwa Bunge letu. Kwa hiyo, pamoja na yote Spika atakayofanya ni mikutano ya kuweza kurudi na mipango itakayotusaidia. Lakini wakati huohuo ningependa kuwafahamisha tu kwamba Benki ya Dunia, ambayo makao makuu ni Washington *DC,* wamekubali kimsingi kutusaidia katika *Corporate Strategic Plan* ya Bunge 2008/2012. Mazungumzo yanaendelea, kwa hiyo, kwa yote hayo mawili niliona ni muhimu niweze kwenda. *(Makofi)*

Niseme tu kwamba mambo yote nyeti yatasubiri, nadhani mnanielewa. Yale mambo nyeti yataanza nikisharejea. Kwa hiyo, na hili ni elekezo kwa Naibu Spika, asije akakurupuka akaanza kuyavaa masuala ya *RICHMOND*, *EPA* na kadhalika. Hayo yatasubiri kwa sababu tutakuwa na wiki nzima ya kuyashughulikia. Sitakuwapo Jumatatu hadi Alhamisi, nitarejea Ijumaa Mwenyezi Mungu akipenda. Mtaona mara kwa mara namwomba Naibu Spika, anisaidie ili niweze kupata afueni ya haraka. Nikikaa zaidi ya saa moja mbili kunatokea kama hali ya ganzi na kuvimba kwa sababu nilifanyiwa operesheni ya goti. Kwa hiyo, inanibidi kwa ushauri wa madaktari nisikae sana kiasi hicho. Namshukuru sana Naibu Spika, ananisaidia na hakika kama mambo yatakwenda hivi ninavyoyaona mwezi wa nne nitakuwa katika hali yangu nzuri ya kawaida kabisa na Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* niwekee nafasi yangu na jezi kwa mwezi wa nne. *(Makofi/Kicheko)*

Baada ya kusema hayo, naomba sasa Mheshimiwa Naibu Spika aje ili nimkabidhi.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kazi ya Muswada wa UKIMWI. Katibu!

**Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vya UKIMWI Nchini wa Mwaka 2007 *[The HIV and AIDS (Prevention and Control) Bill, 2007]***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnapotoka muwe mnaacha maneno. Nina Wabunge sita watakaojadili Muswada huu. Tutaanza na Mheshimiwa Jenista Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Dakta Mahenge na Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o ajiandae. Yupo Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Peter Selukamba, Mheshimiwa Rosemery Kirigini na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Muswada ulio mbele yetu na kwa kweli ni Muswada muhimu sana. Lakini kabla sijaendelea kuchangia Muswada huu, naomba nitoe pongezi zangu kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Peramiho kwa Mheshimiwa Rais wetu, kwa nafasi aliyopewa ya kuwakilisha Bara letu la Afrika. Hiyo ni heshima kubwa sana kwa nchi yetu ya Tanzania, lakini ni heshima kubwa sana tuliyopewa sisi wananchi wote wa nchi hii Tanzania. Kwa hiyo, naomba apokee pongezi hizi kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Peramiho.

Vilevile Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi ya pekee kuwapa pole sana wananchi wa Jimbo la Kiteto, kwa kufiwa na Mbunge wao, tunamwomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira na awasaidie katika uchaguzi huu mdogo unaokuja kule

kwao.  Basi uchaguzi uishe kwa amani, amani ya nchi yetu na amani ya jimbo la Kiteto iendelee kubaki kama ilivyokuwa na hivyo kutufanya wote tutekeleze majukumu yetu ya kuendeleza nchi yetu ya Tanzania kwa utaratibu na kwa Kanuni ambazo zinatakikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba niipongeze sana Serikali kwa kutuletea Muswada huu mbele yetu.  Tunafahamu kabisa kwamba suala la *UKIMWI* ni janga kuu ambalo liko katika nchi yetu na ulimwengu kwa ujumla.  Lakini suala hili la *UKIMWI* lina matukio ambatanishi ya namna moja au nyingine.  Kwa ujumla ni kwamba kama hatutazingatia kushughulikia kwa marefu na mapana tatizo la *UKIMWI* basi tunaweza tukajikuta mipango yote ya maendeleo tuliyonayo itashindwa kufanikiwa na kufikia pale tunapotakiwa kupafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba wenzetu wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi kubwa na ninaomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana kwa yale ambayo wamekuwa wakiyashughulikia katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inapambana na janga hili la Ukimwi. Nawapongeza sana na ninawapa moyo kwa sababu kazi hii ni ngumu lakini ninaamini kabisa na hasa kiongozi wao anayeongoza Tume hiyo wanaweza wakatusaidia kusimamia hii mipango tunayoiweka ili kuhakikisha kwamba janga hili linaweza kuondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende katika Muswada wenyewe. Mchango wangu utakuwa katika namna mbili, kwanza nitapitia vifungu vya Muswada lakini pia nitakuwa na mapendekezo ya jumla katika suala zima hili la tatizo la Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unatueleza mambo mbalimbali ambayo yatafanyika ili kuhakikisha kwamba tunapambana na janga la Ukimwi. Sehemu ya tatu ya Muswada, nianze na kifungu kile cha 8, kinajihusisha moja kwa moja na suala zima la elimu kwa jamii na programu mbalimbali ambazo zitashughulikia mapambano haya dhidi ya Ukimwi.

Sehemu ya 8(1), kinazungumzia wajibu wa Wizara husika na wajibu wa watendaji wengine wa afya na wafanyakazi wengine wa sekta binafsi na sekta za umma pamoja na *NGOs* katika kutoa elimu na kuhakikisha kwamba taarifa mbalimbali zinazohusu suala hili la Ukimwi zinaifikia jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu kile cha kwanza, liko eneo ambalo linazungumzia wajibu wa hivyo vyombo nilivyovitaja kwamba vita-*disseminate information* zinazohusu Ukimwi katika jamii yetu. Katika eneo lile shughuli kubwa isiwe tu *dissemination* ya *information* zinazohusiana na suala hili la Ukimwi nafikiri pale tungeongeza pia ziwe na taarifa zinazohusu masuala haya ya Ukimwi lakini na matukio mengine ambayo yanaweza kupelekea kuongezeka ama kupungua kwa tatizo hili la Ukimwi. Kwa hiyo, eneo hilo lichukue haya yote isiwe ni taarifa zinazohusu janga lenyewe tu la Ukimwi lakini yapo matukio ambayo yanaweza kupelekea angalau labda kupambana ama kupunguza tatizo hilo la Ukimwi. Kwa hiyo, kwenye ku-*dissiminate* hizo *information* pia isizingatie tu zile *information* zinazohusu tatizo lenyewe kwa ujumla

lakini kama yapo mambo ambayo yanaweza yakatupelekea katika kuondokana na tatizo hilo, nafikiri pia tungeongeza kitu cha namna hiyo ili liwe ni eneo mojawapo la kulifanyia kazi ama la kulitolea taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tisa, katika eneo hilo hilo la *part three* inaonyesha wajibu wa utoaji wa elimu katika maeneo ya kazi na kwamba utafanyika. Ukiangalia katika ule Muswada, ukurasa wa 38, eneo hilo linazungumzia pia *distribution of condoms and support to people leaving with HIV/AIDS*. Sasa katika maeneo ya kazi, ni kweli kabisa labda *distribution* ya hizo *condom* ni muhimu katika ku-*support* watu *leaving with HIV* lakini kwa nini tusiongeze kwamba suala hilo la ugawaji wa *condom* lisiishie katika eneo tu la ku-*support people leaving with HIV* bali hata wale ambao hawana Ukimwi. Kwa nini tusiongeze kwamba na wao pale katika maeneo ya kazi wasaidiwe maana hilo ni eneo la elimu? Wasaidiwe kugawiwa *condom,* wakielimishwa tu bila kugawiwa *condom* nadhani litakuwa siyo suala la msingi. Nafikiria tungeongeza tena pale kwamba hiyo, *support to people leaving with HIV/AIDS* iwe pia hata kwa wale ambao hawaishi na Virusi hivyo vya Ukimwi na wao wangehusishwa katika maeneo yao ya kazi wakagawiwa hizo *condom* katika utaratibu ambao unaonekana unafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 16, kinahusu usiri katika kutoa matokeo ya upimaji wa virusi vya Ukimwi. Sina tatizo sana na kifungu hicho lakini shida yangu kubwa sijui tutatumia kanuni gani ya usiri kwa sababu usiri ni haki za binadamu, ukabakia kwa mtu mwenyewe. Tatizo langu kubwa ni kanuni ipi ya usiri itatumika kuwalinda wale watu ambao labda ndiyo watakaokuwa wanamhudumia mgonjwa huyo? Kama usiri utabakia katika kutoa matokeo ya vipimo unakuta wananchi wetu wengi katika maeneo ya vijijini wasipojua tatizo la mgonjwa na tunajua kabisa tatizo la Ukimwi linakuwa na maambukizi ya namna moja au nyingine wakati wa ku-*care* au wakati wa kum-*support* yule mgonjwa mwenyewe, kama familia ama jamii inayomhudumia mgonjwa yule haitakuwa imejua kiini na tatizo la yule mgonjwa na wakashindwa kumhudumia kwa kutumia labda *protective gears* ambazo zinatakiwa zitumike, naona hapa labda tunaweza pia tukasababisha kwa namna fulani Wauguzi nao wanaweza wakajikuta wanapata maambukizo bila kujua lakini kwa haki za binadamu ni kweli kila mtu matatizo yake yanatakiwa yabakie kuwa siri. Sasa sijui kanuni gani itatumika au itatungwa baada ya Sheria hii ili kuweza kuwasaidia na kuwaelekeza wale ambao watakuwa wanamhudumia huyu mgonjwa ili na wao pia wasiweze kuathirika kutokana na tatizo hilo na hasa katika eneo hilo ambalo nimelizungumzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya Muswada, inaeleza suala la kutoa elimu. Kifungu cha 7(2), kinaeleza jinsi ya kuwashirikisha vijana katika kupata elimu. Naipongeza Kamati kwa sababu iliona kwamba suala hili la elimu lisiishie kwa vijana tu lakini liende pia hata kwa akina mama na makundi mengine maalum kama walemavu na watu wa namna hiyo. Lakini tunatengeneza mkakati upi nadhani labda tungeongeza jambo jingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua Muswada wetu katika maeneo hayo yote umeshughulikia sana suala la tiba, suala la kupima na vitu vya namna hiyo lakini hatujagusa sana *causes* zinazotupelekea kupata janga hili la Ukimwi. Kwa mfano, yako

maeneo mengine hakuna *entertainment* nyingine yoyote inapofika jioni zaidi ya *sex*, hakuna *TV*, hakuna ngoma, ikishafika usiku, giza likiingia watu wanaona *alternative* ya *entertainment* iliyobakia katika maeneo hayo ni aidha iwe *sex* halali au ama *sex* ambayo siyo halali. Nadhani Muswada huu pia ungelenga kwa mfano kundi la vijana ambao ndiyo waathirika wakubwa hivi inapofika jioni ni kweli wanahitaji wapewe elimu tu au yako mambo mengine wakipewa yatawasaidia kuondokana na tatizo hili la ngono na kupelekea kwenye tatizo la Ukimwi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Muswada huu hasa katika kipengele hiki ambacho kimegusa makundi maalum, kila kundi lingejaribu kuwekewa mkakati maalum aidha wa kuzuia, kutibu ama wa elimu kulingana na mazingira yanayoligusa kundi lenyewe kwa ujumla. Yako mambo mengine ambayo labda tutaishauri Serikali kwa mfano mpango huo wa umeme vijijini ni muhimu watu wakipata umeme wanaweza wakatengeneza *entertainments* nyingine za ziada na vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tume-*concentrate* sana katika mfumo wa utoaji elimu ambao unahusisha vyombo hivi vya habari na magazeti lakini sijaona mahali ambapo tumesisitiza kutumia ngoma zetu za asili, maigizo na ile michezo yetu ya asili iliyokuwa inatumika katika maeneo yetu ya vijijini. Michezo ile ingesaidia sana kuliko hivi vyombo vingine ambavyo wakati mwingine hata kwenye maeneo ya vijijini, havifiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri zile Sheria ambatanishi ambazo ziko katika nchi yetu ambazo zinajihusisha na masuala mengine lakini yanagusa masuala ya afya, nazo zingeangaliwa kwa haraka ili kuufanya Muswada wenyewe uende vizuri. Kwa mfano, tuna Sheria ambayo inazungumzia masuala ya *Nurses and Midwife Registration Act* na zipo *Caps* nyingine ambazo tunakiwa kuzingalia ili ziweze kuendana na malengo ya kupitisha Muswada huu mfano *Private Hospital Regulations* ambayo ilitungwa mwaka 1996 na nyingine nyingi tunatakiwa kuzipitia ili ziweze kuoana na Muswada ambao tunauzungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimalizie kwa dakika zangu hizi mbili au tatu kwa kuzungumza mambo ya jumla. Masuala ya Ukimwi ni makubwa ambapo asilimia 93 ya Watanzania, kwa taarifa tulizonazo, hawajaathirika na asilimia saba ndiyo walioathirika. Kwa hiyo, kwa kweli nadhani tunatakiwa kuongeza nguvu kuwatunza na kuwahudumia, kutowanyanyapaa, kuangalia wajane na yatima ya hawa asilimia saba ambao wamekwishakuathirika. Lakini hawa asilimia 93 ya Watanzania ambao hawajaathirika nafikiri Wizara na Serikali yetu ijitahidi kuhakikisha kwamba wanaendelea kubaki ama kuongezeka katika kundi la ambao hawajaathirika na wale asilimia saba kwa kweli juhudi zote ziwekwe katika kuwalea na katika kuwahudumia kwa namna moja ama nyingine na pia kutowanyanyapaa katika tatizo hili la Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kusema kwamba suala zima la kupima Ukimwi kwa hiari liendelee kutiliwa mkazo. Ni suala jema, ni heri kupima ukajulikana unaumwa, ukapata dawa na ukaongeza maisha, kuliko kutokupima halafu usijulikane kama unaumwa na watu wakakunyima dawa bila kukusudia na wewe ukapoteza maisha kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napongeza sana zoezi hili na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa kuzindua kampeni maalum ya upimaji wa hiari na naomba kwa kweli Watanzania tuendelee kumuunga mkono na tuendelee kutoa elimu kwa wananchi wetu wajitahidi kuelewa umuhimu wa kupima kwa hiari ili tuweze kupunguza madhara haya ya Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema, nilipokuwa kwenye ziara yangu katika Kijiji cha Magagula katika Jimbo langu la Peramiho, Kata ya Magagula, mama mmoja aliniagiza nitakapozungumza Bungeni nitoe salaam zangu za pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Tanzania ni nchi moja miongoni mwa nchi chache sana ambazo Serikali yake inatoa dawa za Ukimwi bure kwa waathirika na hivyo imeweza kuwaokoa wagonjwa wengi sana waliokuwa katika hatihati ya kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yule mama ameniomba niishukuru sana Serikali yetu. Aliniambia alikuwa na binti yake wa pekee ambaye alitaka kufa lakini kwa kupitia dawa hizi ambazo zinagharimiwa na Serikali yetu, binti yake sasa ni mzima, anaweza kufanya kazi zake kama kawaida na anaweza kushiriki shughuli zote za maendeleo katika eneo analoishi na hasa katika kumhudumia mama yake. Mama yule alitoa pongezi hizo na mimi nakubaliana naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono sana Serikali yetu katika jambo hili na ninaipa moyo iendelee kuona suala la kuwahudumia wagonjwa wa Ukimwi, yatima, wajane lakini suala zima la kupambana na ugonjwa huo ni suala la kimsingi na linalohitaji nguvu ya pamoja ndani ya Serikali yetu, Wabunge, Viongozi wengine na wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu lakini niseme kwamba ninauunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kujumuika na wenzangu kujadili Muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya wananchi wangu wa Makete, kutoa salamu za rambirambi kwa wananchi wa Kiteto kwa kupotelewa na Mbunge wao mpendwa, Mheshimiwa Benedict Losurutia.

Mheshimiwa Naibu Spita, tatu, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana, ndugu yangu, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, yeye pamoja na Naibu wake na Wizara yake kwa ujumla kwa kuuleta Muswada huu bila kusahau pia kuishukuru sana Kamati ya Huduma za Jamii walioshughulikia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwenda moja kwa moja kwenye Muswada na hapa naangalia sehemu ya tatu ambayo inazungumzia suala la *Public Education and*

*Programs.* Hapa Wizara inasisitiza kwa kushirikiana na wadau na taasisi zake mbalimbali kuweza kuandaa mikakati ya kuzuia unyanyapaa na ubaguzi kuhusu hawa wenzetu ambao wameathirika. Nadhani hapa mkazo zaidi pamoja na kuwa kwenye *programs* za kutoa elimu lakini vile vile ungekuwa kwenye *publicity* kwa maana kuwa wawazi kwenye suala zima la maambukizi ya Ukimwi. Kwa mfano tufike mahali tuwe wazi kutoa sababu za vifo vya watu mbalimbali kama amefariki kwa Ukimwi basi tuseme amefariki kwa Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nadhani ipo haja ya viongozi wa ngazi za juu pale anapogundua kwamba yeye pia ni mwathirika, akiliweka wazi linasaidia sana kuweka hali halisi ya suala la Ukimwi kwenda kwa wananchi kwamba ni sawa na ugonjwa wa kawaida. Kwa mfano Afrika Kusini, Jaji Edwin Camelon aliwahi kutangaza kwamba yeye ameathirika kitu ambacho wananchi waliona ni hatua nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunaona mfano mzuri wa kiongozi mkubwa kama Nelson Mandela ambaye yeye mwaka 2005 alitoa sababu za kifo cha mtoto wake kwamba ilikuwa ni kwa sababu ya Ukimwi. Napenda labda kumnukuu alivyosema, alisema:-

*"let us give publicity to HIV/AIDS and not hide it because that is the only way to make it appear like a normal illness".*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani *publicity* ni suala muhimu sana ili kuondoa huu usiri ambao unajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye sehemu ya tatu ambayo iko ukurasa wa 37, kipengele cha 9 ambacho kinaelezea vile vile nia ya Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali na ambazo siyo za Serikali kuona kwamba wana-*establish programs* kwenye sehemu zao za kazi. Hapa napendekeza kwamba unaposema "*every employer in consultation with the Ministry, shall establish and coordinate work place programs*", hapa humuwajibishi na hiyo *program* anaweza aka-*establish* na asiitekeleze kwa sababu atasema hana hela. Kwa hiyo, napendekeza hapa suala iwe ni ku-*establish policy*, kwamba kila mahali pa kazi, kila kampuni iwe na sera ya *HIV/AIDS* ambapo itaeleza haki ya wafanyakazi wanapokuwa wameugua, haki ya wafanyakazi wanapokuwa wamepata ajali, haki ya mfanyakazi ambaye ameathirika na Ukimwi anapougua, kwamba haina tofauti na mtu mwingine wanapohitaji ama likizo ama kwenda kutibiwa lakini vile vile nadhani hili lingekuwa wazi kwenye sehemu za kazi kwamba mtu anapokuwa ni mwathirika haimpunguzii haki ya yeye kuajiriwa kwa sababu utaona taasisi nyingi mtu anapotaka kuajiriwa huwa anatakiwa afanye *pre-employment testing*. Sasa hii ni aina moja ya unyanyapaa. Kwa hiyo, tunadhani kwamba ni vizuri haya mambo yakawekwa vizuri kama shirika lina sera yake ya *HIV/AIDS*, itaweka wazi kwamba wao wanatoa haki sawa kwa kila mtu na ni haki ya mfanyakazi kuwa na usiri wake na wala halazimishwi na mwajiri kusema *status* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda ukurasa wa 45, ni suala zima la misaada. Katika sehemu hii, imesemwa kwamba wale ambao hawatafikisha zile *fund* kama vile

*individuals,* watu binafsi na vile vile Sheria ya Makampuni inasema kwamba kwa mtu binafsi ambaye amekula zile fedha au hakufikisha ule msaada, basi anaweza akapata kifungo lakini haisemi kwamba kampuni inaweza ikapewa kifungo. Kwa hiyo, napendekeza kwamba adhabu ya kifungo iende pia kwenye makampuni kwa sababu makampuni yana uongozi, yana Wakurugenzi ambao wanaweza wakawajibika na wakafikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kama tunaweza tukatoa adhabu au faini ya shilingi milioni tano tunakuwa tumedhani kwamba ule wizi utakuwa umefanyika chini ya milioni hizo tano au unaolingana na milioni tano lakini kama huo msaada ulikuwa unazidi shilingi milioni 150 au 200 ukamtoza huyu mtu shilingi milioni tano, inaweza kuwa ni tozo ya kawaida kwamba kwanza hawezi kwenda kufungwa kwa hiyo atajua kwamba atatozwa faini ya shilingi milioni tano zingine milioni 145 atakuwa ameshazifanyia kazi lakini kama kungekuwa na *issue* ya kufilisi, ingekuwa ni suala zuri na muafaka zaidi. Kwa hiyo, napendekeza kwamba ni vizuri basi kuwe na uwezekano wa kufilisi mali zinazolingana na hela iliyopotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napendekeza kwamba suala la uwajibikaji wa kufikisha misaada kwa walengwa lisiwe tu la taasisi ambazo siyo za Serikali, liwe ni la taasisi hata za Serikali kwa sababu tumeshuhudia Halmashauri zinapewa hela nyingi sana kwa ajili ya shughuli za Ukimwi na Halmashauri nyingi zimekuwa hazifikishi hela hizo kwa walengwa, nako huko kuna ubadhilifu ambao unatakiwa ufuatiliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakwenda ukurasa wa 39 ambapo limeongelewa suala la upimaji wa hiari. Nadhani changamoto tuliyonayo hapa kwenye upimaji wa hiari, tuna upande mmoja kuhamasisha watu wakapime lakini tuna upande wa pili, ni namna gani Serikali imejiandaa kuwasaidia wale wote watakaokuwa wameathirika na *CD4* zao zimepungua. Nadhani tatizo kubwa lipo upande huu wa namna gani tumejiandaa na huu upande ndiyo unaofanya idadi ya watu wengi kutokujitokeza kwa sababu anajiuliza kwamba sawa, nikipima nikijulikana hali iliyopo sasa hivi ni kwenda kwenye utaratibu uliopo ambao unatumika kwenye Halmashauri wa waathirika kupewa dawa kwenye dirisha kwa foleni. Nadhani pale siyo watu wote wanaoweza wakakubali hilo kwamba tunasema ni siri kwenye majibu lakini kwenye kupewa ile huduma unakwenda kwenye foleni ya watu wote, watu wanaweza wakajua siri yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni lazima Serikali ijiandae kuona kwamba sehemu ya pili inatekelezeka yaani inakuwa na uwezo mkubwa wa kupata hizo dawa za *ARVs* ambazo zitasambazwa sehemu nyingi na tufike mahali kuwe na utaratibu wa kutoa hata elimu *(simple knowledge)* ya namna ya kutumia dawa hizo kwa kutumia hata Madaktari ambaye anaweza kuwa ni *personal friend* wa huyo mtu au mtu wa karibu bila hata kwenda hospitalini kama tulivyofanikiwa kutoa elimu ya matumizi ya *condom* na kwamba mtu anaweza akaikuta chooni akaichukua na akaitumia kwa siri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hata kwenye dawa, tufike mahali tufanye hivyo na tukifanikiwa hilo, idadi ya wapimaji itaongezeka sana kwa sababu atajua

kwamba naweza nikaenda mahali fulani nikazipata hizo dawa bila matatizo. Kwa hiyo, hapa naongelea kuongeza sana vituo vya *VCT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii, kabla sijamaliza, kuishukuru sana Serikali. Kama mnavyojua, Wilaya yangu ni moja ya kati ya Wilaya ambazo zimeathirika na zina vijana wengi, watoto yatima ambao ni kweli wamekuwa wakati mwingine hawapati misaada lakini pamoja na hayo yako makampuni, taasisi za binafsi zinazosaidia sana. Naomba nizishukuru sana taasisi zote pamoja na shukrani zangu *special* kwa Waziri wa Afya ambaye kwa hakika ametusaidia sana Makete kwani hivi ninavyoongea Makete tulikuwa na vituo vitatu vya kutolea *ARVs* lakini kwa mwaka jana tumeongeza vituo vingine vitatu. Kwa hiyo, nina hakika tukifika mwaka 2010, tutakuwa na vituo vingi na mkijua jiografia ya Makete ni milima na viko mbalimbali sana kwa hiyo, hii itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani zangu kwa jirani yangu hapa, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ambaye anasimamia *TAHEA* na wametoa misaada kwa watoto wetu yatima katika kata nyingi za Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada ulioko mbele yetu.

Kwanza, kabla sijachangia, naomba kwa niaba ya wanawake wote wa Mkoa wa Iringa, nitoe salaam zangu za rambirambi kwa wananchi wa Wilaya Kiteto kwa kupotelewa na Mbunge wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Mchungaji Dr. Rwakatare, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge na kuungana na wanawake katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Wabunge wote wa Bara la Afrika Wanaopambana na Ukimwi, kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Bara la Afrika. Nina uhakika kabisa, Umoja huu umepata jemedari katika mapambano dhidi ya Ukimwi, nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze wana harakati wote nchini katika mapambano dhidi ya Ukimwi zikiwemo taasisi mbalimbali na watu binafsi na wakiwemo watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi kwa sababu wao ndiyo wametusaidia kuweza kufika hapa tulipo.

Nawapongeza sana wana harakati wote nchini, wakiwemo Wabunge wote wanaopambana na Ukimwi ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano chini ya *TAPAC* na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa mmojawao. Nawapongeza Wizara ya Afya na Tume ya Kudhibiti Ukimwi *(TACAIDS)* kwa kazi kubwa waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko katika miaka 25 tangu mgonjwa wa kwanza wa Ukimwi alipogundulika hapa nchini. Tumeshuhudia mambo mengi yakitendeka hapa nchini na leo Bunge au nchi ya Tanzania inaweka rekodi ya kuwa na Sheria ya Ukimwi na kufanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache katika Bara la Afrika zenye Sheria ya Ukimwi. Naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nizungumzie Muswada wenyewe, kipengele cha 2 kwenye suala linalozungumzia utoaji wa elimu kwa jamii *(public education and programs on HIV/AIDS)*. Katika kipengele hiki, suala la jinsia halijaonekana kwa uwazi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango mkubwa unaotolewa na wanawake na watoto wa kike, haujaonekana kwa uwazi kwa sababu tunaelewa kwamba wagonjwa wengi wanatoka kwenye huduma za afya hospitalini wanarudishwa nyumbani na wanaowaangalia wagonjwa hawa ni wanawake na watoto wa kike lakini Muswada huu haujawazungumzia kwa uwazi, suala la jinsia limegusiwa tu kijuu juu lakini halijaangalia mchango ambao wanautoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni wakati wa kuangalia, tunafanya miradi mbalimbali vijijini, huwa michango inatambuliwa, hata tunavyojenga shule wanasema Serikali imechangia kiasi hiki na jamii imechangia kiasi hiki, wanaithamanisha kwa fedha. Sasa ni wakati ambapo tunahitaji kuanza kuthaminisha zile gharama ambazo zinatolewa kwa watoa huduma nyumbani wengi wao wakiwa wanawake na watoto wa kike ili tujue ni kiasi gani ambacho wanagharamia, mchango wao ni muhimu kutambulika katika Muswada huu. Hii pia itasaidia kuhamasisha wanaume pia kushiriki katika kuhudumia wagonjwa nyumbani, Sheria haijazungumzia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda Kifungu cha 15(4) ambacho kinasema kwamba akina mama wajawazito wanaokwenda kupima *clinic* basi washauriwe kupima na virusi vya Ukimwi. Naomba sasa tuangalie pia kuhamasisha wanaume ili kwenda na wake zao *clinic* kwa sababu mama anakwenda *clinic* anashauriwa kupima virusi vya Ukimwi, anapima, anapopima kwenda kutoa majibu nyumbani inakuwa kazi na wengine wanapigwa, wengine wanafukuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri pia Sheria ingeangaliwa ili uwepo uhamasishaji wa kuhakikisha kwamba mama mjamzito anapoenda kupima na ashauriwe kwamba apimwe Virusi vya UKIMWI basi pia awe anaenda na mume wake ili wote kwa pamoja waweze kupima na mfano mzuri umetolewa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipoenda kupima Virusi vya UKIMWI mbele ya wananchi wote wa Tanzania hakwenda peke yake alienda na mke wake, Mheshimiwa Spika alifanya hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya hivyo. Kwa hiyo, nafikiri wote tuendelee kuhamasisha ili akina mama waweze kwenda pamoja na waume zao na Sheria pia izungumzie suala hilo na kushauri waume zao pia washiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 22, kinasema kwamba aliyepatikana na Virusi vya UKIMWI atoe taarifa kwa mwenzi wake. Ni vizuri lakini ningeomba Sheria pia iweke tahadhari kwa wale ambao labda anapoenda kutoa zile taarifa kwa mwenzi wake anafukuzwa au kupigwa kama nilivyoeleza mwanzoni na hata mara nyingine kuuawa, je, Sheria inalizungumzia vipi suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia suala hili, naomba niseme kwamba wiki moja iliyopita, nimemshuhudia mama aliyeletwa hospitali akiwa mgonjwa yeye na mtoto wake lakini alitelekezwa, mama akalazwa hospitali, akafariki ikabidi tuchukue jukumu la kuzika. Baada ya muda mama alipofariki tunarudisha maiti, ofisi yangu ikabidi ishughulikie kurudisha maiti kijijini na pale kijijini tulikuta baba amehama, amefunga nyumba na ameondoka kwa sababu tu yule mama alionekana anaumwa UKIMWI. Sasa je, Sheria inachukua mkondo gani kwa aidha mwenzi au mume anayeweza kufanya vitendo vya namna hii? Ninaomba pia vitendo hivi viangaliwe au pale mama anapoenda kutoa taarifa au baba anapoenda peke yake pia akakutwa ana Virusi vya UKIMWI ambapo mengi haya hayawatokei wanaume wengi wanaotokewa ni wanawake, ndio maana nimesema suala la jinsia hapa halijazungumzwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kondomu, limezungumziwa suala la usambazaji lakini matumizi yake hayajazungumziwa kwa mfano jinsi ya kutupa kondomu zilizotumika bado ni tatizo katika jamii, tunakuta kondomu zimezagaa na watoto wanatumia kama Maputo. Ninaomba pia Sheria izungumze utupaji wa kondomu hizi ili kunusuru watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kipengele cha 25, kinachohusu kupewa dawa za *ARVs.* Ninaishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya ya kuhakikisha wagonjwa ambao wamefikia kupewa dawa hizo wanapewa dawa bila kulipia. Hii ni hatua kubwa sana na wananchi wengi wanashukuru na kuipongeza Serikali kwa hatua hii. Lakini kuna wale ambao hawawezi kumudu chakula, tunaelewa kwamba wengi wao wanakuwa wana afya duni na zile dawa zina nguvu sana, Serikali ingeangalia uwezekano wa kuwapatia chakula angalau ile miezi mitatu ya mwanzo hadi miezi sita wakati hali yao inapoimarika na kuweza kufanya kazi zao kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 26, kimesema kwamba wale waliambukizwa wanaweza pia kupewa huduma kwa mfano watoa huduma wakiambukizwa, wafanyakazi wa hospitali, wanaweza kuangaliwa lakini hatujawaangalia watoa huduma nyumbani! Kwa mfano kama mtoa huduma wa nyumbani alikuwa hana Virusi vya UKIMWI na kwa vile wagonjwa wanarudishwa nyumbani akaambukizwa wakati wa kutoa huduma, je, yeye anaangaliwaje na Serikali? Je, aachwe tu au Serikali inachukua hatua gani ya kuweza kumpa dawa za kuweza kujikinga? Hilo pia ninapenda Sheria hii iliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la wale wanatoa huduma hasa wazee, hawajazungumziwa chochote humu, wale wanaolea watoto yatima, je, *safety net* gani zimewekwa, wanahudumiwaje hao? Hawa ni wazee lakini wanatunza watoto yatima, Sheria pia haijawazungumzia, naomba pia kupata maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia kipengele cha 32 kinazungumzia misaada mbalimbali ambayo watu wenye virusi wanaweza kupewa lakini hakijaangalia utoaji wa *free legal service,* je, wale wenye virusi ambao hawawezi kujitetea, wagonjwa wasioweza kujitetea, ninafikiri ni wakati sasa Serikali kuwapa huduma za kisheria bure, msaada wa kisheria bure, Serikali iwasimamie kwenye kesi zao kwa sababu watu wengi wakiwaona wale wagonjwa wanafikiri watakufa kesho, wanangojea wanapofariki na wanakosa haki zao. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwapa msaada wa kisheria bure na pia kesi zao ziharikishwe, kuwepo na *first track* kwa hawa wagonjwa na hasa wajane ambao wanakosa haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kwamba mapambano dhidi ya UKIMWI yatafanikiwa pale ambapo patakuwa hakuna wasiwasi ndugu, marafiki wanapokuwa wote kwa pamoja wanashirikiana kuwahudumia wagonjwa na tunajua kwamba asilimia 93 ya Watanzania hawajaambukizwa na Virusi vya UKIMWI na ili waweze kuondokewa na woga ni pale haki zao za msingi zitakapokuwa zimeangaliwa. Kwa hiyo, naomba huduma za afya ziboreshwe na vitendea kazi pia vipatikane kwa watoa huduma hospitalini ndio maana kunakuwepo unyenyepa kwa sababu na wenyewe wanaogopa kwa sababu hawana vitendea kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendea kazi vitakuwepo tu vya kutosheleza kama Serikali itaongeza Bajeti ya Wizara ya Afya kufikia asilimia 15 kama walivyokubaliana kwenye mkutano wa Abuja ambao uliomba Wakuu wa Nchi wote waweze kuhakikisha kwamba Bajeti ya Wizara ya Afya inafikia asilimia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda nirudie tena kuipongeza Wizara ya Afya kwa kazi nzuri waliyofanya, ninaipongeza Tume ya Kudhibiti UKIMWI lakini naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza kipekee Waziri wa Afya ambaye kwa muda wote toka mwaka 2001 amekuwa Mweka Hazina wa *TAPAC* kwa kazi nzuri anayoifanya na ninampongeza pia Naibu Waziri wa Afya ambaye ndiye aliyekuwa Katibu Mkuu wa kwanza wa *TAPAC*. Nina hakika wanatumia uzoefu huo katika mapambano dhidi ya UKIMWI na nina uhakika Sheria hii itaangaliwa vizuri na itatekelezwa kwa kushirikiana na wadau wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufuatana na Sheria hii kwa vile Tume ya Kudhibiti UKIMWI ilianzishwa kabla ya Sheria ya UKIMWI haijakuwepo, ni wakati muafaka sasa Serikali kuleta marekebisho ili Sheria iliyoanzisha Tume ya Kudhibiti UKIMWI iweze kubadilisha baadhi ya vipengele ili viweze kuendana na Sheria hii mpya ambayo tunaijadili leo na hatimaye itapitishwa kuwa Sheria na kuweka rekodi ya nchi yetu kuwa mojawapo ya nchi mahiri katika mapambano dhidi ya UKIMWI katika Bara la Afrika. Ninapenda niwaambie Wabunge wenzangu, niwaombe tuipitishe kwa kauli moja kwa sababu sisi Bunge la Tanzania ndio kinara katika mapambano dhidi ya UKIMWI katika nchi za *SADC* na Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, ni Mwenyekiti wa Mtandao wa Kupambana na UKIMWI kwa Wabunge katika Bara la Afrika na Tanzania, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kupambana na UKIMWI katika Bunge la *SADC*, ndio maana akasema sisi tuko katika mstari wa mbele Bara la Afrika na *SADC*. Tunaendelea sasa ni Mheshimiwa Yono Kevela.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii ya kipekee kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mada hii ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika, wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi kwa kweli wanakupongeza sana na mimi ndio mwakilishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Kiteto kwa kupotelewa kwa Mbunge wao. Kwa kweli wananchi wangu wanawapa pole sana Wanajimbo la Kiteto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye Muswada uliopo mbele yetu. Nichukue nafasi ya kipekee kuipongeza sana *TACAIDS* na wadau wote kwa jinsi wanavyochapa kazi. Kwa kweli mimi binafsi, ninaona hawana tatizo kabisa. Kwa kweli wanatufurahisha sana na Jimbo la Njombe Magharibi wanalikumbuka sana, hasa Dr. Magoti yule Mratibu wa UKIMWI pale Iringa, tunamshukuru sana, amepeleka misaada mikubwa pale Ilembula. Kwa hiyo, wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi, wanakushukuru sana kwa ile misaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba kweli huu Muswada umechelewa ilitakiwa uje mapema sana hapa Bungeni kwa sababu tayari athari zimekuwa kubwa sana na tayari Serikali imeshapata hasara kubwa kweli kweli. Kwa kweli niseme hivi, umechelewa lakini kuchelewa hakumaanishi kwamba hatuwezi kupitisha Muswada huu, umekuja kwa kuchelewa ilitakiwa uje mapema zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nije kwenye hoja ambayo niliwahi kuizungumza hapa Bungeni kuhusu waeneza UKIMWI kwa makusudi. Hili suala kwa kweli nilishalizungumza kwamba ingekuwa busara sana ingetungwa Sheria kali sana mpaka nikadiriki kusema kuwepo na utambulisho kabisa kwamba huyu ni mueneza virusi vya UKIMWI kwa makusudi, hii ingesaidia sana watu kuogopa, hili ni tatizo. Niseme kwamba hawa waeneza virusi kwa makusudi nawalinganisha na wauwaji, ni sawa sawa na wabakaji, hali ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavipongeza sana Vyombo vya Habari kwa mfano Gazeti la Majira ingawaje kuna Mwandishi mmoja alininukuu vibaya, hakunielewa lakini ninalipongeza sana Gazeti la Majira hasa Mhariri Mkuu jinsi alivyorekebisha nilivyokuwa ninamaanisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, alielezea vizuri kwamba alikuwa anamaanisha waeneza UKIMWI kwa makusudi siyo wale wagonjwa wote wa UKIMWI na wala siyo kweli kwamba waathirika wote wa UKIMWI wawekewe alama usoni, siyo kweli, alifafanua vizuri na ninapenda nieleweke kwamba sikumaanisha hivyo, nilichokuwa ninamaanisha ni wale wauwaji, wanaoeneza virusi vya UKIMWI kwa makusudi, wanasema sifi peke yangu na inafikia hatua kuna sehemu zingine wanatoa na fedha nyingi wanasema sifi peke yangu hii fedha ikakusaidia upate sanda. Kwa hiyo, inasikitisha sana na inasikitisha sana kwa mwathirika na inasikitisha sana kwa jamii na nikisema jamii nikimaanisha hata Taifa lenyewe linapunguza nguvu kazi yaani rasilimali watu kwamba wataalam wanapotea, Walimu wanapotea na wataalam mbalimbali kama Madaktari wanapotea, kwa hiyo ndio nilikuwa ninamaanisha hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nataka nizungumzie kuhusu suala la hawa waathirika, hawa waathirika wa UKIMWI siyo wote nilikuwa ninamaanisha wale wanaoeneza kwa makusudi, ninarudia tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwanaharakati niko pamoja nao katika kupambana, kuzuia na kuthibiti UKIMWI, nina kituo cha kulelea watoto yatima, ninawasaidia wajane na kama hawa watoto yatima ninawasaidia hata kuwasomesha Elimu ya Sekondari, Elimu ya Msingi na hata Chekecheka. Kwa hiyo, ninasikitika sana sana nilivyokosa kueleweka. Kwa hiyo, mimi ni mwanaharakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina kituo cha kulelea watoto yatima na bahati nzuri wale walioathirika waliojitokeza, wanaharakati wakasema kwamba ni vizuri tufanye mkutano nao, tukafanya nao mkutano pale Dar es Salaam walikuwa zaidi ya 100, walinipongeza sana na waliniunga mkono juu ya hili suala la hawa wanaoeneza virusi kwa makusudi kwamba hawa watu ni watu wa hatari hata wao wenyewe wanawapiga vita sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwa kweli kuwapongeza sana wale tuliokaa kikao cha pale Dar es Salaam. Vile vile nichukue nafasi hii kukishukuru kikundi cha watu waliojitolea na kusema kwamba wao wameathirika cha Faraja, kiko pale Ilembula, kwa kweli waliniunga mkono sana.

Vile vile nichukue nafasi hii kutoa shukrani kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Njombe Magharibi kwa kunielewa. Yule Mwandishi wa Habari aliyeandika kwa kuninukuu vibaya, kwa bahati nzuri walinihoji na nikawaelewesha na wanajimbo, hasa wapiga kura wangu wa Njombe Magharibi wakasema kwa kweli kama suala ndio hilo nafuu Sheria ije haraka sana kwa sababu hawa watu watatumaliza. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wapiga kura wangu wa Njombe Magharibi na sehemu mbalimbali ambao waliniunga mkono katika hoja ambayo nilitoa mwezi Novemba hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kuhusu suala la wagonjwa wa UKIMWI. Ni kweli tunapitisha hii Sheria lakini kwa kweli bado hawa waathirika wa UKIMWI

wana mateso makubwa sana kwa sababu huu ugonjwa wa UKIMWI siyo kwamba njia zinazoenezwa ni moja, wengine wanapata kwa njia ambazo si zile ambazo watu wengine wanasema ni za kujitakia, watu wengine wamepata UKIMWI kwa bahati mbaya. Sasa hawa wanatakiwa upendo na wanatakiwa wasinyanyapaliwe kabisa. Kwa hiyo, ninatoa wito kwa wananchi wote wa Tanzania na sehemu zingine kwamba tuwe na upendo wa kutosha kwa watu hao na tutoe misaada mbalimbali na kwa Serikali isiishie kutoa dawa zile za *ARVs* tu, tutoe ruzuku kwenye chakula, lishe. Mbona Serikali inatoa ruzuku kwenye mbolea? Sasa hawa wenzetu ambapo ni kundi dogo tu kwa nini tusiwape ruzuku ya lishe? Hii ingesaidia sana kuwaongezea maisha na kuchangia pato la Taifa kwa sababu ile ni nguvu kazi tena wengine ni wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali iangalie hilo ili kupata unafuu wa misaada mbalimbali ikiwezekana wapunguziwe hata bei ya mbolea ya ruzuku wapewe walau kwa bei nafuu na hata kwenye mahoteli vyakula wapunguziwe au kwenye vyombo vya usafiri kama zilivyo nchi zingine, wapewe unafuu kwamba huyu mtu mnaelewa ameathirika ana cheti chake, apewe unafuu isiwe inaonekana ni sawasawa na mtu ambaye hajaathirika, ninaomba sana Serikali iliangalie suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nizungumzie kuhusu suala la hawa watu walioathirika, tujitokeze kwa wingi kuwasemea, kuwatetea, kuwasaidia kwa hali na mali kwa sababu hawa watu ni kundi dogo lakini sasa maambukizo yamezidi kuenea, hawa waeneza Virusi vya UKIMWI kwa makusudi inakuwa ni tatizo kubwa kweli. Kwa hiyo, ni vizuri hawa watu tutafute njia zozote za kuwasema mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba wadau mbalimbali, wafadhili tusiache mzigo kwa Serikali tu tuangalie njia za kuwasaidia hata madhehebu ya dini yasaidie hawa watu, vikundi mbalimbali isionekana kwamba Serikali tunaitwisha mzigo peke yake kwa sababu Serikali ni sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri ni vizuri ifikie wakati ambao tunawasemea, tunawasaidia kwa hali na mali tena ingetokea wakati sisi Wabunge katika Mkutano kama huu wa Kumi, tunapitisha mchango, tunapeleka kwa watoto yatima au tunajenga shule za kusaidia watoto yatima, ingekuwa busara sana kwa sababu huko hali ni mbaya sana, wanakosa ada, wanakosa *uniform*, wanakosa chakula, wanaishi maisha magumu sana. Kwa hiyo, nafikiria ni vizuri suala hili tulitilie mkazo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumze Jimboni kwangu maana nimezungumza kwa ujumla jumla. Kule Njombe Magharibi na hasa pale Ilembula kuna tatizo la hizi dawa za *ARVs,* kwa kweli zinaenda kidogo sana na hata kondomu ni chache. Nilikuwa ninazunguka madukani nikakuta kondumu zinauzwa kwa bei mbaya ya shilingi 200 sasa mwananchi wa kawaida hawezi kununua wakati hata mlo mmoja kule ni ngumu. Kwa hiyo, ninaomba wapeleke misaada mikubwa sana kule kwa mfano hizi *counting machine* za kupimia UKIMWI, ni tatizo kubwa sana mpaka waende Iringa Mjini, wananchi wangu wanateseka sana na wamenituma nitoe ombi hilo Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nizungumzie kuhusu suala la athari zinazotokana na ugonjwa huu. Athari zinatokana na ugonjwa huu, sehemu kubwa zinalenga nchi ambazo hazijaendelea yaani nchi maskini kama Tanzania. Sasa sielewi

uhusiano wa UKIMWI na nchi ambazo ni tajiri ambako pengine ndio sehemu hata kondomu zinatoka kule maambukizi ni kidogo sana. Nilienda Geneva, Japan, Ujerumani maambukizi ni kidogo siyo kama huku Tanzania au nchi ambazo hazijaendelea. Sasa nikijaribu kuangalia sijui hapa kuna nini! Tuseme labda wenzetu elimu imekuwa kubwa kuliko sisi? Kama kweli elimu ni kubwa kuliko sisi, wenzetu wale watatusaidiaje? Je, kweli wapo katika kutusaidia au wako katika ajenda zingine kibiashara? Hilo siingii ndani sana kwa sababu watu watasema thibitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli huu ugonjwa wa UKIMWI unapokuwa kwenye nchi za kimaskini, umaskini unazidi kuwa mkubwa na nchi za wenzetu kule zinazidi kutajirika kwa sababu kule ndio vifaa vingi vinatoka kule. Sasa tuangalie ikiwezekana na wenzetu kule wajaribu kupunguza hata lile suala la utaalam, waweze kutusaidia bure au ikiwezekana utaalam wao uwe wa bei nafuu sana hata dawa zinazokuja wajitahidi kupunguza bei waelewe kwamba wanasaidia kama watoto wao kwa sababu sisi tuna matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kutoa changamoto kwamba nchi zilizoendelea hasa nchi tajiri hizi ziangalie njia za kusaidia nchi ambazo ni maskini ikiwezekana misaada wanayotoa isiwe ya masharti makubwa na waelewe kwamba sisi ni binadamu kama wao, kwa hiyo, wajitahidi kupunguza gharama kwa kiasi kikubwa sana mfano za *CD4 machine* au madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nichukue nafasi ya kipekee, kushukuru haya madhehebu ya dini kwa sababu dawa kamili ya kuzuia au kudhibiti UKIMWI, ni kubadilisha tabia yaani tabia iwe nzuri siyo kubadilisha tabia iwe mbaya. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuzishukuru mfano Dini za Kikristo, Dini za Kiislam, Mashehe, Mapadre, Maaskofu, Wachungaji na waumini mbalimbali na kwamba tujitahidi kufuata imani zetu ili tuondokane na hili tatizo na tujitahidi kuwapenda sana hawa waathirika wachache, tuwape faraja na hii ndio itakuwa dawa nafuu na tutapunguza haya maambukizi ya UKIMWI na tutadhibiti na kuzuia kabisa suala la UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninawapongeza Wabunge wenzangu, wametoa michango mingi, mimi ni kama ninamaliziamalizia tu lakini kwa kweli ninawapongeza sana kwa michango yao na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pale kwa kweli ninawapongeza sana kwa jitihada zote wanazozifanya hapa nchini Tanzania na kwa jinsi wanavyojitolea kuhakikisha kwamba huu ugonjwa unatokomezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, sasa nitamwita Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kabla sijaanza kuchangia, uniruhusu nianze kwa kutoa salamu zangu za mwaka mpya kwa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuongea Bungeni toka tumeanza mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, niungane na Watanzania wenzetu na Wabunge wenzangu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *AU*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Kigoma Mjini, tulipokea kwa masikitiko makubwa kifo cha Mbunge mwenzetu Benedict Losurutia, tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kichwa cha habari cha Muswada huu ni *HIV and AIDS ( Prevention and Control)*, kwa kweli nadhani moja ya kazi kubwa tunayopaswa kuhangaika nayo ni ku-*control* kuliko kutibu. Hili la kwanza tu limenipa faraja kubwa sana kwamba sasa tumeanza kufikiri *to the best direction* namna ya kuhangaika na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine, nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Mkoa wa Kigoma maana Kigoma kwa kweli bado sisi tunashika namba ya mwisho katika maambukizi ya ugonjwa huu wa UKIMWI, niwaombe tuendelee kushika namba ya mwisho nadhani hili ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini UKIMWI siyo maafa, UKIMWI ni ugonjwa kama yalivyo magonjwa mengine na kwa kweli ukiangalia *statistics* zetu tokea tumeanza hali yetu siyo nzuri sana. Nianze na hili la pesa zinazokuja. Ukiangalia ripoti ya *Controller and Auditor General*, kuna pesa nyingi sana zinapotea katika kitengo hiki cha UKIMWI. Niwaombe wenzetu wa Serikali watusaidie sana, hizi ni pesa zinazokuja kwa ajili ya kusaidia watu wetu walioathirika na tusizipoteze hela hizi nyingi kwenye vikao, kwenye semina hazitusaidii, watu wetu wana shida sana na pesa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka siku moja tulikuwa tunafanyiwa semina na watu wa *USAID* wakasema wanasikitika kwamba pesa nyingi zimekuja lakini hazijatumika. Kwa hiyo, matarajio yangu ni kwamba watu wanaosimamia mambo haya, hizi pesa zitumike kama ilivyopangwa ili kwa kweli mapambano haya ya UKIMWI yaenda sambamba na sisi kuwa *responsible* ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mimi nishukuru kwa juhudi za dhati kabisa alizoanzisha Mheshimiwa Rais ili kuhakikisha watu wote tunapima. Nina mapendekezo ingawaje ninajua tutaambiwa kuna suala la haki za binadamu lakini nadhani ambacho tunatakiwa tuanze nacho ni kufanya sensa ya kweli ili kujua tatizo la UKIMWI kwa Tanzania ni kubwa kiasi gani. Ni kweli tumeanzisha zoezi la kupima kwa hiari na watu wengi wamejitokeza lakini ukiangalia namba ya Watanzania tunakaribia 40,000,000, waliojitokeza ni wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nadhani kwa maana ya Serikali kujua ugumu wa tatizo, hata kwa siri, kila mgonjwa anayeenda hospitali kupima malaria, kuna dhambi gani tukichukua damu yake tukapima UKIMWI? Hakuna haja ya kumwambia matokeo lakini nia yetu ni ili tuwe na sensa ya kweli kweli na kujua hili tatizo ni kubwa kiasi gani. Maana ukiangalia hii ya watu kujitolea, siyo watu wote wanaenda kupima watu wengine ni waoga. Kuna watu wengine ukishaanza kumwambia tuanze na kukupa ushauri nasaha, anaondoka au anakuja anapima lakini tuifanye *internally* tuhakikishe kila anayekuja tunampima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wamama wajawazito wanafanya vizuri na kwa watu wengine wote wafanye hivyo ili sasa tukishajua hili tatizo ni kubwa kiasi gani *then* ni rahisi hata kupanga mipango ujue tunahitaji fedha kiasi gani, tunaweza kufanya mipango gani kwa sababu tutakuwa tunajua sasa kama Serikali tatizo ni kubwa kiasi gani. Ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Afya, atusaidie suala hili ili tujue tatizo ni kubwa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni sisi wenyewe viongozi, hili suala la UKIMWI hatujaamua vizuri sana. Nilikuwa ninaangalia kwenye *internet* siyo mfano mzuri sana lakini ndio ukweli wenzetu walikofika. Hivi karibuni kule Brazil huwa kuna tamasha la *Carnival* linafanyika kila mwaka. Ni tamasha kubwa sana Duniani wanajaa watu wengi sana. Kwenye tamasha la mwaka huu wameongeza *supply* ya kondomu kwani wao wana hakika kwenye tamasha hilo mambo hayo yatakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka siku moja nilisoma kwenye magazeti kulikuwa kuna tamasha Dar es Salaam watu wamelala pale, watoto wanacheza muziki, asubuhi kwenye magazeti wanasema uwanja wa *Leaders* umekutwa umejaa kondomu. Hilo eti likawa ni tatizo. Nilidhani lilikuwa ni jambo jema kama watu wameamua kutokuwa wavumilivu lakini wametumia kondomu, *then* kama nchi tume-*achieve*, tumeweza kuzuia watu wasiambukizwe na ndio maana tumeambiwa kama hatuwezi kujizuia basi angalau utumie kondomu lakini sisi watu wakikuta kondomu zimetumika hilo jambo ni baya yaani ni kama siyo jambo la kusema kwenye jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani lazima jambo hili tuwe wakweli, tuwe wawazi kwa sababu hili tatizo ni kubwa, nguvu kazi inaisha na hasa kwa sisi vijana hali ni mbaya zaidi, watusaidie, tusilionee haya ili tuweze kulieleza jambo hili vizuri na kwa sababu hiyo tutaweza kushinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la UKIMWI. Ninaamini UKIMWI, ni mtambuka. Ukiliangalia suala la UKIMWI kwa mapana yake ukaanza kuangalia jinsi ambavyo linazagaa hapa Duniani, ukianzia nchi kubwa zilizoendelea unaanza kuona *element* ya umaskini nayo ipo. Kwa hiyo, nadhani tuhangaike na kukuza uchumi wa nchi yetu, tukifanikiwa, uchumi ukikua, nadhani hata mapambano haya ya UKIMWI yatapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine pale Dar es Salaam kuna mtu mwingine unamuuliza Bwana vipi? Anasema aaah, Bwana mimi mtu akija hata kama

mnasema ana UKIMWI sawa ni kheri niishi maisha mazuri sasa kuliko nikae muda mrefu ambao nitapata shida. Unaweza ukaona ni *mentality* gani ambayo imeingia, maana yake ni ya umaskini kwamba mtu akinunuliwa gari hata akiambiwa huyu Bwana ni *suspected* anasema aaah, maskini wa Mungu mimi ningepata gari lini? Ngoja nijaribu, baadaye wakati ukifika, nitakufa, nitaondoka. Hii ni *mentality* ya umaskini. Kwa hiyo, naamini ni lazima tupambane na umaskini kwa nguvu zetu zote, sisi wananchi tushiriki kwa kufanya kazi kwa bidii, tukifika hapo mapambano hayo ya UKIMWI yatapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda nchi kama Japan wanavyosema maambukizi ni madogo ni kwa sababu hata muda wenyewe ni mdogo kwani muda wote watu wako kazini maana mambo haya ukiwa huna kazi ndiyo unafikiria cha kufanya. Kwa hiyo mambo haya ni lazima tuyaangalie kwa upana wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limo kwenye Muswada nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Afya, ni suala la *Research Centers*. Ninaamini tunayo *Research Center* ya *NIMRI*, sidhani kama ni sahihi kuanzisha kitu kingine kinachofanana na *NIMRI*. Ninachokiona mimi ile *NIMRI* iongezewe uwezo, majukumu kwa sababu *already infrastructure* ipo, tusikimbilie kuanzisha *Institutions* hata hizo hela ambazo zingekwenda kuwasaidia watu kwa ajili ya madawa ya kurefusha maisha na lishe tunayapeleka kwenye kuanzisha *Institution* wakati tunayo *Institution* ambayo tukiiongezea nguvu na tukaiongezea vitendea kazi bado wataweza kufanya hii kazi na tutapunguza gharama ili pesa nyingi inayokuja ya wafadhili iende kwa wale wanaohusika. Kwa hiyo, ninaomba sana Waziri wa Afya, aangalie uwezekano wa *NIMRI* kuongezewe nguvu ya kiutendaji kwa sababu wao *already* wana *infrastructure*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niombe kwa suala la mila na desturi zetu, kule ambako maambukizi ni madogo, ukifuatilia sana bado watu wanashika dini vizuri, suala la mila pia nalo limetusaidia sana. Ni vizuri turudi kwenye *basics* zetu kama Watanzania, tutaweza kupambana na jambo hili. Tufike sehemu ile ambayo wakati wenzetu mlipokuwa mnakuwa kuna haya mambo hayakuwa rahisi hivyo lakini sasa yamekuwa rahisi mno, kwa hiyo turudi kwenye *basics* zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuombe dini zitusaidie, Mashehe Misikitini na Viongozi wa dini za Kikristo, haya mambo tuyaongee bila uoga, tuwaambie watu jambo hili ni dhambi. Tukifanya hivyo tutafanikiwa lakini baada ya hapo tuhangaike na suala la elimu katika umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono Muswada huu kwani umekuja kwa wakati *in fact* umechelewa. Kwa kweli pale kwenye adhabu ya watu wale wanaosambaza UKIMWI, naomba nimalizie kwa kusema naamini adhabu ni ndogo, hawa watu wanaua watu tena wengine kwa makusudi, wengine ukiwafuatilia ni kwa sababu wamepata pesa za rahisi hata hawakuzifanyia kazi wanatumia pesa hizi kuwaua Watanzania. Mimi nasema watu hawa tusiwaonee aibu na ni rahisi tu, watu wanaofanya hivyo wanajulika, tufike sehemu tuweke Sheria na tuweke kwenye taratibu zetu kwamba mtu akihisiwa tuwe na utaratibu apimwe, hawa watu tuwashughulikie, tukiwafikisha

hapo, wataogopa maana hatuwezi kuangalia mtu anaua watu inabaki ni hadithi mtaani tu wenyewe utawasikia, mtu anawanunulia magari mekundu maana yake kwamba uko njiani kuondoka, *why* tuwakubalie watu hawa? Kwa nini wanasema wasipimwe hawa ili wakikutwa Sheria ifanye kazi? Mimi nasema tuwe wakali kwenye jambo hili na ndiyo njia tutakayoweza kuokoa kizazi hiki bila hivyo hiki kizazi kitateketea sijui tutapata dawa lini mimi napata shida hasa kwa sisi vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita msemaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada huu.

Kabla ya kuanza kuchangia, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mara, napenda kutoa salamu zetu za rambirambi kwa wananchi wote wa Wilaya ya Kiteto kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wao Marehemu, Benedict K. Losurutia. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa uvumilivu na amuweke Marehemu mahali pema Peponi, Amen!

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuanza kuchangia Muswada huu kwanza kwa kuipa pongezi Wizara kwa kuleta Muswada huu ambao mimi binafsi nilipokuwa nikiupitia, nimeona umepitia maeneo mbalimbali katika kukabiliana na tatizo ambalo lipo mbele yetu. Sioni kama kuna sababu ya kuusahihisha Muswada huu bali tunatakiwa tu kutoa ushauri kwani Muswada ni mzuri na umegusa maeneo yote.

Vilevile napenda pia kuipongeza Wizara kwa kukubaliana na kuondoa neno hili ambalo lilikuwa linaonekana kwenye Muswada lililokuwa linasema kwamba “*whenever resources allows*” na badala yake wameweka neno “*using available resources*”. Hii imetuonyesha kwamba sasa Wizara iko tayari kukabiliana kwa asilimia mia moja na janga hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niipongeze Tume ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)* kwa shughuli nzito ambayo wamekuwa wakiifanya na hatimaye kupelekea maambukizi kwa kiwango fulani hatusemi kiwango kikubwa sana lakini kwa kiwango hichohicho kidogo kupungua. Kwa hiyo, nawapongeza sana *TACAIDS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu kutoa ushauri kwenye sehemu ya tatu ya Muswada inayosema *Public Education and Programmes on HIV/AIDS*. Kutokana na kwamba shughuli nzima ya kuratibu na kusimamia shughuli nzima za maambukizi ya UKIMWI zinasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, napendekeza kutokana na ufinyu wa bajeti ya Wizara ya Afya, *item* namba 7 – 9 ingeshughulikiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa na UKIMWI na zile *item* nyingine basi zingeweza kushughulikiwa chini ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri kwenye *item* namba 12, kumekuwa na *procedures* nyingi sana *surgical and dental procedures* ambazo zinafanyika kiholela kwenye hizi hospitali na *dispensaries*. Kwa hiyo, naiomba Wizara iweze kuweka mikakati madhubuti na mikakati muhimu kabisa ya kuweza kuzisimamia hizo hospitali ili wasiweze kufanya hizi *procedures* kiholela kwani tumeona kwamba baadhi ya maambukizi yametokana na hizo *procedures* ambazo zimekuwa zikifanyika kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *part* 4 ya Muswada ambayo inahusu *testing and counselling,* neno ambalo limetumika sana katika Muswada huu yaani *voluntary testing* tuongeze pia upimaji hata kama ni wa siri, tukizingatia haki za kibinadamu, kila mgonjwa anapokwenda hospitali chochote kile anachoumwa, basi achukuliwe damu na aweze kupimwa virusi vya UKIMWI. Tumeona kuwa hatupati takwimu ambazo ziko sahihi kutokana na kwamba tunasubiri tu wale wagonjwa wanaopima kwa kujitolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi za Kusini mwa Afrika kama Afrika Kusini, Namibia na hata Botswana wamekuwa na takwimu ambazo ziko juu sana na nchi kama ya kwetu Tanzania tunajiridhisha kwamba nchi zile ndiyo zenye maambukizi makubwa lakini je, kwenye nchi yetu, ni watu wangapi wamepima? Ni watu wachache sana. Kwa hiyo, tuchukue hizo damu kwa kila mgonjwa anayekwenda pale hospitalini, tukiunganisha na hizi *voluntary testing,* basi tunaweza tukapata takwimu ambazo kwa upande mmoja au mwingine zitatupa usahihi wa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *confidentiality,* tumekuwa na matatizo sana na hivi vituo vya afya vinavyohusika na masuala yote ya kupima na kutoa ushauri nasaha. Pale imedhihirika kwamba hakuna usiri jambo ambalo limeongeza hata namna ya kuwanyanyapaa wale wagonjwa na kuongeza hofu ya watu ambao hawajapima kwenda kupima kwenye vile vituo. Kwa hiyo, nina imani kabisa kuwa utaratibu uliowekwa chini ya kipengele hiki utaweza kuwashughulikia au kuvishughulikia vituo vyote vile ambavyo havina usiri kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo naona kama Muswada haujalizungumzia ni namna ambavyo wagonjwa wanaweza kupata haki yao ya usiri hasa pale wanapokuwa tayari wameshapata majibu yao kwamba wako *HIV infected* na wanatakiwa kupata dawa. Wanapokwenda pale hospitali wanakuwa dirisha tofauti na dirisha linalototolewa dawa za wagonjwa wengine wa kawaida na hata ukiangalia kadi zao zinakuwa na rangi tofauti. Kwa hiyo, pale wale wagonjwa wanakuwa hawana usiri, unapomuona mtu ana kadi ya *blue,* unajua huyu tayari ni *HIV positive*. Kwa hiyo, naomba Wizara iangalie namna ya kuweka usiri kwa wale wagonjwa aidha kwa kuchukua dawa katika dirisha la kawaida na kutumia hata kadi za kawaida ili kuweka usiri kwa wale wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya sita, napenda kuipongeza Serikali kwa suala zima la kuleta madawa ya kurefusha maisha lakini nina imani kabisa kwamba Serikali inatumia gharama kubwa kwa kuleta madawa haya. Sasa tumeona viwanda vya hapa nchini kwa mfano *Shellys Pharmaceutical* wameanza kutengeneza hizi dawa. Ninaiomba Wizara ijaribu kushirikiana na viwanda vya hapa nchini ili kuangalia mkakati

mzima wa utengenezaji wa dawa hizi hapa nchini ambao utalipunguzia Taifa letu kutumia pesa nyingi juu ya dawa hizi ambazo tunazileta kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu hii ya sita ya Muswada kwenye *item* namba 25, *prevention of transmission from mother to child,* suala hili bado halijatiliwa umuhimu au umakini. Tukienda kwenye hizi *Antenatal Clinics* bado suala hili la kupima akina mama wajawazito ni la hiari. Ninapenda kuishauri Wizara kwamba kwenye hizi *Antenatal Clinics* zote suala la kumpima mama mjamzito lisiwe suala la hiari, kila mama mjamzito atakapokwenda pale apimwe virusi vya UKIMWI ili atakapogundulika basi aanze kupatiwa zile tiba baada ya mama kuulizwa je, upo tayari? Kama hayupo tayari anasema mimi sipo tayari basi anaendelea na kulea mimba yake baada ya miezi 9 anajifungua mtoto na mtoto anakuwa *infected*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada, sehemu ya saba, kuna hawa *Health Practitioners,* wamezungumziwa humu ndani kwamba watapewa fidia. Ninaomba Wizara ituwekee wazi kwamba hii fidia wanayopewa watu hawa wanapokuwa wanahudumia wagonjwa ambao tayari ni *infected* aidha kwa kujichoma na vile vifaa, ni fidia ya aina gani na kama ni pesa basi ni pesa kiasi gani? Watuwekee wazi badala tu ya kuandika kwenye Muswada kwamba watapewa fidia, iweke wazi ni fidia ya aina gani na kama ni pesa basi ni pesa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la *establishment of Research Committee,* msemaji aliyepita amezungumzia kuhusu *NIMRI*, sote tunafahamu kwamba *researches* kuhusu UKIMWI zimekuwa *vexing tries* na *research* mbalimbali zimekuwa zikiendelea siku hadi siku. Lakini mimi najiuliza au naiuliza Wizara zile *research findings* ziko wapi mbona hatuzioni? Kwa hiyo, napenda kuweka msisitizo kwa Wizara kwamba tunaomba hizi *research findings* sasa zianze kutoka na ziwe wazi badala tu ya kuambiwa kwamba wanafanya *research* hatujui hizo *research* zitaisha lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwenye hii sehemu ya kumi na moja inayohusu *offence and penalties*. Hawa watu wanaoambukiza watu wengine kwa makusudi, ninaona kwamba hii adhabu iliyotolewa haitoshi kwa sababu kitendo cha kumuambukiza mtu UKIMWI kwa makusudi ni sawasawa na mtu anayeua. Kwa hiyo, hii adhabu haitoshi na ninapendekeza iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna suala lingine ambalo ni tatizo na ningependa Wizara itoe ufafanuzi, ni juu ya wale watu ambao tayari wameshajitangaza hadharani kwamba wao wameambukizwa virusi vya UKIMWI, watu hawa watalindwa vipi na hii Sheria? Maana inaweza kutokea mtu hampendi mtu fulani ambaye tayari ameshajitokeza hadharani kwamba ana vizuri vya UKIMWI *lets say* mimi nimejitokeza hadharani, nina mtu kwa makusudi hanipendi, anakwenda anasema kwamba nimemuambukiza virusi, je, hatuoni kwamba hii Sheria itawafanya hata watu waogope kujitoa hadharani kwamba wana virusi vya UKIMWI? Kwa hiyo, naomba Wizara inifafanulie hapo hawa watu ambao tayari wameshajitokeza hadharani watalindwa vipi na hii Sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hawa watu ambao wanaambukiza virusi vya UKIMWI, tendo lile ni makubaliano ya watu wawili, sasa mimi najiuliza, je, hatuoni kwamba tutakuwa hatumtendei haki yule mtu wa upande wa pili kwa sababu wote wawili wamekubaliana? Kwa hiyo, ninaomba pia Sheria hapa ijaribu kutueleza yule mtu wa pili, kwa nini mtu mmoja anachukuliwa hatua za kisheria kwa nini watu wote wawili wasichukuliwe hatua za kisheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninarudia tena kusema naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PAUL P. KIMITI:** *HIV and AIDS (Prevention and Control) Bill.*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuuleta Muswada huu ambao hali ya maambukizi bado ni kubwa. Nina ushauri ufuatao kwa Sheria hii.

1. Usambazaji wa kondom kutolewa kwa waathirika, kunaweza kuchochea waendelee badala ya kuwafanya wawe waangalifu. Hata hivyo, nashauri *condoms* zipunguzwe bei yake ili isifanye wenye kipato kidogo kushindwa kununua.

2. Nashauri sheria iwe wazi kuhusu fidia kwa watumishi wa afya ambao wataambukizwa virusi kutokana na kazi zao. Waganga na Wauguzi wengi wameathirika sana na hili. Tunawalinda vipi kwa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, katika mikoa ambayo haina *NGOs* za kushughulikia masuala yote haya, kwa nini sheria isiwatake wadau wasambaze huduma katika maeneo ya vijijini badala ya kung'ang'ania mijini na kwa misingi hiyo sheria itambue waganga wa jadi ambao wako huko ili wasaidie kuifanya kazi hii kwa misingi itakayokubalika.

Hivyo mwongozo na kisheria uandaliwe ili mazingira ya waganga hawa wa jadi ambao wamekubali kushirikiana na tafiti za kisayansi, waingizwe kisheria. Katika kusimamia kwa karibu wimbi hili la maambukizi, mpango kamambe nay a uwazi kuhusu matumizi ya fedha yaandaliwe kwa kila wilaya/mkoa na hata kwenye kata na vijiji – ili kila mtu ajue kitu gani kinafanyika kwa kila fedha inayoletwa kwa waathirika inatumikaje.

Majumu ya Wabunge katika kueneza elimu hii, ni kubwa sana. Ni katika mkakati huo, nashauri sheria au kanuni zitambue rasmi Umoja wa Wabunge wanaoshiriki masuala yote haya kama *TAPAC* na *TPAPD* ili navyo view vinapewa fedha za kuendesha elimu kwa umma, siyo kwenye majimbo yao tu, bali kwa kubadilishana maeneo ya kueneza ujumbe huu.

Tuwe na *Exchange programmes* miongoni mwa Wabunge wote. Hii italeta msisimko sana kwa kubadili sura za waelimishaji.

Mheshimiwa Spika, semina kwa Waheshimiwa Wabunge zihamie kwenye majimbo yao. Fedha zitolewe kwa kila jimbo ili Wabunge sasa wakaeneze ukumbe huu kwa wananchi wao kuanzia shule zote za msingi, sekondari, vijiji, kata na jimbo. Tuendelee kujifunza kutoka majirani zetu wa Uganda – na pia toka Mkoa wa Kagera, nini wamekifanya na kufanikisha kupunguza maambukizi haya ya ukimwi.

Naunga mkono hoja hii ya Muswada muhimu kwa maisha ya Watanzania wenzetu wote.

**MHE. DR. GUIDO SIGONDA:** Naipongeza Wizara kuleta Muswada wakati huu. Yapo mambo kadhaa yanayohitaji kuangaliwa kwa karibu na makini sana.

1. *Sec. 4 – (1) a-f* na (2) (3). Pia sec. 7, 8, 9 zinazohusu elimu kwa wananchi juu ya uzuiaji na udhibiti.

Swali: Ikiwa hivi sasa Wizara ina upungufu mkubwa wa watumishi kwenye zahanati zetuhasa kwenye jimbo la Songwe. Je, shughuli hii ya utoaji elimu kwa wananchi Wizara italishughulikiaje?

*Part IV Sec. 13, 14,* na 15 kwenye jimbo la Songwe kipo kituo kimoja tu – cha Mwambani – Jambo ambalo wananchi walioko nje ya kituo hicho kwa sababu ya umbali wanashindwa kupata huduma hiyo.

Swali: Je, Wizara haiwezi kuanzisha vituo vingine kwenye kituo cha afya cha Mbuyuni na kwenye zahati za Saza, Kapalala, Ngwala, na Guan a Galula?

Sec p. 21 je wale ambao tayari wameathirika lakini hawajajitangaza nab ado wanatambulika kuendelea na ufuska. Sheria inasemaje?

Sec. 23 matumizi ya *condoms.* Baadhi ya madhehebu ya dini hayako tayari kuhamasisha matumizi ya *condoms.* Je, sheria inasema nini juuya hali hiyo?

Tiba asilia: Je, kitengo cha utafiti wa tiba dhidi ya maambukizi ya virusi vya ukimwi kilichoko Muhimbili kwa kutumia dawa asilia (miti shamba) bado hakijapata ufumbuzi) wowote kupitia dawa hizo.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nipongeze Muswada huu kuja Bungeni na maoni yafuatayo (*Reservations).*

Muswada umechelewa sana ingawa kuna usemi usemao *better late than never*. Kwenye *interpretation local government authority* mwisho naomba iongezwe 1982 *as amended.*

5.6 (4) *Roles of Sectors* inaelezea kila *sector* ikitaka kufanya shughuli kupanga au programe ni lazima wapeleke *TACAIDS* kwa ajili ya kuratibiwa. (wazo hili ni zuri) lakini ni muhimu *TACAIDS* wakawa na Ofisi kila wilaya (wawe *De-centralized) = National*

maana *TACAIDS* ni *National* tutapoteza muda fedha na sisi kazi zetuni kwa kazi ili tuweze kuokoa maisha ya watu kwa kasi.

5.7 *Public education and programes on HIV and AIDS.* Muswada umetaja ni wajibu wa Wizara, Serikali za mtaa na wadau wengine hapa kuna wadau muhimu sana na ni *Press* na *Media.*

Mheshimiwa Spika, ukimwi ni janga wengi wametafsiri tofauti. Umeme, lukanda-kanda, wa muledio wa-muTV na kadhalika ngoma na kadhalika. Leo hii hakuna Mtanzania ambaye hajawahi kufiwa na ndugu, jamaa au rafiki kutokana na *HIV/AIDS* ombi kwa vyombo vya habari waelimishe taifa wananchi bure tupone. Sio sawa kutoza hela nyingi kama matangazo ya biashara.

Ni muhimu *TACAIDS/*Serikali/Wizara ianze kuongea na vyombo vya habari radio/TV magazeti watoe huduma hii bure kabisa kwa lengo la kuokoa maisha kama vile Duwasa HIV zinatolewa bure.

Pongezi kwa Muswada huu kukumbuka masuala ya *Gender responsiveness* kwa kweli wanawake nchini ni wengi sana na wana mzigo mkubwa sana kulea yatima, wagonjwa, vijijini kutafuta maji hivyo katika kupitisha Muswada huu naomba sana wanawake wapewe kipaumbele katika kupata elimu kwani nchi yetu bado ina mila na desturi ambazo zinamweka mama nyuma sana.

E.g. sheria zinasema *there shall be a chairman.* Baba ni kichwa hata tunapoongelea masuala ya *family planning* mwenye sauti ni baba. Hivyo wanawake waathirika zaidi hawana sauti katika familia. Wapewe nafasi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika,S.12 (3) mtu akizembea katika huduma yake kwa mfano wakati wa *operation*/matibabu ya meno na kadhalika akasababisha kumuambukiza mtu HIV kwa kutochemsha vifaa na kuwaandaa kikamilifu atakuwa ametenda kosa na atalipwa faini isiyopungua laki tano nashauri iwe au/*improsnment not less than six months or both.*

Mheshimiwa Spika,*5.15 (5)* Nashauri *every pregnant woman and every* person hiyo *every pregnant woman* itoke ibaki *every person.*

Mheshimiwa Spika, 15(6) kila mhudumu wa afya anapaswa ku-cheki HIV. Je kama na yeye ana ukimwi na anataka kuendelea kutoa huduma itakuwaje. Nashauri akiwa na ukimwi *any health practice* yeye asitoe huduma kabisa.

Mheshimiwa Spika,5.17 *Medical Confidentiality (*usiri) Je, kwa mfano mtu ametoa siri itakuwaje. Ni muhimu tukubaliane kwamba ni *offence* na *penalty* yake itakuwaje.

Mheshimiwa Spika,21.21 *Prevention of Transmision.* Lakini pia haijawekwa kama *Offence.* Nashauri iwe ni kosa tena la jinai maana ni *intention to kill* na ni kama *timing boom.* Ingawa *practicaly* ni ngumu ku-*prove.*

Mheshimiwa Spika,5.34 (1) Mstari wa 3. *The most vulnerable children* ongeza *and women.*(2) *Most vulnerable children and women*(3) baada ya sentensi *includes orphans and women.*

Mheshimiwa Spika, 5.36 (2) (a) (Ipo kwenye *amendment)* badili ya *Chairman* iwe *Chairperson* baada ya (i) iongezwe (j) awepo mtu mwenye ukimwi *One person living with HIV and aids – check schedule of amendment T: item (l)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia Muswada huu muhimu wenye nia ya kupambana na janga kuu la *UKIMWI* linalomaliza Watanzania.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake, na wataalam wote wa Wizara hii ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuandaa na kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kupambana na ugonjwa huu wameweka utaratibu wa kutoa dawa za kupunguza makali kwa waathirika. Dawa hii inatolewa kwenye Vituo na Hospitali zilizoko Wilayani na Mikoani.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi sana waathirika wako vijijini na kutokana na hali ya ugonjwa na kukosa kipato hata ile nauli ya kufuata dawa hizo Wilayani au Mikoani hawana. Naomba huduma hii ya dawa hizi ziwekwe kwenye Vituo vy Afya na Zahanati za Kata ili waathirika waweze kuzipata kiurahisi na hivyo kusaidia afya zao.

Mheshimiwa Spika, sambamba na utoaji wa dawa za kurefusha maisha Serikali ijitahidi sana kuhusu upatikanaji wa vyakula kwa waathirika hao wa UKIMWI. Hali ya wananchi huko vijijini ni mbaya sana sana ikizingatiwa waathirika hawa ni dhaifu hawana nguvu za kufanya kazi za kuwaletea kipato cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri alieleza Bunge hili Muswada huu /Sheria hii inawaweka wapi watoto wanaobakwa na hatimaye kuambukizwa VVU? Sheria hii inawabana vipi wale wanaume wanaofanya vitendo hivyo vya kinyama kwa watoto na kuwasababishia kuathirika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu *NGO's* Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayojihusisha na masuala ya UKIMWI, nyingi ya NGO's hizi zinapata fedha nyingi sana nje na ndani ya nchi, lakini haziwafikii walengwa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Mashirika hayo yapo kujinufaisha na mengi yapo *Centred* Mijini yanatoa huduma kwa watu ambao wana uwezo. Hawaendi vijijini kule wanapoishi waathirika wengi sana na hawana uwezo wowote.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa kwa Waziri wa Wizara hii kudhibiti kwa nguvu zote Mashirika haya yaweze kutoa huduma inayokusudiwa kwa walengwa na siyo kujisajili kwamba watasaidia suala la UKIMWI kumbe wanajinufaisha wenyewe.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni kwamba Serikali kuhakikisha kupeleka vipimo vya VVU maeneo yote muhimu na hasa kule wananchi wengi wanapoishi badala ya kuishia Mikoani na Wilayani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Wizara hii kwa kuleta Muswada huu pamoja na Sheria hii nzuri sana. Mimi maoni yangu ni masikitiko makubwa sana kwa Mashirika ya Misaada yanayokuja kutosaidia walengwa wenyewe. Baada ya kusaidia unakuta walaji wanatoka pembeni wanajiorodhesha kwamba ni wagonjwa wanawasaidia wakishapata misaada hiyo haiwafikii na huo mchezo ufe. Naomba Wizara itangaze kabisa watu baki wanaofaidika na miradi hiyo.

Kuna vituo vingine vina watoto yatima naomba Wizara hii kuvitembelea mara kwa mara ili kuona shida zilizopo kwenye vituo hivyo. Kuhusu upimaji Wizara hii naomba Mheshimiwa Waziri kuhamasisha sana hasa Mkoa wa Kagera. Wizara iongeze kasi maana ninashukuru Mungu Mkoa wangu hali siyo mbaya sana kama mara ya kwanza ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kituo kimoja, kuna vituo vipo Bukoba Serikali au Wizara itavisaidiaje? Vituo hivyo kwa watu waliojiorodhesha kulea watoto yatima kimoja kipo Kashai na cha pili Hamugembe. Mama Nuru na mama Sada hivyo vituo vina hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri anisaidie pamoja na kudhibiti misaada ya waathirika na wajane. Nitashukuru akinisaidia mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu mbele ya Bunge letu Tukufu.

*Part II* (5)(a)(b. Adhabu zinazopendekezwa chini ya kifungu hivi ni ndogo kulingana na uzito wa makosa. Nashauri vipandishwe. Aidha, napendekeza kuongezwe kifungu kingine kuhusu fidia itakayotolewa kwa mgonjwa atakayeathirika kutokana na makosa haya kama vile ilivyo kwenye *section* 26(c).

*Part III section* 12(3). Viwango vya adhabu inayopendekezwa ni ndogo haviwezi kuwaogopesha watenda makosa.

*Part IV Testing.* Napendekeza Serikali ihakikishie upatikanaji wa nyenzo za kupimia *HIV* (*Testing Kits*) kwa watu binafsi kama ilivyo kwa wanaopima mimba zinaweza kuuza katika maduka ya madawa *(Pharmacies).*

*Part VI section* 24(2). Upatikanaji wa ARVS urahisishwe kwa kuongeza vituo vinavyotoa huduma hii. Aidha, Serikali iruhusu "*Licensed Pharmacies*" kuuza dawa hizi kwa wale wenye ruhusa malaum ya Madaktari (*Prescriptions*). Vilevile Serikali ihimize utengenezaji wa dawa hizi ARVS hapa hapa nchini ili ziweze kupatikana kwa bei nafuu sana.

Matumizi ya fedha za wafadhili kwa ajili ya UKIMWI. Ipo haja kubwa sana ya kudhibiti kwa kiasi kikubwa matumizi ya fedha hizi nyingi ili ziweze kuwafikia walengwa. *NGO's* nyingi ni za mifukoni haziwafikishii walengwa fedha hizo. Nyingi zinaishia mfukoni mwao. Serikali isimamie kwa karibu sana matumizi ya fedha hizi.

*Section 47.* Sehemu hii iboreshwe kwa kusisitiza kwamba mtu yeyote mwenye virusi vya UKIMWI akifanya tendo la ngono bila kinga atakuwa amefanya kosa chini ya kifungu hiki.

*Sectio*n 49. Adhabu zilizopendekezwa chini ya kifungu hiki ni ndogo. Hazitoshi kuwaogopesha watendaji makosa. Napendekeza adhabu hizo ziongozwe.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuunga hoja mkono mkono.

Mheshimiwa Spika, Muswada huo ni muhimi sana kwa sababu UKIMWI ni kama vita ambapo watu wengi wanapoteza maisha kutakuwa na wagonjwa wengi ambapo nguvu kazi katika nchi yetu inapotea lakini wagonjwa hawa pamoja na watu wenye virusi ambao bado hawajaonyesha dalili za ugonjwa wotye hawakupata huduma ya tiba katika hospitali zetu ambapo wafanyakazi wa hospitali ambayo wanahusika kwa namna moja au nyingine kwa mfano:-

(i) Waganga: kwa mfano Tabibu Wasaidizi, tabibu waganga wasaidizi na Madaktari kwa ujumla.

(ii) Wauguzi.

(iii) Wafanyakazi wa maabara.

Mheshimiwa Spika, watu hawa kwa ajia yeyote ile wapo katika hatari kubwa mna sana au katika hatari kubwa mno; katika kuambukizwa vizuri wakiwa kazini *(occupational hazards).*

Hivyo basi nafikiri wakati umefika watumishi hawa wawekewe Bima ya Maisha hata kama malipo ya Bima hiyo hailingani na uhai wa mtu. Lakini angalau kifuta jasho; na itawapa nguvu ya kufanya kazi kwa moyo.

Lakini pia ushauri wangu wakati umefika kwamba kupima virusi kwa watu watakaooana (Wanandoa) iwe ni lazima na isiwe option kwa sababu tumeshaona watu wanapuuzia jambo hili na watu wanapoteza maisha baada muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuwapongeza sana walioleta Muswada huu muhimu kwa namna moja au nyingine nawaombea sana Mungu azidi kuwapa nguvu. Mwisho naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, (a) Kifungu cha 9 kwa kuwa Wizara ilikuwa imefikia hatua nzuri ya usambazaji wa *condom* kwenye maeneo hasa hatarishi e.g *Guest Houses* n.k. Ombi; kipengele hicho kiboreshwe kwa kuunganisha na wasioishi pia na virusi vya UKIMWI katika ugawaji wa *condoms*.

(b) Kifungu cha 16 (I): Naungana na usiri wa utoaji wa majibu ya aliyepima tu. Lakini Sheria itakuwa au itamuweka katika mazingira yapi mme au mke ambaye hakupimwa ili ndoa idumu na wanandoa hao walielewe tatizo na kukabiliana nalo?

Naomba kipengele kingine kiongezwe kikizingatia usiri kwa wanandoa wote bila kuiathiri ndoa yao.

(c) Usiri kwa Ujumla: Kwa kuwa sasa waathirika baadhi yao wameamua kuwa wazi, niombe sasa Serikali katika bajeti yake kuwatengea fedha ya kutosha katika kujenga vituo vyao karibu ili wapate huduma zilizosahihi na kuwa haraka hii wasichanganywe tena na wagonjwa wengine katika hospitali ya matibabu ya magonjwa mengine.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia katika muswada huu.

Kabla ya kutoa maoni yangu, naomba kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Losurutia kwa msiba walioupata pia nitoe pole kwako na kwa wabunge kwa kumpoteza Mbunge mwenzao tunamwomba mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mchungaji Rwakatare na tunamkaribisha Bungeni ili tueendeleze kazi iliyotuleta humu ndani.

Mheshimiwa Spika, nianze na fedha zinazopelekwa katika Halmashauri zetu za ukimwi kama walivyosema waliotangulia fedha hizi hazina mwenyewe.

Semina nyingi na makongamano zinaendeshwa huko na wanaopata hizo semina siyo waathirika wa UKIMWI wanapelekana wale wazima wagonjwa wenyewe wanaachwa wakiumia wakati fedha hizo zilizotolewa kwa ajili yao. Ninaomba sana fedha

hizo zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu wapewe maelekezo ya jinsi ya kutumia fedha hizi ilitusaidie wale watakaotumia fedha hizi vibaya.

Mheshimiwa Spika, Elimu kwa Umma pamoja na kuwa na semina nyingi zimetolewa na nyingi zimefanyika mijini tu kuliko vijiji ambako wagonjwa wengi wako huko na wametokea mijini bado elimu inahitajika vijijini kwa wale wote wanaowatunza wagonjwa wao majumbani ili nao waweze kujikinga na maambukizo.

Pia elimu itolewe kwenye matumizi ya *condom* kwa wale wote wanaofanya tendo la ndoa ili kupunguza maambukizo mapya. Jambo jingine ni kuelimisha wananchi juu ya mila ambazo zimepitwa na wakati kama kurithi wajane. Elimu itolewe ninaamini kabisa tunaweza kuzibiti ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja ambalo ninaona ni kumnyanyapaa mgonjwa wa UKIMWI hasa kwenye matibabu yao kwa kutumia kadi tofauti na za wagonjwa wengine hii inawatia hofu wagonjwa kwa kuona wamepata ugonjwa mbaya kuliko magonjwa mengine.

Suala hili ningeomba kama bado lisitishwe vinginevyo watu hawatajitokeza kwenda kupima na wengine hawatakwenda kupata matibabu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa maoni niliyokuwanayo.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Muswada huu ni mzuri kwani jamii ilikuwa inakosa mahali au hatua za kuchukua pale ambapo uambukizaji wa makusudi wa VVU unapofanyika na watu ambao wanajulikana na jamii kama wana virusi vya UKIMWI.

Aidha, Serikali ingezuia waganga wa Jadi kutangaza kama wao wanatibu UKIMWI, wakati inajulikana wazi kuwa ugonjwa huo hauna tiba. Kwa watu waelewa wenye elimu, hilo siyo tatizo lakini kwa wananchi wa vijijini ambao uelewa wao ni mdogo kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha, ni rahisi kurubuniwa na wganga hao na athari yake ni kuwadhoofisha wananchi kiuchumi.

Napendekeza pamoja na campains za kudhibiti UKIMWI kupitia elimu mashuleni semina na ugawaji wa kondomu zigawiwe bure kama moja ya mchango wa taasisi zinazoshughulikia udhibiti wa maradhi haya ya UKIMWI.

Hasa vijijini asasi zote zinazoshughulikia kampeni dhidi ya UKIMWI, wawaelimishe wananchi juu ya kinga kwa kutumia kondomu. Siyo lazima kondomu hizi zigawiwe kwa waathirika tu kama kifungu cha 9 sentensi ya mwisho inavyosema. Badala yake napendekeza wote waathirika na wasioathirika wapewe kondomu bure.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu kuhusu huduma kwa wagonjwa na au watu wanaoishi na VVU. Kumekuwa na tatizo la wagonjwa hawa kutopata huduma vyeo kwa usahili kama inavyotakiwa, kama vile chakula, madawa na mambo kama hayo. Naomba Wizara ijaribu kufuatilia kwa karibu kuhakikisha hawa watu wanapata huduma ya kutosha.

Lakini pia kuna tatizo la hawa wapimaji wa kipimo cha UKIMWI kutoa siri za wagonjwa. Ukweli haipendezi kabisa naomba Wizara ifanye marekebisho kidogo ili wafanakazi hawa wajitahidi kutunza siri za wagonjwa, nadhani itakuwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atoe ufafanuzi jinsi gani tutaweza kuhakikisha kuwa mtu amemuambukiza mwezie kwa makusudi. Kwa kuwa mama mjamzito anapokwenda kupima kliniki anapima na kipimo cha VVU. je, si vyema kama na mumewe angepimwa pia angalau kuleta uwiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu kifungu cha mgonjwa anayeambukiza kwa makusudi. Ningeomba angalau adhabu ya kifungo cha maisha ipunguzwe iwe hata miaka kumi angalau.

Naunga hoja mkono asilimia mia.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nfasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na wataalam wote wa Wizara ya afya na Ustawi wa Jamii kwa kuleta Muswada huu mbele ya bunge ili ujadiliwe na baadaye Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiukubali uwe sheria. Kwa maoni yangu Muswada umekuja kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi naomba nichangie katika maeneo yafuatayao:-

1. Kifungu cha 23(3) kumekuwa na malalamiko kutoka kwa watu wengi kwamba baadhi ya kondom kwa mfano salama kondomu siyo imara na kwamba zinapasuka kwa urahisi sana. Wakati huo huo zimeidhinshwa zitumike napenda kujua je kondomu za aina hiyo zimekidhi viwango vya Tanzania *Bureau of Standards* lakini pia ningeshauri shirika la viwango Tanzania liainishe aina fulani za kondomu badala ya kuwa na aina nyingi sana za kondomu na nyingi zikiwa hazina viwnago vinavyostahili.

2. Mheshimiwa Naibu Spika, viongzi wengi wa dini mbalimbali wamekuwa wakikataza matumizi ya kondom kwa waumini wao. Hata hivyo bado waumini wao hufariki dunia kutokana na UKIMWI mimi naona wakati sasa umefika kwa Serikali kuingilia kati juu ya mgongano huo. Yaani Serikali kutaka wananchi wasiokuwa waaminifu kwenye ndoa zao watumie kondom lakini wakati huo huo viongozi wa dini wanakataza matumizi ya kondom huku watu wakiendelea kufa.

3. Mheshimiwa Naibu Spika, (kifungu cha 27(3)) kuna waganga wengi wa kienyeji wamekuwa wakitangaza kwamba wanatibu UKIMWI; tena wanatangaza kwenye vyombo vya habari. Aidha, kwa baadhi ya viongozi na madhehebu ya dini wamekuwa wakitangaza kupitia vyombo vya habari kwamba wanaponya UKIMWI kwa njia ya maombi kwa kuwa sasa tuna Muswada huu ambao nina hakika utapita na kuwa sheria. Je, Serikali kupitia Wizara itakuwa tayari sasa kupiga marufuku matangazo ya namna hiyo kwani kutoa matumiani kwa waathirika kwamba wanaweza kupona UKIMWI kwa dawa za kienyeji au kwa maombi?

4. Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 35(1) kwenye jedwali la marekebisho kinazungumzia matumizi mabaya ya misaada *(misuse of aid).* Ni kweli kumwekua na matumizi mabaya ya misaada fedha zinazotlewa na Serikali pamoja na za wafadhili.

Kwa mtazamo wangu matumizi mabaya ya misaada fedha yanatokana na sababu nyingi lakini muhimu ni udhibiti mbovu kwa viongozi wanaohusika na misaada fedha hizo, pili na muhimu zaidi kumekuwa na vikundi vingi mno vinavyojihusiaha na mapambano dhidi ya UKIMWI.

Uwingi huu husababisha upotevu wa misaada ya fedha kwa sababu baadhi ya vikundi hivyo viko pale kwa maslahi binafsi.

Napenda ni shauri kwamba kwa kuwa sasa tunakaribia kuwa na sheria hii ya UKIMWI basi vikundi ambavyo tayari vipo viwe screened ili vile tu vitakavyoonekana vinafanya kazi nzuri basi hivyo vibaki na viendelee kusaidiwa.

5. Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana sijaona kifungu chochote kitakachowalinda watoto akina mama wajane ambao wazazi au waume zao watathibitika kufa UKIMWI; kwa misingi kwamb amali atakazoacha marehemu basi ziwe nai kwa familia ya marehemu na kwamba yeyote atakayesimamia mirathi ajue kwamba anafanya h ivyo kwa manufaa ya famili ya marehemu na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mapendekezo kama ifuatavyo:-

1. Futa kifungu kidogo cha 15(4)(a), kinapingana na kifungu cha 18(c).

2. Ondoa usiri juu ya watu wenye VVU ili kuondoa unyanyapaaji na uoga usio wa lazima. Itadhibiti uambukizaji mpya.

3. Walioathirika na VVU na UKIMWI wapewapo dawa wasiwe wanatengewa siku maalum, chumba maalum, muda maalum, vitambulisho maalum na kadhalika.

Maana yangu ni kwa kufanya hivyo ni kuwanyanyapaa na kuondoa usiri unaofichwa maana wanakuwa wamefahamika na watu wengi tu.

Hivyo basi wapewe dawa madirisha ya kawaida na siku yoyote kutegemea na mtu anavyopangiwa na madaktari.

Naunga mkono hoja hii.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima na kufika katika mwaka 2008 nikiwa salama na janga hili.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kwa kutuletea Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, gonjwa hili ni adhabu tuliyopewa na Mwenyezi Mungu baada ya ukaidi wa kuacha zinaa, na ili kuliepuka gonjwa hili ni kucha zinaa?

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na adhabu zilizopendekezwa kwa wale wote ambao watasambaza gonjwa hili kwa makusudi bila ya kuwaonea huruma.

Mheshimiwa Spika, mtu yeyote aliyebainika ameambukizwa au ana maradhi ya UKIMWI na bado anaendelea kufanya ngono huyo ajulikane anasambaza kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa janga hili asilimia kubwa linapatikana kwa kujamiiana ninaomba matangazo yote ya kondom yazuiliwe kwani yanafundisha ngono kwa watoto na hata kwa jamii nzima. Kwani yanahimiza na kushawishi ngono na kwenda kinyume cha maadili ya dini zetu.

Mheshimiwa Spika, pia ninaishauri Serikali kuvisaidia uwezo vikundi vya vijana ambao wamejitokeza kuelimisha umma madhara ya UKIMWI na kuwasaidia wale walioathirika.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa kusema kuwa kupima UKIMWI isiwe kwa hiari iwe ni kwa lazima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu.

**MHE. ROSEMARY KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Wizara kwa kukubali kufanya marekebisho ya Muswada kwenye zile sehemu zote ambapo neno "*Where resources allow*" na kutumia neno "*Using available resources*" hii imeonyesha wazi kabisa *commitment* nzima ya Wizara juu ya suala hili zima la AID and HIV *prevention and control*.

Katika *Part III (Public Education and programmes on* HIV and AIDS): Binafsi ningefurahi sana kama suala hili zima lingechukuliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu chini ya Kitengo cha Maafa na UKIMWI kwani mafungu yote ya UKIMWI toka *global fund,*

*TACAIDS* na kadhalika yapo chini ya Ofisi hii. Sote tunaelewa bajeti ya Wizara ya Afya haitoshelezi kabisa katika kushughulikia janga hili ambalo ni la kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika part IV (*Testing and Counseling*): Ningependekeza katika Muswada suala la *voluntary testing* liondolewe na badala yake *testing* iwe ni suala la lazima. Tumeona tunashindwa kupata takwimu sahihi kwa sababu ya hizi *voluntary test*.

Tunashindwa kujua ni kwa kiwango gani ugonjwa umeenea katika nchi yetu. Hivi karibuni tumepewa takwimu za waliopima na waliogunduliwa na virusi takwimu hizi si sahihi sababu ni idadi ndogo sana ya Watanzania waliopima katika *Part V* (*Medical confidentially*).

Vituo vingi vya kupima na kutoa ushauri nasaha vilionekana kwenda kinyume kabisa na maadili. Wengi wameshindwa kuweka usiri na hali hii imepelekea kuongezeka kwa unyanyapaaji wa wagonjwa wa UKIMWI jambo ambalo limepunguza kasi ya upimaji. Mikakati katika hospitali na *dispensaries.* Ni lazima kabisa kukafanyika uchunguzi wa hizi hospitali/*dispensaries* ili kuangalia namna *Surgical procedures* na *dental procedures* zinavyofanyika kiholela kila kuzingatia kanuni kwangu watu wengi wamepata maambukizi kutokana na kutokuwepo kwa ubora wa vifaa na ubora wa wafanyakazi waliopo kwenye sehemu hizi.

No confidentially on patient himself/herself Part XI offences relating to spread of HIV:

Suala hili limeongeza unyanyapaaji kwa watu waliokwishajitokeza hadharani kwani watu hawa wako kwenye hofu kubwa sana ya kusingiziwa na hivyo kukutana na adhabu hiyo. Suala jingine ni kutokutenda haki kwa upande mmoja wakati suala zima lilifanyika kutokana na makubaliano ya watu wawili na katika Muswada hatujaelezwa kuhusiana na huyo mfungwa awapo gerezani je mbali na adhabu hiyo ataendelea kupata matibabu na mlo*/special diet?*

Ahsante, naomba kuwasilisha.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, Naunga Mkono Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kuthibiti VVU/UKIMWI Nchini ya mwaka 2007.

Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara pamoja na timu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri kubwa ya kuleta Muswada huu na kushirikisha wadau.

Mimi kama mdau wa harakati ya kuzuia na kuthibiti VVU/UKIMWI, ni kweli usiopingika kuwa watu walioathirika na kujijua kuwa wana UKIMWI kwa makusudi kabisa wanaeneza VVU/UKIMWI.

Serikali ni lazima watu hao wathibitiwe kwa kuwekewa sheria kali. Sheria kali hii itakuwa ina maana hasa watu hao waweze kutambuliwa kwa wananchi kujitokeza kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola au sehemu husika ambako watahojiwa na kupelekwa Mahakamani.

Endapo ushahidi ukipatikana na kuonekana kuna kosa basi sheria ichukue mkondo wake. Hatua za kisheria kali ni pamoja na sheria zile kama za ubakaji na mauaji, kifungo, fidia na adhabu za viboko, au Mahakama itakavyoona inafaa.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, kulikuwa na utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wale ambao hutoa huduma majumbani (*Home based care)* ambayo yalitolewa na Mashirika mbalimbali kama vile *AMREF* na kadhalika.

Mashirika haya yalitoa vyeti mara baada ya mafunzo kumalizika, na hivi sasa utaratibu huo wa Serikali kwa maelekezo ya kwamba Serikali itatoa vyeti hivyo.

1. Nini tatizo, kama vyeti hivyo vingeendelea kutolewa na watoa mafunzo wenyewe? (yaani Mashirika husika).

2. Ni kwa nini sasa vyeti hivyo havitolewi kwa wakati baada ya kuyazuia Mashirika husika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakupongeza kusimamia Bunge na kuendesha vizuri kikao hiki cha kumi. Kwa makusudi sasa pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya Mheshimiwa David H. Mwakyusa pamoja na Naibu Waziri wa watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, UKIMWI, ni maradhi makubwa na Serikali ina wajibu wa kushughulikia na kuwajali wananchi wake, kutoa elimu, kinga na mambo mengine yote yanayosababisha kupata maradhi hayo.

Mheshimiwa Spika, dawa za maradhi hayo zitatolewa bure na zienezwe zikidhi haja. Pia zana zinazotumiwa kwa operesheni, chanjo, sindano vitumike kwa kufuata utaratibu na kwa wagonjwa wapatiwe lishe pamoja na misaada inayotolewa na nchi za nje au misaada mingine itumike kwa wahusika kusiwe na ubabarifu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu.

**MHE. BEATRICE M. SHELUKINDO:**Mheshimiwa Waziri, Asalaam Aleykum! Nichukue fursa hii kukupongeza wewe na Naibu Waziri wako kwa kuleta Muswada huu hapa Bungeni.

1. Kimsingi ni sahi, ila wasiwasi wangu ni kwenye utekelezaji wake. Pamoja na juhudi nyingi zinazofanyika kupambana na gonjwa hili, kuna baadhi ya maeneo ambapo kazi inayofanyika ni kidogo sana ikiwemo Wilaya ya Kilindi. Pamoja na Kamati

kuundwa, fedha ambazo tumeahidiwa na *TACAIDS* hadi sasa ni kidogo mno. Hivyo kazi ya uhamasishaji imekuwa ngumu sana. Pamoja na ugumu huo, kwa jitihada ya Sekta ya Afya kupitia huduma ya Benjamin Mkapa, Kilindi iliongoza katika Mkoa wa Tanga kwa zoezi la upimaji kuunga mkono agizo la Rais.

**Pendekezo:** Pengine tungeweka kipengele ambacho kinahusu maeneo ambayo bado uhamasishaji ni mdogo na *resources* za kufanya hivyo ni ndogo au hakuna na mila na desturi bado ni imara, waweza kuangaliwa kwa umakini zaidi ili muswada huu wa maana kwa watanzania wote na kwa ujumla utekelezeke.

**2. Kipengele 9:-**Hapa panahitajika pawepo na msisitizo na pengine hatua itakayochukuliwa kwa muajiri ambaye hatafanya hivyo. Yaani *work place programmes,* kwani maeneo mengi hawafanyi hivyo. Labda kufanyike tathmini Fulani kila mwaka au vinginevyo

**3. Kipengele 12 (c):**Je! Waziri ana taarifa ya mradi uliopo chini ya Wizara wa "*John Snow,*" uliobuni sindano ambazo hutumika mara moja na ambazo hadi sasa zimesambazwa maeneo mengi kwenye Hospitali zote za Mikoa na baadhi ya Vituo vya Afya na ambazo zina *containers* maalum za kutupia na kuchomwa?

Je! Hakuna haja ya kusema zile sindano nyingine zote zifutwe?

*Stock* iliyopo ikimalizika basi! Kwani *stock* ni kubwa mno *MSD* na zinatakiwa zisambazwe kote bure.

**Kipengele 35:-***NGO's, CBO's, FBO,CSO's* zote zinasajiliwa kwingine na kupata *funds.* Je! Ni kipengele kipi kitakachowafanya wanaodaiwa kupewa huduma kujua hilo? Kama *CSO* inachukua kibali (leseni) ya kuhudumia Mkoa wa Tanga, je! Kule Kilindi watajuaje kama na wao wanastahili kupewa huduma?

Kwani kuna *brief case NGO's* ambazo zinapewa fedha kwa maeneo ambayo hayana taarifa, hivyo kuishia hewani au kwa kushirikisha mtu mmoja mmoja kwa maslahi yao. Kuna haja ya kifungu cha kuwalazimisha wataje na wawajulishe wahusika na kuwe na *facal point* kwa maeneo yote ya huduma. *God bless you as you answer.* Ahsante.

*N,B:-*Kuna haja ya kuwa makini zaidi katika muswada huu, kwani endapo pana tatizo kubwa katika huduma ya Afya, *eg,* upasuaji tata Muhimbili (kupewa dawa za kuzuiya mamba mvulana Chuo Kikuu *by mistake. (Not sure but quoted in one paper)*).

Je! Hakuna haja ya kuweka hatua kali katika sheria hii ili kuhakikisha kuwa wanakuwa *careful* kwenye maambukizo ya *UKIMWI* na hatua za wazi kuchukuliwa kwa atakayebainika.

**SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, Ninakushukuru kwa dhati kabisa kwa fursa uliyonipa kuchangia kwa maandishi. Awali ya yote ninachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Afya kwa kutuletea Mswada huu tuweze kuujadili.

Kwa heshima ninaomba Waziri arejee sehemu ya IV, kifungu 15(5) na 16. Anapopimwa mwanamke mwenye mamba kwa hiyari na ikatokea kuwa ana virusi vya *UKIMWI*, akijifungua haruhusiwi kunyonyesha.

Swali langu ni kwamba, inapotokea hivyo, ulimwengu mzima si unapata taarifa kuwa mama huyo ameathirika? Mimi ninaamini kuwa hapo hakuna siri tena. Je! Hali hii itasaidiwa vipi? Hii siyo kuwanyanyapaa?

(3)Je! Serikali na *NGO's* ina *programme gain* kuhusu lishe ya watoto hao ambao wanazuiwa kunyonya siku za awali?

Mheshimiwa Spika, ninaomba kupatiwa majibu na ufafanuzi. Ahsante.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kutoa pole kwa wapiga kura wa Jimbo la Kiteto kwa kumpoteza Mbunge wao, marehemu Benedict Losurutia. Aidha natoa pole kwa Wabunge wote kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu huyo. Napenda pia kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu.

Kwa ufupi nina mchango ufuatao:-

Mosi. Ni vyema sasa baada ya kuwa na wagonjwa wengi, Wizara ya Afya iimarishe Idara ya Kinga ya Wizara ya Afya katika kushughulikia suala la *UKIMWI*. Hali ya sasa ya kuwa na *NGO's* nk, ambazo zipo kwa ajili ya kupata fedha tu na sio kusaidia wenye ugonjwa wa *UKIMWI* itaisha tu endapo Idara ya Kinga na Vitengo vyake vitaimarishwa na kuboreshwa.

Pili. Wizara ya Afya ianzishe mara moja kuingiza kwenye *syllabus* ya Wizara ya Elimu na Mafunzo, masomo ya afya na *UKIMWI*. Mimi naamini vijana wetu wadogo na wanafunzi watachukua tahadhari za *UKIMWI* endapo watajua tangu mapema dalili, kinga/tahadhari na mambo yanayohusiana nayo.

Kumbuka vijana ndio wenye nguvu na ndio tegemeo la Taifa, si vyema wasiwe na ufahamu mpana wa afya zao juu ya *UKIMWI*. Vinginevyo tutazidi kupoteza kwa kasi nguvu kazi ya Taifa.

Tatu. Kwa kuwa, uzoefu umedhihiri kuwa kuwepo kwa tafrija na sherehe za usiku kwenye maeneo ya vijijini kumekuwa chanzo cha ngono hatarishi, mfano ngoma, na kadhalika. Maana ngono hufanywa bila kinga yoyote kama *condoms*.

Ni vyema utaratibu uwekwe katika Taifa zima, mkesha (ngoma za usiku) upigwe marufuku. Ngoma za usiku ziishie saa 4.00 usiku na sio zaidi. Maana baada ya saa 4.00

usiku, minajili ya ngoma huisha na kuchoshwa, na hivyo kuhamia kwenye kufanya ngono.

Nne. *UKIMWI* sasa ni ugonjwa ulio dhahiri, hakuna haja ya usiri usiri wa kupita kiasi. Baadhi ya mambo yawe wazi zaidi ili kuepusha hofu kwa wananchi na kusaidia uhamasishaji wa wananchi ili watoe taarifa kwa uwazi na urahisi. Hii itapunguza maambukizi.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika kabla sijaendelea naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Pia nampongeza Waziri wa Afya kwa Mswada huu wa kuzuia Virusi vya UKIMWI. Huu ni Muswada ambao ni mzuri sana lakini naiomba Wizara ijitahidi kutoa elimu kwa wananchi kuhusu unyanyapaa wa ugonjwa huu. Kwa sababu unyanyapa unadhalilisha sana wagonjwa wa UKIMWI. Kuhusu wanaoambukiza kwa makusudi kama kweli watapatikana watu kama hao ni vizuri wachukuliwe hatua. Lakini je, watajulikana vipi watu hao na kuthibitika kuwa anaambukiza kwa makusudi. Na je, kama mgonjwa huyu wakati wa tendo la ndo anavaa kondom mgonjwa atawekwa fungu gani wakati Serikali inahimiza watu watumie kondom.

Naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutoa rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Losurutia kwa kuondokewa na mpendwa wao. Napenda kutoa mchango wangu katika muswada huu kwa kusema naomba wakati waathirika wanapochukuliwa vipimo au wanapokuja kuchukua majibu yao basi kwakuwa wanachukua masaa mengi kabla hawajapata vipimo au majibu, masaa mengi kabla hawajapata vipimo au majibu basi angalau katika fedha za UKIMWI watu hao waweze kupatiwa hata kitu cha kutafuna ama chai ama maziwa. Hili tulilishughudia na Naibu Waziri wakati tulipofanya ziara katika Hospitali ya Seokou Ture iliyoko Jijini Mwanza.

Pili katika shoo zinazofanyika katika kumbi mbalimbali wasanii wa kike kucheza wakiwa nusu uchi. Hapa Serikali inasema nini kwani kunengua ukiwa umevaa halafu pia panakilevi hamwoni hii inaleta vishawishi. Je, hali hii mnaonaje mimi nahisi pia ni hatari inasababisha ongezeko la maambukizi. Naomba mliangalie hili kwa undani. Pia wakubwa tunapokuwa na virusi na tukifa linakuja neno eti hili ni shinikizo la damu kwanini matangazo yasitoke na watu tukajifunza kuwa ukimwi hauchagui.

Pia, kwanini pesa za ukimwi hazifiki kwa walengwa ili zinazobakia kwenye makongamano. Naomba Serikali ihakikishe fedha hizi ziwafikie walengwa na waweze kupatiwa dawa na chakula pia pale wanapopimwa na kuona wameathirika?

**MHE. MSOLWA COSMAS MSOLWA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Afya kuuleta Muswada huo muhimu sana kwa taifa letu hasa tukizingatia hali ya ugonjwa huu umekuwa tishio kwa binadamu kwa miaka mingi sasa na baya zaidi hadi sasa hakuna dawa ya kuutibu. Hivyo kuwa na Sheria zinazohusu na ugonjwa wa VVU.

UKIMWI kwa nchi yetu ni muhimu sana kwa viele Watanzania walio wengi watazielewa ipasavyo ili hatimaye kuutokomeza ugonjwa huu hatari. Sheria hizi ni vizuri ikatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na kusambaza nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, naunga na waheshimiwa Wabunge ambao wanashauri kuwa kila kiongozi ni lazima apime VVU, lakini isiishie hapo tu zoezi la kupima VVU usiishie kwa viongozi peke yake bali upimaji huo uwe ni wa lazima kwa watu wote. Hata hivyo kwa viongozi wasiopima adhabu kali zichukuliwe dhidi yao ikiwemo ya kuwalazimisha na kuwasimamia kupima VVU/UKIMWI.

Kifungu cha 13 cha Muswada kinaainisha vituo/maeneo yatakayokubalika kupima VVU ambayo yamepata vibali vya *NACP*. Ushauri wangu ni kuwa Tanzania ni nchi ina eneo kubwa na vijiji vingi hivyo ni vyema Wizara ya Afya ikifanya maandalizi mazuri ya kuhakikisha kuwa kila kijiji nchini kinakuwa na kituo cha kupima VVU kinachotambuliwa na *NACP* badala ya vituo hivyo kuenea mijini tu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na kifungu cha 47 cha Muswada wa Sheria hii wa adhabu iliyobuniwa na Muswada huu wa kifungu cha maisha kwa wanaoeneza *HIV* kwa makusudi na ninashauri wafungwa hao watengewe magereza yao na wasichanganywe na wafungwa wengine wasiokuwa na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wafadhili wengi siku hizi wanapendelea kupeleka misaada yao ya miradi ya jamii ukiwemo ule wa UKIMWI kupitia kwa taasisi zisizo za Kiserikali *(NGO's, CBO's* n.k), ni vyema Wizara ya Afya kwa taasisi zote zinazojihusisha na miradi ya UKIMWI iziorodheshe upya upya wote nchini na izitake kuwasilisha taarifa zao zote zikiwemo matumizi ya fedha wanazopata kupitia kwa wafadhili mbalimbali na pia ifanye usimamizi wa karibu zaidi ili kuhakikisha kuwa fedha wanazozipata zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Hatua kali zichukuliwe kwa taasisi zisizo na zilizo za kiserikali zinazotumia vibaya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu mbele ya Bunge hili Tukufu ili ujadiliwe na hatimaye tupate sheria.

Nasikitika tu kwamba tangu mwaka 1983 ulipojitokeza ugonjwa huu kwa mgonjwa aliyegundulika katika hospitali ya Ndolage, iliyoko Jimboni Muleba Kaskazini, na leo 2008 ndipo unaletwa Muswada, Watanzania wengi wameumia na kuumizwa ama kwa kutokujua na kwa makusudi ya walioathirika kuambikiza wenzao kwa nguvu.

Napendekeza kwamba japokuwa maambukizi kitaifa yameshuka hadi 5% bado wako watu wengi wenye vizuri vya UKIMWI na hata wagonjwa walioko vitandani kwa kuugua UKIMWI, wakiwa hawana matumaini wapewe matumaini.

Jimbo langu la Muleba Kaskazini, ni moja lenye maeneo ambayo hayafikiki, mfano visiwa vya Kelebe, Bumbire na vijiji kama Ngenge na rushwa ni mbali na hata kusikika redio wanapata shida.

Sasa tuanze kampeni ya nyumba kwa nyumba, kijiji kwa kijiji, Kata kwa Kata hadi tuhakikishe watu wote wamepata lakini wamejua haki zao na wajue wanavyoweza kujikinga, na kutunza na kujitunza kwa wale wagonjwa.

Napendekeza pia, ufungaji wa ndoa iwe ni lazima kwa wanandoa watarajiwa wanaofunga ndoa rasmi makanisani misikitini Serikalini na hata kimila wapimwe kabla ya ndoa ili waanze ndoa bila kuwa na hofu wala mashaka. Vilevile waathirika wanaotaka kufunga ndoa wapate ushauri wa mara kwa mara ili wapate njia muafaka za kuishi kwa matumaini.

Napendekeza pia, pesa za UKIMWI zifike kwangu hasa visiwa vya Bumbire na Kerebe ambako hakuna aliyewahi kwenda huko kutoa elimu ya UKIMWI.

Aidha, iwapo programu ya kuelimisha mashuleni ongezeko kubwa la wanafunzi wanaopata mimba mashuleni ni uthibitisho tosha kwamba watoto wanashiriki ngono katika umri mdogo bila tahadhari ya kutumia kondomu. Waelimishwe sasa ili wasiambukizwe UKIMWI pia wasipate hizo mamba.

Mwisho narudia kwamba na kushauri kwamba elimu imetolewa ya kutosha mjini na maofisini sasa nguvu hiyo hiyo ihamie vijijini kwa ratiba mahsusi na takwimu za kitaalam

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Waziri nakupongeza wewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara yako za mashirika yote ya ndani na nje ambayo yamesaidia Muswada huu ufike Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Iramba Mashariki na wananchi wengi wa Tanzania hii wanaomba sasa Serikali iingilie kati na Wizara yako ndiyo isimamie ugonja huu.

Kwanza naomba elimu ya UKIMWI iwekwe kwenye mitaala kuanzia shule za msingi. Shule za Sekondari na vyuo Vikuu. Hii itasaidia sana vijana wetu kumfahamu na kuanza kujikinga wakingali wadogo.

Mheshimiwa Waziri fedha, zinazotolewa na Serikali na Mashirika yote ya nje zianze kupitia Hazina kwenye *busket fund* na itengenezwe miongozo inayoeleweka na muongozo huo utumike kwa nchi nzima na uletwe Bungeni ili Kamati ya Bunge inayokagua mahesabu ya Halmashauri za wilaya ifuate na kuhakikisha fedha hizo zinatumika vizuri na malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, wawakilishi wa kanda wengi hawawafikii walengwa kwa sababu wako kwenye kanda na muda mrefu kushughulikia hasa maeneo ya mkoa walipo. Iramba fedha zilikuwa zinatolewa na *TACAIDS* kuwasomesha watoto yatima lakini toka mwaka juzi fedha hizo zilianza kupitia kanda ya kati lakini nasikitika kusema wanafunzi wanaosoma sekondari za Lugugumo, Gumanga, Chemchem, Mzumbe, Msohi Technical Secondary School, mpaka leo hawajalipiwa ada.

Mheshimiwa Spika, wengine wamemaliza mafunzo na kunyimwa vyeti kwa sababu kuna kipindi ambacho hawakulipiwa ada naomba kwa makusudi wahusika yaani wawakilishi wa *TACAIDS* wa mikoa wapite kwenye shule zilizotajwa hapo juu walipe hizo ada. Pia watoe maelekezo kwa Halmashauri ya wilaya ihakiishe wanafunzi wote walipiwe ada.

Pia kule vijijini kuna waathirika wengi wanataabika hawapati dawa hata lishe kwa sababu hizi dawa zinahitaji mtu ale chakula bora. Pia ada *uniforms* na vifaa vingine vitolewe kwa wanafunzi yatima.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuchangia kwa kusema ningependa kuelezea masikitiko yangu kwa jinsi unavyoendelea kuwaathiri wagonjwa hasa kwa wahudumu wa afya unyanyapaa umekuwa ni tiketi ya kuwaongezea wagonjwa hao madhara na kufupisha maisha yao.

Kifungo hakitasaidia kwani lengo ni kudhibiti. Je, akifungwa UKIMWI utapungua na huyu mlalamikaji atakuwa wapi kwa kipindi chote cha *incubation?* Je, Serikali imeandaa majumba ya kuwahifadhi hawa ili kupata ushahidi sahihi?

Kuhusu akinamama wanaoambukiza watotowao kwa makusudi hao nao Muswada unasemaje? Kuna akinamama wanapimwa wakiwa wajawazito na kugundulika wana VVU na wakaambiwa lakini bado wanabeba m imba nyingine na hawaendi kliniki mpaka wajifungue kwa hofu ya kugundulika. Hawa nao Muswada huu unasemaje?

Lakini Muswada huu hausemi chochote kuhusu aliyeambukizwa yeye anashughulikiwaje na Muswada huu?

Ninaomba adhabu hii ya kifungo ifutwe kwani itafanya waathirike wajamiiane zaidi na *underground.* Hivyo kuongeza tatizo zaidi. Kwanini tusichukue mfano wa Uganda ambao *prevalence rate* imetoka 30% 1980s hadi kufikia 5% sasa je walifunga waathirika wanaoambukiza kwa makusudi?

Lakini hata Tanzania *prevalence rate* imeshuka toka 7% - 5% bila kufunga ninaamini *campaigns* za *HIV awareness* ni muhimu zaidi na uhakika fedha za UKIMWI zikitumiwa vizuri watu wataelimika na kamwe hawataambukiza kwa makusudi.

Nashauri kuwe na sheria ya kupima kwa lazima kwa watu wote na matokeo yawekwe kwenye *data bank* ili panapokuwa na *case* ya aina hiyo basi matokeo yapo tayari.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakupongeza kwa kuleta muswada huu muhimu kwa Taifa letu, pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Kwa kuwa, zipo ASASI zilizokuwa za kiserikali ambazo hupewa fedha nyingi na wafadhili/ wahisani wa kushughulikia tatizo la UKIMWI:-

(a)Je, Serikali inasimamia ama kudhibiti vipi ASAS hizo ili fedha za UKIMWI ziweze kuhudumia walengwa, waathirika wa UKIMWI, je, ASASI ambazo hupewa fedha na wafadhili kwa ajili ya tatizo hili na hutumia fedha hizo kwa kazi zingine. Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti hali hiyo na hata kuzifungia ASASI hizo ambazo hutumia fedha za UKIMWI vibaya. Je kuna ASASI yeyote ambayo serikali imeshaichulia hatua kwa matumizi mabaya ya fedha za UKIMWI?

(b)Je Serikali itakubaliana nami kwamba fedha zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya kupambana na UKIMWI zisaidie zaidi waathirika kununua madawa, Lishe elimu zaidi hadi vijijini na mashuleni?

Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruksa yako awali ya yote naungana na Wabunge wenzangu kutoa rambarambi kwa ajili ya kifo cha Mbunge mwenzetu Benedict Losurutia, Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi amina. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Getrude Rwakatare kwa kujiunga na Bunge letu kama Mbunge wa Viti Maalum.

Mimi naafiki kabisa, na naunga mkono mswada huu na nasema kwamba umekuja kwa wakati muafaka kwa kuwa sasa elimu ya kudhibiti UKIMWI umesambaa sana nchini na wananchi wamekuwa na upeo mzuri wa uelewa wa masuala haya. Kwa hivyo tunapoweka Sheria ni rahisi wananchi kuelewa tunazungumzia nini? Hili ni janga la kitaifa.

Katika Sheria hii naomba kuweka msisitizo wa masuala yafuatayo:-

(1) Sheria hii ihakikishe inazingatia msuala ya kijinsia bila kubagua wanawake. Mara nyingi mume na mke wanapoathirika kwa pamoja lawama ya kumwambukiza mwenzake, anatupiwa mnyonge ambaye ni mwanamke na hata inapotokea mwanamke ametangulia mama ananyimwa haki zake zote kwa kuonekana muuaji. Sheria hii imlinde na mwanamke.

(2) Sheria hii au Muswada huu pia uhusishe na magonjwa mengine ya kuambukiza kama *TB* na magonjwa mengineyo ya kuambukiza maana yote yanapelekea

binadamu kufariki. Hii ni tahadhari kuwa unapomshitaki mtuhumiwa kwa suala la ugonjwa wa UKIMWI, unashindwa kumshtaki aliyeambukiza kwa makusudi ugonjwa mwengine unaoua.

(3) Taasisi au *NGO's* zinazoshughulikia masuala ya UKIMWI, wawekewe masharti madhubuti ya kudhibiti na vyombo vingine vya kiserikali ili wenye *NGO's* hizi wasijichukulie maamuzi yao binafsi ya kutumia fedha jinsi wanavyotaka.

(4) Kule ambako sana hivi takwimu za maambukizi yako chini, Serikali ielekeze nguvu huko kwa kuwa kuzuia ni bora kuliko kuponya. Hii itapunguza sana gharama ya kupeleka dawa na huduma kwa watu wanapokuwa wameathirika kuliko gharama ndogo itakayotolewa kwa watu wanapokuwa hawajaathirika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii.

**MHE. DR. HARRISON MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa kudhibiti VVU/UKIMWI umekuja kwa wakati muafaka ambapo Watanzania karibu wote wanaelewa hatari inayotukabili na kampeni ya kupambana na hatari hii inahitaji ushiriki wa kila mwananchi. Sheria hii itatusaidia sana kiutawala hali inayotukabili. Nina maoni machache tu ya kuboresha muswada huu:-

(i) Ibara ya 3 ya Muswada ambayo inahusu tafsiri, inahitaji masahihisho katika tafsiri ya (*Court*) badala ya maneno (*with exception to primary court)* yawepo maneno *(with exception of the primary courts)* ambayo ni fasaha zaidi kwa lugha ya kiingereza.

Aidha tafsiri ya *sexual partner* ni pana mno inakanganya hivyo inahitaji kuboreshwa. Ikiachiwa kama ilivyo inawajumuisha hata wabakaji, waathirika wa kitendo hicho cha jinai, walawiti na hata walawitiwa na kadhalika. Tafsiri ya *Sexual partner* iwe (*restrictive*) isijumuishe wanaojihusisha na vitendo haramu vya kujamiiana.

(ii) Ibara ya 4 ya Muswada inaongelea wajibu wa kila mtu, taasisi na mashirika, wajibu wa kulinda haki za yatima kwa kuwapatia huduma ya afya na za kijamii. Kuzuia upimaji wa lazima wa VVU/UKIMWI nje ya sheria na kupambanadhidi ya unyanyapaa na ubaguzi ni wajibu wa msingi wa Serikali yenyewe na si taasisi au *NGOS'* Ibara ya 9 na ya 14 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaweka wajibu huo kwa mamlaka ya nchi na vyombo vyake vyote. Ibara ya 4 (c) ya Muswada iondolewe sehemu hii ya muswada.

(iii) Ibara ya 9 ya muswada inaongelea pamoja na mambo mengine utoaji wa *condoms* sehemu za kazi. Napenda kusisitiza hiki kipewe tafsiri pana linajumuisha hata rumande na jela zilizopo nchini, tukianza ingawa *condoms* rumande na jela tutakuwa tumehalalisha vitendo haramu vya kulawitiana kinyume kabisa cha sheria zetu za jinai. Hivyo Ibara ya 9 irekebishwe kuondoa utata huo.

(iv) Ibara ya 25 (2) irekebishwe ili *counselling servives* zisiwe kwa *pregnant and breast feeding women* peke yao, wahusishe vilevile *their spouses*

(v) Ibara ya 27 (1) inaongelea sharti la *Scientific Verification* kabla ya kutangaza tiba ya UKIMWI. Upo umuhimu wa kuweka kipindi maalum cha *scientific verification* ili tusiwakatishe tamaa watafiti wetu kwa kukalia uvumbuzi wao miaka na miaka kwa kwa kisingizio cha *verification* .

(vi) Ibara ya 28 maneno (*enact any law)* yaondolewe hayana maana, hakuna mtu mwenye madaraka hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rambirambi kwa familia ya Marehemu Losurutia, naomba Mungu ailaze roho yake mahali pema.Kwanza napenda kuwauliza kuwa, kuna kipengele gani kwa wakeketaji na ni adhabu gani wanapewa kwani ukeketaji pia unaambukiza UKIMWI na kama kuna adhabu ili ukeketaji ukome. Pia mila potofu za kurithi wajane mtazikomesha namna gani? Kwani watu wamefikia kurithi hata wajane wa UKIMWI kwa mila potofu. Pia dawa za ongezeko au kuongeza maisha zifike hadi Vijijini ili kuwapunguzia mwendo waliopima na wanaoishi mbali na hospitali ambazo wanapata huduma. Tunaomba mfanye kuwapa wagonjwa wa UKIMWI chakula cha protini pale ambapo wanachukua dawa. Ahsante.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa hatua hii ya kupitisha Muswada huu wa UKIMWI. Hali hii itasaidia kukomesha baadhi ya waathirika kuambukiza mabinti zetu kwa makusudi ili kuwakomoa na kusema bora wafe wengi. Kuna baadhi ya ya matajiri huwashawishi wasichana kwa kuwanunulia magari na kuwajengea nyumba wasichana wakati wakijijua ni waathirika.

Watu hao wanajulikana kila mahali lakini jamii imekaa kimya kutokana na hali ngumu ya maisha. Wasichana wengine hudiriki kusema bora kuishi ukiwa na mali kwa muda mfupi kuliko kuishi kwa muda mrefu ukiwa maskini. Kwa hiyo, tabaka hili haliogopi kuambukizwa na wengine huambukizwa kwa kutojua na kuendekeza tamaa. Muswada umekuja kwa kuchelewa, watu wengi wameshaathirika, lakini ni mwanzo mzuri. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kuungana na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa wale wote waliofiwa na watoto wake na familia zao. Vilevile nawapa pole kwa wananchi na Wabunge wenzangu kwa kufiwa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Benedict Losurutia. Mungu ailaze mahali panapostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Muswada huu ulioko mbele yetu. Katika Muswada huu wasiwasi wangu katika kipengele ambacho achukuliwe hatua mtu

ambaye anaambukiza VVU/UKIMWI kwa makusudi. Mtu huyu utamjua vipi kama anaambukiza VVU/UKIMWI kwa makusudi, kwa sababu mtu akishaona kama anajulikana katika mji au kijiji basi anahama na kwenda mbali asikojulikana na kuanza kuambukiza.

Naomba Serikali mtu yeyote ambaye anakwenda hospitali kwa sababu anaumwa basi apimwe kabla hajafanyiwa matibabu kama vile wanavyopimwa wajawazito bila ya kushauriwa ili Serikali iweze kupata takwimu halisi na hivyo kuepusha madhara makubwa zaidi kwani tunapoteza watu wengi nguvu kazi wanatutoka kwa wasiwasi wa kunyanyapaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba elimu zaidi na zaidi itolewe mpaka vijijini ili watu wapate kuondoa wasiwasi, waende wakapime bila ya wasiwasi na kama mtu ameathirika apatiwe dawa na vilevile lishe kwani watu wengi wa kijijini hawana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Prof. David Mwakyusa, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Naibu Waziri *Dr*. Aisha Kigoda, Katibu Mkuu, wadau wote na watendaji wote walioshiriki kuandaa Muswada huu muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuwa mstari wa mbele katika harakati za kupambana na ugonjwa huu mbaya wa UKIMWI. Serikali ilitengeneza sera ya kupambana na UKIMWI kisha iliandaa Mkakati wa kupambana na UKIMWI ambao ulikuwa chini ya *TACAIDS*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengi yaliyofanywa na Serikali, pamoja na kuendesha semina, warsha, makongamano na kadhalika. Bado palikuwa na ugumu wake kwani hapakuwa na sheria ya kuwabana wale wanaoambukiza kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, nina matumaini makubwa sasa kupitia Muswada huu maambukizo ya makusudi yatapungua kama sio kumalizika kabisa na nawaomba Wabunge wenzangu wakubali Muswada huu kupita.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupima VVU kwa lazima, naipongeza pia Serikali kuhamasisha wananchi kukubali kupima ili kuhakikisha kama hawana VVU au wanavyo ili waweze kujua namna ya kuweza kulinda afya zao. Pamoja na hamasa ya Serikali ya kuwahamasisha wananchi kupima, mimi naishauri Serikali kumpima kila mgonjwa afikapo hospitali ili tuweze kujua takwimu sahihi na kuwapa elimu wale ambao tayari wameathirika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya fedha za UKIMWI, naipongeza Serikali kwa kutenga Mfuko wa fedha wa kupambana na UKIMWI pamoja na

wahisani mbalimbali. Ni ukweli usiojificha kuwa Mfuko huu una lengo zuri sana bali watendaji wanautumia vibaya. Fedha nyingi zinatumika kwenye semina nyingi ambazo zimetosha badala ya kutumika kwa walengwa kwa maana ya kuwapa lishe na kusomesha yatima ambao wazazi walikufa kwa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, mila zilizopitwa na wakati, bado kuna mila zinazoendelezwa ambazo zinasababisha maambukizo mfano, kurithi wajane, ukeketaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mila hizo naomba zipigwe marufuku na sheria kali ziendelee kuchukuiwa dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, nina matumaini kuwa Muswada huu ukipitishwa utasaidia sana kuwakomesha wale ambao wamekuwa wakiwaambukiza wenzao kwa makusudi kabisa.

Mheshimiwa Spika, napenda nitamke rasmi kwa njia ya maandishi kuwa naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. USSI A. PANDU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara yake kwa kuleta mbele yetu Muswada huu wa Kuzuia na Kudhibiti UKIMWI ambao kwa sasa Watanzania wengi wanaendelea kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu elimu kwa umma, kama alivyosema Mheshimiwa Rais kwamba Tanzania bila UKIMWI inawezekana. Ni kweli lakini pamoja na Watanzania kupima lakini kama elimu kwa umma haitatolewa mafanikio yatakuwa madogo ya kupunguza maambukizi haya.

Hivyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba elimu kwa umma isiishie Mijini na ifike mpaka Vijijini ambako kuna watu wengi wanaokosa elimu hiyo ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu kupima kwa hiari, kama kweli tunataka kuishi na tuna lengo la kuondoa au kupunguza maambukizi ni lazima tukubali watu wote wapime UKIMWI.

Hivyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Afya kuwe na marekebisho ya Sheria kuona kwamba watu wote wanapima UKIMWI vinginevyo ugonjwa huo utaendelea.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu adhabu, bado ni ndogo miaka mitano (5) mpaka kumi (10) haitoshi, ikiwezekana mpaka miaka 20 ingeongezwa kwani kuna baadhi ya watu wanaoambukiza kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu sana. Kwani UKIMWI ni ugonjwa usiochagua yeyote aweze ambukizwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri nasaha ni jambo muhimu sana kabla na baada ya vipimo. Lakini elimu hiyo haitolewi vya kutosha mfano upo hai watu wengi wamejiua baada ya mshauri kumpa maneno ya kutisha kama ugonjwa hauna dawa subiri kifo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu Serikali ianzishe *course* maalum ya *psychology and councelling* ya muda mrefu, kuliko ilivyo sasa *course* ya wiki mbili ambayo haitoi ufanisi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kupima, suala hili ni la hiari vile vile ni lazima hasa kwa wajawazito na katika hospitali nyingi wanawapima wagonjwa bila hiari yao. Ushauri wangu kuwepo kifungu kinachotoa ulazima wa kila Mtanzania kupima ili udhibiti na uzuiaji uwe rahisi na hii itasaidia katika kujua uhalisia ni asilimia ngapi wameshaathirika ili wapatiwe dawa.

Mheshimiwa Spika, vifaa vya kupimia, Serikali iweke wazi ni vifaa vipi ni bora kupimia? Kwani vipimo vingi havitoi vipimo sahihi, mtu aweze kuambiwa anao kumbe hana.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ituambie mpaka sasa mashine za *CD4* ni ngapi nchi nzima na Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kuwa angalau kila kituo cha afya cha Kata kinapatiwa mashine ya *CD4* na vipimo sahihi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lishe, lishe ni muhimu sana kwa mtu yeyote hasa waathirika. Serikali imeleta Muswada wa kuzuia na kudhibiti UKIMWI na kuna vifungu vinavyoonyesha kuwa Serikali itatoa kondom na *support* kwa waishio na *HIV* na *AIDS*. Rejea kifungu cha 9, sasa *supports* ya aina gani? Ni kondom peke yake.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha tano (5) kinaonyesha Wizara itahakikisha virusi vinapungua au maambukizi yanapungua. *Promotion* hiyo nashauri isitoke juu Wizarani kwenda chini kwa maana ya kupeleka wataalam vijijini kwa siku moja *then* warudi. Bora Wizara itoe elimu kwa vikundi vya uhamasishaji kama vikundi vya sanaa vijijini na maeneo mengine waishio wananchi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16 kinaelezea usiri wa majibu, lakini inashangaza kuwa kuna baadhi ya hospitali wanatoa kadi maalum mfano Muhimbili zipo kadi za *blue.* Sasa Serikali haioni si siri tena kwani wana vitambulisho na Serikali haioni kuwa huo ni unyanyapaa? Na hili ni tatizo linalosababisha watu wasipime kuogopa kuwa *labled* na kunyooshewa vidole.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni kipengele cha adhabu. Serikali ianglie upya adhabu kwani itakuwa ngumu kujua ameambukizwa lini? Labda adhabu hii itekelezwe kwa wale watu wa mjini wanaojulikana wanaambukiza kwa makusudi na waanze kuichukuliwa hatua sasa kwa kuhojiwa na kutafutwa ushahidi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, wauguzi wawekewe bima lakini Serikali iangalie wale wazee na ndugu watunzao wagonjwa majumbani nao wasaidiwe katika elimu ya jinsi ya kumuuguza na kujikinga na maambukizi.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kwa kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *AU.* Hii ni sifa kubwa kwa Watanzania. Ninamwomba Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wetu maisha yenye afya tele na Mungu amtangulie katika uongozi wake. Napenda kuchangia kama ifuatavyo:- Kifungu 47 inasema atakayeambukiza virusi vya *HIV* kwa makusudi atatumikia kifungo, Je sheria hii inawabana vipi wanaofanya biashara ya kuuza miili yao watapimwa kwanza ili kujua walioathirika na *VVU/HIV* na wasioathirika? Serikali haioni kuwa bila kuwabana wanaofanya biashara ya kuuza miili yao, Sheria hii au kifungu hiki hakitatekelezeka ipasavyo? Kifungu 16 kinahusu usiri wa majibu kwa anayepima VVU kifungu 29. Kinazungumzia unyanyapaa kwa waathirika wa *HIV/AIDS.*

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wangu waathirika wa *HIV/AIDS* wananyanyapaliwa wa Wizara/Wahudumu wa afya na hakuna usiri wowote kwani muathirika anapoanza kuchukua dawa anapewa kadi ya kuchukulia dawa yenye rangi tofauti na kadi ya wagonjwa wengine; ana siku maalum ya kuchukua dawa na ana dirisha lililotengwa kwa ajili ya kuchukuwa dawa. Je, huko siyo kunyanyapaa? Kadi ya hospitali kwa ajili ya *ARV* ni kitambulisho tosha kuwa mgonjwa huyo amekwisha athirika je usiri uko wapi hapo? Kwa nini asiwe na kadi ya kuchukulia dawa kama ya mgonjwa wa malaria? Je, huko sio kumtangaza muathirika bila ridhaa yake?

Mheshimiwa Spika, kifungu 35 kinazungumzia Asasi *(NGOs)* zisizo za Serikali zinazojishughulisha na waathirika wa *HIV/AIDS.* Ninashauri matumizi ya pesa za Asasi hizi zijulikane kwa Serikali Asasi nyingi zinanufaisha watu binafsi na huduma wanazozitoa hazilingani na pesa wanazopewa. Ugonjwa wa ukimwi ni sawa na marathi mengine kama vile saratani, malaria, kipindupindu, ebola, lukemia, na kadhalika. Sasa kwa nini majibu ya waathirika wa *HIV/AIDS*yawe ya siri na kwa magonjwa mengine siyo siri. Serikali haioni kuwa usiri kwa waathirika ndio unaowapa kiburi waathirika kuwaambukiza wengine kwa makusudi?

Wanawake wajawazito hupimwa maambukizi ya *HIV/AIDS* ili kuzuia maambukizi kwa mtoto atakayezaliwa. Je, baba wa mtoto mtarajiwa habanwi na sheria kupima maambukizi? Je, kama wanaume wanaowapa mimba wanawake ambao wanagundulika kuathirika hawabanwi na sheria kupimwa VVU, Sheria hii itawabana wanaume kama hao?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba niungane na wenzangu kutoa pole kwa Ndugu na familia ya Marehemu Benedicto

Losurutia. Aidha nawapa pole wapiga kura wa Jimbo la Kiteto. UKIMWI hauambukizwi kwa tendo la ndoa tu zipo njia mbalimbali za kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumejitokeza tatizo kwa baadhi ya wale ambao wamejijua kuwa wameambukizwa. Hawa wanausambaza kwa makusudi na wanasema hasa kuwa hawatakufa peke yao, watakuwa na msururu wa wenzao. Kutokana na sheria hii ya kuzuia na kudhibiti UKIMWI itasaidia kuwabaini wale wote walioathirika na kuweza kujiepusha nao katika tendo la ndoa lisilo salama.

Mheshimiwa naibu Spika, pia kuna wale wanaotoa msaada wa damu, wakati mwingine inatokea mgonjwa wa ghafla anahitaji damu na mtoa damu kwa muda ule anatoa damu bila kujali kuwa amepima kwa marudio. Yeye anapimwa pale pale na jibu linakuwa ni *positive* ili hali ndio amepimwa pale pale na kupewa jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iliangalie hili utoaji wa damu wa papo kwa papo baada ya kumpima mtoaji damu.

Kuhusu waathirika wanaotumia dawa, hawa wanapata matatizo makubwa kutokana na lishe duni na uwezo mdogo kimaisha. Fedha zinazotolewa kwa ajili ya kuisaidia wenye VVU/UKIMWI hazitolewi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii itasaidia wale wote ambao wanaueneza UKIMWI kwa makusudi. Kuna wale ambao pia wana nyadhfa kubwa na wanaomba rushwa ya ngono ili wawapatie ajira baadhiya kina mama wanaofika maofisini mwao.

Mwisho naiomba Serikali itoe tamko hasa kwa wale baadhi ya madhehebu ambayo anapofariki mtu wao wanamuosha bila kutumia *gloves* wakati hawajui mfu huyo iwapo amefariki kwa UKIMWI.

Wengi wa waosha maiti wanapata UKIMWI kutokana na kitendo hicho cha kuosha maiti kwa vile uoshaji maiti ni ajira kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze wote mliohusika katika kuutayarisha Muswada huu.
Ninaunga hoja mkono, lakini ninazo hoja chache zifuatazo:-

(i) Kudhibiti ubora wa kondomu.
(ii) Kondomu zisambazwe kwa watu wote.
(iii) Uthibiti wa pesa za UKIMWI ni muhimu sana na lazima pamoja na *transparence.*
(iv) Adhabu ya matumizi mabaya ya pesa za UKIMWI isiwe kwa taasisi tu bali hata watu waliohusika kwani aliyetumia kuiba ni mtu na siyo taasisi.
(v) Baada ya kuwepo kwa taarifa za baadhi ya watu wachache kufahamika ya kuwa wameathirika lakini kuna baadhi ya watu wengine kujipeleka/kujitoa

na kushiriki tendo la ndoa pasipo na kinga ya aina yoyote kwa masharti ya kupatiwa pesa au kumnunulia vitu *properties.* Je hawa wanaojipeleka na kusema bora aishi maisha mafupi yenye raha badala ya kuishi maisha marefu yenye taabu na shida hawastahili kushitakiwa ?

(vi) Sheria itafsiriwe kwenye lugha nyepesi ya Kiswahili ili iweze kueleweka kwa watu wote.

Mheshimiwa Spika, ninarudia kuunga mkono hoja.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Nichukue fursa hii kuunga mkono wote waliotoa rambirambi kwa kifo cha Mheshimiwa B. Losurutia na pongezi kwa kuapishwa kuwa Mbunge. Mheshimiwa G. Rwakatare. Kwa juhudi zake katika kupambana na maambukizi ya *HIV/AIDS* na kutoa huduma bure kwa waathirika na janga hilo.

Muswada huu mimi nasema umechelewa. Laiti ungeletwa mapema usemi wa Tanzania bila UKIMWI ingekuwa imechukua nafasi yake siku nyingi, tukizingatia kushuka kwa maambukizi toka 7% kwenda 4% ya idadi ya Watanzania. Nasema Muswada umechelekwa kwa sababu wananchi wengi hasa vijana waliambukizwa virusi na wale waliojua fika kuwa ni waathirika eti wakisema wasife peke yao au eti walijaribu kuhakiki kuwa kweli nimwaathirika. Unanyanyapaa, unachangia sana usiri wa waliothairika kwa kuogopa kunyanyapaliwa. Kitendo cha usiri wa upimaji *HIV/AIDS* na utoaji majibu ni sehemu ya unyanyapaa kwa sababu magonjwa mengine mgonjwa akipimwa majibu hayafichwi japo hayatangazwi.

Tunaomba majibu ya *HIV/AIDS* yatolewe kama yale ya magonjwa mengine lakini tiba yao ibaki kuwa na kitengo maalum kwa huduma bora.Huduma kwa wagonjwa majumbani *(home based care)* wahudumu wa wagonjwa hawa ni jamaa na Ndugu wasio na elimu na wanaweza wakapata ugonjwa/maambukizi haya bila kujua.

Mtu wa namna hiyo akimwambukiza mtu ; kwa kurejea hali ya familia yake atashutumiwa kwa kuambikiza kwa makusudi. Nashauri elimu ya kupima kwa hiari iendelee kutolewa.

Sambamba na hilo naiomba Serikali iongeze huduma ya chakula kwa waathirika. Kubwa kuliko yote naomba waathirika wahamasishwe kujiweka wazi/kujitangaza ili wapewe huduma zote za Serikali na kupunguza unyanyapaa na maambukizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wachangia hoja inayohusu UKIMWI kwa kutoa mapendekezo yafuatayo :-

(i) Ninaamini kama Serikali ingesitisha dawa zinazotolewa bure ingekuwa ni fundisho kwa watu wanaoendekeza ngono. Sababu kubwa ni kuwa wangeshindwa kumudu gharama na kuamua kuacha ngono. Katika hili kwa waathirika wanapopata

dawa hizo wananenepa na kupoteza dalili zote za kuumwa. Hali ambayo inakuja kuwavutia watu na kuendeleza vitendo vya ngono.

(ii) Ningeshauri wale wote wanaoeneza UKIMWI kwa makusudi na wakijulikana washitakiwe.

(iii) Wapo watu wakubwa Serikalini na kwenye mashirika ya umma wanaocheza ugonjwa kwa kuwarubuni wanawake. Nina shauri watu wa namna hii wapigwe picha na kuzionyesha kwa kutumia vyombo vya habari ili wananchi wawaogope na kuwakimbia.

(iv) Kwa makusudi mazima Serikali iache kutoa dawa bure kwa waathirika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamuita Mheshimiwa Naibu Waziri lakini yeye atatumia dakika 15 kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Waziri, karibu!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuchangia, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Bara la Afrika. Hii ni heshima kubwa kwa Watanzania. Kwa hiyo, tumuombee afya njema na umri wake uwe mrefu ili aweze kumudu majukumu mengi aliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude P. Rwakatare, kwa kuapishwa majuzi kuwa Mbunge wa Viti Maalum. Tunamkaribisha sana, tukishirikiana tutaweza kusukuma gurudumu la maendeleo kwa nchi yetu. Vilevile, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Tanga, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapa pole sana jirani zetu wa Kiteto, kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Benedict K. Losurutia. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, Amen!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mingi sana ambayo wameileta kwa maandishi na kwa kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia sehemu chache tu ya wale waliozungumza lakini mambo mengine Mheshimiwa Waziri atamalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, alikuwa amezungumzia kuhusu fedha za UKIMWI ambazo zimepelekwa Wilayani anasema ziambatane na maelekezo ya jinsi ya kuzitumia ili ufuatiliaji uweze kufanyika. Hili tunakubaliana nalo na ushauri wake Wizara imeuzingatia. Lakini vilevile amesema wagonjwa wa UKIMWI wananyanyapaliwa kwa kuwapa kadi tofauti na

wagonjwa wengine na hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengine na kwamba hii itawazuia watu kujitokeza kwa ajili ya kupata matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba kadi zote za hospitali huwa zinaagizwa kwa kuzingatia rangi maalumu, kwa kuzingatia aina ya ugonjwa au huduma lakini vilevile pale tunapoona kwamba italeta matatizo basi Wizara itaangalia uwezekano wa kuweza kurekebisha hili.

Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, ameuliza, je, mtu ambaye anapimwa ili aweze kutoa damu kipimo kimoja kinatosheleza kuonyesha usalama wa damu yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo kimoja kinatosheleza kuonyesha usalama wa damu kwani ni kipimo kinachotumika, kina uwezo wa hali ya juu yaani *high sensitivity* ya kutambua kuwepo au kutokuwepo kwa maambukizi ya UKIMWI yaani zile *antibodies*. Aidha, damu inayokusanywa, ni kwa watu wenye uwezekano mdogo yaani *low risks profile* kuwa wameambukizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile amesema kwamba Serikali itoe tamko hasa kwa yale madhehebu ambayo mtu akifariki wanamuosha bila kutumia *gloves* kwani wengi wanaoosha maiti wamepata UKIMWI kwa njia hiyo. Elimu ya afya inayotolewa kuhusu UKIMWI huwa inasisitiza masuala kama haya hivyo hakuna haja ya kutoa tamko rasmi.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, ameulizia kuhusu asasi zinazotumia vibaya fedha za UKIMWI ambapo hili pia limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba, je, hizi asasi zinawajibishwaje? Vilevile ameuliza Serikali inadhibiti vipi fedha za UKIMWI zinazopewa asasi hizi? Kifungu cha 35 kuhusu Muswada ulio mbele yetu kinatoa adhabu kwa watu wote na taasisi zitakazotumia vibaya fedha za kudhibiti UKIMWI. Lakini vilevile ameuliza kwamba je, kuna mfano wa asasi iliyoadhibiwa na je, Serikali itakubaliana naye kuwa fedha zote za UKIMWI zitumike katika kusaidia waathirika kununua dawa, lishe, elimu vijijini na mashuleni?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ikipitishwa, adhabu zitaanza kutolewa rasmi na hizi fedha za UKIMWI zitatumika kuwapelekea Watanzania wote kitita cha afua zinazotumika kudhibiti UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuwakinga wale ambao hawajaambukizwa mijini na vijijini.

Mheshimiwa Guido Gologolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, Chunya Magharibi, aliuliza kwamba ikiwa sasa hivi Wizara ina upungufu mkubwa wa watumishi kwenye Zahanati zetu hasa kwenye Jimbo lake la Songwe, je, shughuli hii ya utoaji elimu kwa wananchi Wizara inashughulikiaje suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau wengine huelimisha umma kuhusu UKIMWI hivyo suala la upungufu wa watumishi halitaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Muswada huu.

Lakini vilevile ameuliza Wizara haiwezi kuanzisha vituo vingine kwenye kituo cha afya cha Mbuyuni na kwenye Zahanati ya Saza, Kapayaya na zile ambazo amezitaja?

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za kutoa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI zinaendelea kupanuliwa kwa awamu kulingana na uwezo wa Serikali. Hivyo, lengo ni kufikia ngazi zote za huduma ikiwa ni pamoja na Zahanati ambazo amezitaja.

Vile vile ameulizia wale ambao wameathirika lakini hawajajitangaza na wanajulikana kuendelea na ufuska, Sheria inasemaje? Lakini vilevile ameuliza Sheria inasemaje kwa yale madhehebu ambayo hayako tayari kuhamasisha matumizi ya kondomu?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili litatekelezwa kwa kuzingatia kifungu cha 51 cha Muswada huu kwa wale ambao wanajulikana wameathirika lakini wanaambukiza wenzao kwa makusudi au bado wanaendelea na mambo ya ufuska kama alivyozungumza yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Serikali hailazimishi madhehebu ya dini ambayo hayako tayari kuhamasisha matumizi ya kondomu ikiwa inapingana na imani zao. Suala hili limezingatiwa katika kifungu cha 53 cha Muswada huu.

Lakini vilevile ameulizia kuhusu Kitengo cha Utafiti wa Tiba dhidi ya Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kilichopo Muhimbili kwa kutumia dawa za asili yaani mitishamba kwamba je, bado hakijapata ufumbuzi wowote kupitia dawa hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba wameainisha mitishamba inayosaidia kuongeza uwezo wa mwili kutokana na magonjwa nyemelezi lakini mpaka sasa hakuna dawa yoyote ya asili iliyothibitishwa kwamba inatibu UKIMWI, hivyo uchunguzi bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, aliuliza kuhusu kifungu cha 23(3) kwamba kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa watu kuhusu baadhi ya kondomu kama *Salama Condoms* kwamba kondomu hizi hazina kiwango cha ubora cha *TBS* na kwa nini basi *TBS* isiainishe aina chache za kondomu badala ya aina nyingi kuingizwa nchini bila kuwa na viwango?

Mheshimiwa Naibu Spika, kondomu zote zinazoingizwa nchini zinapimwa na pia zinathibitishwa ubora wake na *TBS* kabla hazijasambazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile amesema kwamba viongozi wa dini wamekuwa wakikataza matumizi ya kondomu kwa waumini wao, hata hivyo, waumini hao baadhi hawana uaminifu wa ndoa na wanapata UKIMWI na kuambukiza wengine, kwa nini Serikali isiingilie kati?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaruhusu uhuru wa imani ya dini kwa kila mtu. Hivyo Serikali haiwezi kuingilia suala hili kwa madhehebu ya dini kukataza

matumizi ya kondumu lakini sisi kama Serikali tutatumia njia nyingine ili kuweza kuwaelimisha watu waweze kuepukana na balaa hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja kwamba kuna waganga wengi wa kienyeji ambao wanatangaza uwezo wa kutibu UKIMWI na pia kuna baadhi ya Viongozi wa dini wanatangaza uponyaji wa UKIMWI kwa njia ya maombi, je, Serikali iko tayari sasa kupiga marufuku matangazo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakataza mambo haya kwa mujibu wa kifungu cha 27.

Mheshimiwa Mbunge aliuliza kwamba katika jedwali la marekebisho kumekuwa na matumizi mabaya ya misaada au fedha zinazotolewa na Serikali na wafadhili na pamekuwepo pia na vikundi vingi mno vya kudhibiti UKIMWI vinavyopewa misaada na fedha, je, ni hatua gani zinachukuliwa ili kudhibiti ubadhilifu huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu hiki cha 35(1), kimewekwa kwa lengo la kudhibiti ubadhilifu huu.

Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, alisema kwamba sehemu ya nne, kifungu cha 15(5) na 16 mwanamke mwenye mimba anapoamua kwa hiari kupima UKIMWI akijifungua haruhusiwi kunyonyesha, je, hapo si kwamba usiri wa hali yake unapotea? Je, hali hii inasaidiwa vipi ili wajawazito wasinyanyapaliwe? Lakini vilevile ameuliza Serikali ina mpango gani kuhusu lishe ya watoto ambao wazazi wao watakuwa wamezuiliwa kuwanyonyesha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa akina mama hawa wanaelimishwa sababu na nia ya kutekeleza mpango huu wa kupima, katika mazingira hayo, hakuna usiri uliovunjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Serikali haina mpango wa kutoa lishe kwa watoto ambao wazazi wao watakuwa wamezuiliwa kunyonyesha na badala yake wazazi wanaelimishwa jinsi ya kutumia vyakula vilivyopo katika mazingira yetu ili kukidhi mahitaji ya lishe ya watoto hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, alisema kwamba Idara ya Kinga iimarishwe ili kushughulikia masuala ya UKIMWI na wahudumu wa Wizara iwe ni nje ya Wizara lakini siyo *NGOs*. Lakini vilevile alisema kwamba Wizara ya Afya ishauri Wizara ya Elimu iingize katika silabasi za shule mafunzo ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kudhibiti UKIMWI ni la sekta zote na wadau wengi. Hivyo, wadau wa Idara ya Kinga pekee hawataweza kumudu majukumu yote haya. Aidha jukumu na suala la elimu ni kwamba jukumu hili litaachiwa Wizara ya Mafunzo ya Elimu na Ufundi kama ilivyoainishwa katika jedwali la marekebisho katika *paragraph E* kifungu cha 7. Kwa hiyo, suala hili litashughulikiwa katika *By Laws*.

Mheshimiwa Castor Ligallama, amesema kwamba Serikali izuie waganga wa jadi kutangaza kama wao wanatibu UKIMWI, hili tumeshalizungumza na linazungumziwa katika kifungu cha 27.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kondumu kugawiwa bure, tumesema kwamba hili Serikali inalitekeleza. Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, ameshauri kwamba Serikali ianzishe Mfumo Maalum wa Saikolojia na ushauri wa muda mrefu si ya wiki mbili kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliopo wa kutoa mafunzo ya kujiendeleza unakidhi mahitaji. Hata hivyo Idara ya Ustawi wa Jamii, inaendesha mafunzo ya ushauri nasaha na kozi mbalimbali za Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mbunge pia amesema kwamba pawepo na kifungu kinachotoa ulazima wa kila Mtanzania kupima ili udhibiti wa virusi na VVU uwe rahisi. Sera ya kudhibiti UKIMWI nchini inasisitiza kupima kwa hiari na siyo kwa lazima. Lakini vilevile amesema kwamba Serikali isambaze sasa mashine za *CD4* nchi nzima na Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha angalau kwenye kila kituo cha afya kinapatiwa *CD4*?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nia ya Serikali kuona kwamba mashine hizi zinapatikana katika vituo vya kutolea huduma nchini lakini kwa sasa huduma hizi zinatolewa kulingana na uwezo wa Serikali. Mpaka sasa hivi tumefikia ngazi ya Mkoa na pesa itakaporuhusu basi itakwenda mpaka ngazi za chini.

Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, aliomba kudhibiti ubora wa kondomu, suala hili limezingatiwa kwa mujibu wa kifungu cha 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kondomu kusambazwa, kama nilivyosema mwanzo, suala hili linatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu alizungumzia pia udhibiti wa pesa za UKIMWI kwamba ni muhimu sana na ni lazima uandamane na uwazi. Fedha za Serikali zinadhibitiwa kwa kanuni na taratibu za fedha jambo ambalo mamlaka husika hutekeleza. Aidha, Sheria hii itasimamia suala hili kwa kupitia kifungu cha 35.

Mheshimiwa Mbunge vilevile alisema kwamba baadhi ya watu wachache hufahamika kuwa wameathirika lakini kuna baadhi ya watu wengine hujipeleka na kushiriki tendo la ndoa pasipo na kinga ya aina yoyote, watu hawa wanaojipeleka watachukuliwa hatua gani? Suala hili litasimamiwa kwa mujibu wa kifungu cha 51 cha Muswada huu.

Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, ameuliza kwamba kuna adhabu gani kwa wakeketaji? Pia akaushauri kwamba mila potofu za kurithi zinaendeleza UKIMWI hivyo zipigwe marufuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linatekelezwa katika Sheria nyingine kwa hiyo haliwezi likajitokeza hapa. Lakini vilevile suala hili linahitaji kuelimisha jamii na ni mtambuka na linahitaji kushughulikiwa na Sheria nyingine pamoja na jamii.

Mheshimiwa alishauri pia kwamba watumiaji wa dawa za UKIMWI wapewe chakula. Serikali haina uwezo wa kutoa chakula kwa kila muathirika bali ushauri kuhusu lishe utatolewa kwa wagonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Diana M. Chilolo, ameshauri kila mgonjwa afikapo hospitalini apimwe UKIMWI. Kama tulivyosema, suala la kupima UKIMWI ni la hiari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pi alishauri kwamba fedha ziende kwa yatima badala ya kufanya warsha na makongamano, ushauri huo umezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mila potofu kama kurithi wajane, kama nilivyozungumza, suala hili linahitaji kuelimisha jamii.

Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, ameongelea kuhusu Vifungu vya 5, 12(3) na 49, anasema adhabu zinazotolewa ni ndogo kulingana na uzito wa makosa. Anapendekeza adhabu ziongezwe. Sheria hii imezingatia haki za binadamu katika kutoa adhabu.

Vilevile anasema kwamba Serikali ihakikishe kunakuwa na nyenzo za kupima *HIV* kwa watu binafsi kama ilivyo kwa wanaopima mimba. Upimaji wa virusi vya UKIMWI ni lazima ufanyike chini ya usimamizi wa Wataalamu wa Maabara.

Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mbunge wa Mtoni, yeye amesema kwamba elimu ya afya kwa umma isiishie mijini bali ifike huko vijijiji. Lengo la kutunga Sheria hii ni pamoja na kuelimisha umma kuhusu haki zao za msingi na kusisitiza kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI katika ngazi zote.

Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mbunge wa Viti Maalum, amezungumzia kuhusu adhabu kali kwa wanaoeneza UKIMWI kwa makusudi, nimelizungumzia na Kifungu cha 47 kimeainisha adhabu hiyo.

Mheshimiwa Pindi H. Chana, yeye amezungumzia Kifungu cha 6(4) kwamba *TACAIDS* wawe na ofisi kila Wilaya ili kuepuka ucheleweshaji wa mipango yake, ushauri huo utawasilishwa *TACAIDS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amesema kwamba wanawake wapewe kipaumbele kupata elimu, hili tumeshalizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu adhabu ya kifungo kisichopungua miezi sita kwamba kiongezwe, Kifungu cha 12(3) adhabu zinazotolewa zimezingatia maoni ya wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, amependekeza pia kwamba watumishi na wahudumu wengine wa afya wakikutwa na virusi vya UKIMWI wasiruhusiwe kuendelea kutoa huduma, katika Kifungu cha 15, Muswada huu unakataa unyanyapaa na huo ni unyanyapaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alipendekeza Kifungu cha 36(2)(a) kubadili neno "*Chairman*" kuwa "*Chairperson*". Neno *Chairperson* ni *gender neutral* kwa misingi ya lugha za kisheria.

Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, amesema muda umefika kwa wafanyakazi wa maabara kuwekewa Bima ya Maisha kutokana na athari ambazo zinaizingira kazi zao. Pia ameshauri kwamba kiwepo Kifungu cha kuwalazimisha kupima watakaotaka kuoana. Hii hapa tumeijibu katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Ussi Ame Pandu na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir walizungumzia mambo yote yanayohusiana na elimu, vikundi vya vijana.

Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, amesema kuwa mambo ya VVU yafanyike kwa watu wa Bunge, viongozi na watu wengine, nafikiri mambo yote haya tulikuwa tumeyajibu hapo mwanzo na tutayazingatia kwa kadri tulivyojibu.

Mheshimiwa Rosemary Kirigini alisema kwamba elimu ya afya kwa jamii na mkakati wa kupambana na UKIMWI uwe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mkakati wa Taifa kudhibiti UKIMWI unaandaliwa na kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu moja ya afua zitakazotekelezwa ni elimu ya afya kwa umma.

Mheshimiwa Janeth Massaburi, alisema kwamba wapo watu wanaoeneza UKIMWI kwa makusudi hasa matajiri na kuwaambukiza wasichana kwa hiyo yeye anasema Muswada huu umekuja wakati muafaka. Tunasema tunamshukuru kwa kuliona hilo na Wabunge wengine wote ambao wameliona hilo.

Mheshimiwa Martha Umbulla amesema kwamba Sheria izingatie jinsia na *NGOs* zinazotekeleza afua za UKIMWI zisimamiwe na Serikali hususani katika masuala ya matumizi ya fedha. Tumeshalijibu lakini vilevile Sheria hii inatambua na inazingatia masuala ya jinsia kama yalivyojitokeza. Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga ametoa ushauri kwamba *condom* zitolewe kwa waathirika tu na aidha bei ya kondom ipunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuzuia maambukizi ya UKIMWI linagusa kila mtu hivyo kondomu zinatolewa kwa watu wote na kusambazwa bure nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Uliacha dakika tano siyo? Sawa lakini sasa Waziri ili aweze kukamilisha hoja mbalimbali tulizozitoa, tutaahirisha saa 11.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo kutoka utawala wa Ofisi ya Bunge kwamba Wabunge ambao ni wanahisa katika Benki ya Wananchi ya Dar es Salaam, wanatakiwa wakutane leo tarehe 1/02/2008 katika Ukumbi wa Dodoma Hotel kuanzia saa 1.00 usiku, lakini tutakuwa bado tupo hapa. Balozi Rupia ambaye ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Wananchi Dar es Salaam anawatangazia Wabunge wote wenye hisa katika benki hiyo kuwa kutakuwa na sherehe ya kukabidhi vyeti vyao vya hisa leo Ijumaa tarehe 1/2/2008 katika Ukumbi wa Dodoma Hotel kuanzia saa 1.00 usiku.

Waheshimiwa Wabunge, mimi sina tangazo lingine, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 Jioni.

(*Saa 7.00 Mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge mchana, tulishaanza kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, sasa namwita mtoa hoja halafu tutaendelea na hatua zinazofuata. Mheshimiwa Mtoa hoja, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi nyingine ili niweze kuhitimisha hoja iliyoletwa mbele ya Bunge jana asubuhi.

Kabla sijaendelea, ninapenda nitoe pongeza za dhati kwa Watanzania wote, kwa Rais wetu kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *African Union. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu na wengine waliochangia kwa maandishi. Wote nawashukuru, wametusaidia sana katika utekelezaji wa Sheria hii pale itakapopitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi uliyompa Naibu Waziri wangu asubuhi ambapo hoja za Wabunge ishirini na moja alizitolea ufafanuzi na hawa waliobaki, nitatoa ufafanuzi mchana huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kawaida, naomba niwatambue waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na kwa utaratibu wa kawaida najua kwamba hizi dakika hazitahesabiwa kwa sababu orodha ni ndefu sana.

**NAIBU SPIKA:** Zinahesabiwa. Aaah, hazihesabiwi, ndiyo, sawasawa.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Omar Shaban Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii; Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Profesa Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Rosemary Kirigini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa maandishi wako arobaini na moja, nao ningependa niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Jadi Kadika Mgeni, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa George Malima, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Nuru Bafadhil, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Amir Ali Ameir, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Saverina Mwijage na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Ussi Pandu, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Siraji Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mheshimiwa Muhonga Said Luhanywa, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Felix Kijiko na Mheshimiwa Felister Bura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Wabunge wenzangu walioboresha Muswada na kutusaidia jinsi tutakavyojipanga wakati wa utekelezaji.

Nianze kwa kusema kwamba, hoja zilizotolewa ni nyingi, nyingine zilikuwa zinajirudia na katika muda ulionipa, nitajaribu kuzigusia zote, lakini endapo nitashindwa kufanya hivyo, Wizara inaahidi kwamba majibu yote yatatolewa kwa maandishi kwa kila Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo yaligusiwa na Wabunge wengi na niliona ni vema nianze na haya mambo ya jumla kabla sijaanza kumtambua kila mmoja alisema nini.

Moja ni kuhusu elimu kwa umma, wote waliochangia katika masuala ya elimu katika mchakato mzima wa Sheria hii, wametoa msisitizo katika eneo hili na wamesema kwamba isiishie mjini tu, mipango iendelee mpaka vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii inasisitiza hili na tumeweka kipengele cha kuziwezesha Halmashauri na kuweka mazingira mazuri kwa wadau wengine ili kutoa elimu hiyo.

Kulikuwa na ushauri kwamba Elimu ya UKIMWI ianze kutolewa katika shule za msingi. Napenda kutoa taarifa kwamba *handbooks* zimeshatayarishwa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Wizara yangu na baadhi ya Walimu wamepewa kozi maalum katika eneo hili. Kinachofikiriwa sasa hivi ni endapo somo hili litaweza kuingizwa katika mitaala, mazungumzo bado yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *condoms* limejitokeza mara nyingi. Kifungu cha 9, hakikueleweka kwa baadhi ya Wabunge, kifungu hicho kinazungumzia habari za gender responsive HIV and AIDS education, kama ni kitu kimoja, distribution of condoms kama kitu kingine na support to people living with AIDS, wengi walitafsiri kwamba distribution of condoms ni kwa wagonjwa wenye ugonjwa wa UKIMWI ambayo si sahihi. Activities hizi tatu zilizozungumzwa zinajitegemea, condoms zinatolewa kwa watu wote bila kujali kama mhusika ameambizwa au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine kuhusu *condoms* ni kwamba, baadhi ya Wabunge walisema *condoms* nyingine zina ubora hafifu, kwa hiyo Serikali iruhusu kampuni chache tu kuingiza *condoms* hapa nchini. Ningependa niwahakikishie Wabunge kwamba *TBS* inazihakiki na kuziruhusu au kuzikataa *condoms* zote ambazo hazina ubora kuingizwa hapa nchini. Tunaomba basi endapo kuna *consignment* imeonekana kuwa haina ubora unaotakiwa, wananchi watoe ripoti *TBS* au katika vituo vyovyote vya kutolea huduma za afya ili hatua za haraka zichukuliwe.

Aidha, hapa nchini tuna soko huria, kwa hiyo itakuwa vigumu kuzikatalia baadhi ya kampuni kuleta vifaa labda kama bidhaa zake ni hafifu na ni imani yangu kwamba tukiweza kuboresha usimamizi wa ubora wa *condoms* wingi wa *importers* unaweza kupunguza bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na wazo kwamba *condoms* zigawiwe katika Magereza. Napenda kusema kwamba tunauchukua ushauri huo na kuangalia Sheria za Magereza zinasemaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba *condoms* ni ghali Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza bei, ningependa kusema kwamba *condoms* zinazotolewa na Serikali zinatolewa bila gharama yoyote, ni za bure. Zile tunazozipata katika maduka

binafsi, bei yake inategemea soko. Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba *condoms* tunazozitoa ambazo ni za bure ziweze kuwafikia wananchi wote vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na malalamiko mengi kuhusu *NGOs* ambazo zinashughulika na masuala ya UKIMWI. Wabunge walionyesha kutoridhishwa na matumizi ya pesa na utendaji wa *NGOs* zinazoshughulikia masuala ya UKIMWI. Kulikuwa na kauli kwamba pesa za UKIMWI haziwafikii walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujue kwamba hadi sasa tulikuwa hatuna Sheria yoyote iliyokuwa inazibana hizi *NGOs* na ndiyo maana moja ya maudhui ya Sheria hii ni kuwabana hawa watakaofuja pesa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine walitoa angalizo kwamba watumishi na vyombo vya umma havikutajwa katika Sheria kwa maana ya kwamba wanaofuja si mashirika binafsi tu. Ninapenda kusema kwamba hilo tuliliona na ukiangalia Kifungu cha 35(2), kipo katika jedwali ambapo wafanyakazi wa Serikali au vyombo ya Serikali vikifuja pesa hizo nao watachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mmoja wa Wabunge alisema adhabu wanayopewa wanaofuja pesa hasa kwa upande wa *NGOs* ni ndogo kwa sababu hawa ni watu wanaokula mamilioni ya pesa na kwamba tungeangalia hizo adhabu na niahidi kwamba suala hili litaangaliwa na tutaoanisha na Sheria za *NGOs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la pesa za kupambana na UKIMWI. Inasemekana kwamba pesa kwa mamilioni zinatumika kwa semina na kongamano na kwamba mwelekeo ubadilike ili sasa zipelekwe kwa waathirika. Ninapenda kutoa ripoti kwamba pesa zinazotumika katika semina, warsha na kongamano katika tafiti zetu ni asilimia 1.2 ya bajeti ya mpango huu. Ukweli ni kwamba pesa zinazotengwa kwa ajili ya waathirika ni nyingi, labda tatizo usimamizi ni mbovu na kama mlivyoona, Muswada huu umejikita katika kurekebisha kwa nia ya kuwabana wanaofuja pesa hizi.

Hata hivyo, ikumbukwe kwamba ili tushinde vita hivi vya UKIMWI, njia pekee ni kuhakikisha kwamba asilimia 93 ya Watanzania ambao hawana UKIMWI hawapati UKIMWI. Nyenzo pekee tuliyonayo ili kuwafanya Watanzania wasipate UKIMWI, ni hao hao Watanzania kubadili tabia na kuuelewa ugonjwa huu vizuri na njia pekee ya kufanya hivyo, ni elimu na ushawishi, semina, warsha, kongamano, mikutano ya hadhara, vipindi vya redio na TV, ni baadhi ya *educational programmes*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala lililojitokeza mara nyingi kuhusu upimaji kwamba usiwe wa hiari. Baadhi ya Wabunge wamesema kwamba kila mtu anayekwenda hospitali apimwe kama ilivyo kwa mama wajawazito.

Kwanza, ninapenda kusahihisha kwamba upimaji wa akina mama wajawazito ni wa hiari. Mama anapewa ushauri nasaha na ana hiari ya kukataa au kukubali kupimwa.

Pili, ni kwamba, upimaji ni suala la kisera na pia ni haki za binadamu na kifungu (j) ambacho kipo katika jedwali la marekebisho kinasomeka kwamba:-

"*Every pregnant women and the man who is responsible for the pregnancy or spouse and every person…*".

Kwa hiyo, kipengele cha kumhusisha mume au mtu yeyote ambaye amempa mimba yule mama pia kimeongezwa ili wote waweze kupewa ushauri nasaha kama watataka wapimwe kwa hiari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa taarifa kwamba kuna *pilot study* inayoendeshwa hivi sasa katika sehemu kadhaa za nchi ambapo Daktari anatoa ushauri kwa kila mgonjwa anayemwona kwa nia ya kumshawishi atolewe damu ili ajue hali yake. Daktari huyo anakuwa na vifaa vya kupimia katika chumba chake na mgonjwa anayekubali kupimwa anafanyiwa hivyo hapo hapo ofisini na kupewa majibu hapo hapo ofisini. Wengi wamejua afya zao kwa njia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende kwa wachangiaji mmoja mmoja na masuala ambayo nimeyagusia sasa hivi sitayarudia tena.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, alitoa mapendekezo mengi katika kuboresha Muswada huu na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati ndiyo msingi wa jedwali la marekebisho.

Vile vile alishauri kwamba Muswada ukipitishwa, Sheria hii itafsiriwe kwa lugha za Kiswahili na kanuni ziandaliwe mapema. Hili tumelipokea na tutalitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwakilishi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab alisema Kifungu cha 12 kiondolewe kwa kuwa Kifungu cha 5, kinatosheleza. Kifungu namba 5, kinatoa wajibu wa ujumla na *heading* yake imeandikwa *general duties.* Ni wajibu wa Wizara kuhakikisha usalama katika sehemu ya utoaji wa huduma za afya wakati Kifungu namba 12 kinatoa wajibu mahsusi kwa wataalam wa afya kuhakikisha kwamba wanazingatia taratibu za usalama ambazo zimetajwa kwenye Kifungu namba 5. Kwa misingi hiyo, hakuna haja ya kufuta Kifungu namba 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu akasema Kifungu namba 9, kwa nini *condoms* zitolewe kwa wanaoishi na *virus* vya UKIMWI tu, hili nimekwishalizungumzia.

Alisema pia Kifungu namba 11(5), hakina sababu ya kuwepo kwa vile adhabu zimetajwa kwenye Kifungu namba 47 cha Muswada. Hivi Vifungu ni tofauti kwa sababu Kifungu alichokitaja kinalenga wanaojitolea damu na viungo kwa ajili ya wagonjwa wanaohitaji ambapo Kifungu namba 47 kinazungumzia wanaoambukiza UKIMWI kwa makusudi.

Vilevile alisema Kifungu namba 16(1), kinazungumzia kwamba upimaji wa UKIMWI utakuwa ni siri je, ni mazingira yapi yatasababisha kuvunja huo usiri? Hayo yameainishwa katika Kifungu namba 18.

Halafu alisema Kifungu namba 26(c), kwa nini mtaalam wa afya atakayepata maambukizi ya UKIMWI akiwa kazini asikatiwe bima? Hili suala litafikishwa mahali panapohusika, lakini tunajua kwamba suala la kiwango cha fidia litaamuliwa na Mahakama kulingana na uzito na mazingira ya uambukizaji wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, alisema pia Kifungu namba 27, taarifa ya tiba ya UKIMWI lazima iwe na uthibitisho wa kisayansi, Kifungu hiki kimezingatia mazingira ya nchi? Tunasema ndiyo kwa sababu kipengele hiki kinalenga kuzuia habari ambazo hazikuthibitishwa kisayansi na ambazo zinaweza kupotosha wananchi, jambo ambalo limekuwa likitokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia akauliza kwa nini Wizara inataka kuunda Kamati ya Utafiti wakati tayari kuna Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (*NIMRI*)? Ningependa kutoa taarifa kwamba Kamati hii haitafanya kazi zinazofanywa na *NIMRI* bali itajihusisha na kazi za kutafuta rasilimali kwa ajili ya kufanya utafiti, kuratibu tafiti, kupitia maandiko (*research proposals*) kwa ajili ya utafiti wa UKIMWI na kupendekeza maandiko ya kipaumbele na kuyapatia fedha.

Mheshimiwa Mbunge pia alizungumzia pia kuhusu elimu ya UKIMWI kufundishwa mashuleni, hili pia nimeshaligusia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Msindai alisema UKIMWI siyo janga, kwa hiyo Wizara ya Afya isimamie mambo yote yanayohusu ugonjwa wa UKIMWI. UKIMWI ulizinduliwa kama ni janga la Taifa linalohitaji ushiriki wa sekta zote kutokana na athari mbalimbali ziletwazo na ugonjwa huu. Ni kweli ni ugonjwa lakini athari zake zinagusa kila sekta, ndiyo maana ikaonekana kuwa chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye mratibu wa shughuli zote za Serikali ndiyo mahali sahihi.

Pia alisema suala la UKIMWI liingizwe kwenye mitaala ya shule za sekondari, nimelizungumzia hilo.

Vilevile alizungumzia kuhusu kuongezwa kwa kipengele cha kuwataka viongozi wapimwe kwa lazima. Hii itakuwa inavunja haki za binadamu. Pia alisema kwamba asilimia ya maambukizi haijashuka. Nadhani hii inatokana na ripoti tuliyosema kwamba sasa hivi ni asilimia tano, lakini ndiyo *data* ambayo tunayo, ndiyo tuna-*base* hapo mpaka tutakapopata takwimu zingine, lakini sasa hivi tunasema asilimia tano ya Watanzania wameambukizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya anasema watu hawana uwezo wa kununua *condoms*, nadhani hili nimeligusia.Pia alisema Kifungu cha 26, kuhusu fidia itakuwa kiasi gani? Serikali haiwezi kukisia, ni suala la Mahakama kwa sababu huwezi kuthaminisha afya ya binadamu kwa pesa. Alizungumzia pia kuhusu

vipimo vya kupima UKIMWI vinavyotumika nchini kwamba havijapitishwa na Shirika la Afya Duniani. Vipimo vyote tunavyotumia yaani *Capellos, Determine, SD Bioline* na *Unigola,* vimesajiliwa na kuidhinishwa na Shirika la Afya duniani.

Alizungumza pia kwamba Kifungu cha 47, kina utata kuhusu uambukizaji wa UKIMWI kwa makusudi. Suala hili kusema kweli ni la Mahakama. Tumepata malalamiko mengi sana ya watu ambao wanawajua watu ambao wanaambukiza UKIMWI na hapa katika mazungumzo toka jana watu wamefikiri ni wanaume peke yao, wapo na wanawake pia wanafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Benson Mpesya, alisema usiri unazingatiwa kwa watu wakubwa tu wanapofariki na akashauri kwamba hata wakubwa wakifa tusiambiwe wamekufa kwa *Blood Pressure*. Hili suala liko nje kidogo ya maudhui ya Muswada huu, hatuwezi kulitekeleza kwenye Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alisema kwamba Kifungu cha 15, kwamba wagonjwa wote wanaokwenda hospitali wapimwe, hili nimeshalizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Said Nkumba, amezungumza habari za fedha za UKIMWI kwamba haziwafikii walengwa na kwamba hizi hazina mwenyewe zinatafunwa, hili nimeshalizungumza.

Pia alisema kwamba ushauri nasaha uondolewe, ninapenda kujibu hivi, ushauri nasaha ni utaratibu ulioandaliwa kwa mgonjwa kwa huduma yoyote ile ambayo itamwathiri kisaikolojia. Hivyo, siyo sahihi kuondoa ushauri nasaha bali muda wa kutoa huduma hii utatofautiana kutokana na uelewa wa mteja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alisema kwamba upimaji usiwe wa hiari, hili nimeshalijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, alizungumzia pia kuhusu elimu ya UKIMWI kwamba iwekwe kwenye mitaala ya shule za msingi, hili nalo nimeshalijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Suzan Lyimo, yeye kwa mawazo yake ni kwamba UKIMWI si suala la Wizara ya Afya peke yake, ni sahihi liwe chini ya ofisi ya Waziri Mkuu. Pia alisema kwamba uenezaji wa makusudi wa UKIMWI ufafanuliwe yaani *intentional*, hili ni suala la Mahakama na kwamba wafungwa waathirika watapewa chakula magerezani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wafungwa waathirika watahudumiwa kama wafungwa wengine wenye matatizo maalum ya kiafya. Kuna wengine wana kisukari, wanapewa chakula tofauti na wenzao, kwa hiyo na hawa pia watahudumiwa kufuatana na hali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kifungu cha 26 alisema, tutatambuaje mfanyakazi wa afya kama kapata UKIMWI sehemu ya kazi na wala si ngono? Kwenye *schedule* tutaweka *protocol* maalum ambayo zitatumika kushughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia aliuliza wale watakaohudumia wagonjwa majumbani wakiambukiza, watafidiwa na nani? Watumishi wa afya wanapewa fidia kulingana na masharti ya mikataba yao ya kazi, ndugu watajihudumia wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia alisema wanaume wote Tanzania watahiriwe. Tuna sera na mambo haya yanaweza kufanywa. Ni kweli kuna ripoti za tafiti zilizofanywa Uganda, Kenya na Afrika Kusini, zinazoonyesha kwamba kutahiri wanaume kunapunguza uwezekano wa kupata virusi kwa asilimia sitini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi bado tunaliangalia kwa sababu hapa kwetu linafanywa, inaweza kuwa kimila wakati mwingine hata kidini. Ukweli ni kwamba maeneo ambayo mila zinasema lazima kutahiri, idadi ya wagonjwa ni chache. Kwa hiyo, tunaliangalia hili na kujiandaa kwa sababu wenzetu Uganda walipoweka kwenye sera yao walijitokeza watu wengi, hospitali zikawa hazifanyi kazi nyingine isipokuwa kutahiri tu. Kwa hiyo, sisi tunaangalia na kutazama tutajiandaaje hapo tutakapoingia kwenye sera hiyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme vile vile Lesotho ambako ni nchi ndogo na wanatahiri karibu wanaume wote, wao wana UKIMWI yaani asilimia ya *prevalence* ni kubwa kuliko hapa kwetu. Kwa hiyo, haya mambo yanatuchanganya kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Mtulia, alisema mashine za kupimia UKIMWI yaani *testing kids* zipelekwe katika ngazi zote za kutolea huduma. Tunakubaliana naye na kwamba tutakwenda polepole kama tunavyofanya mpaka hapo tutakapoweza kupeleka *testing kids* hizo katika ngazi zote.

Alisema pia Kifungu cha 2, mila potofu zitajwe zote waziwazi kama kurithi wajane, kutakasa na kadhalika. Nadhani hii tungeiacha bila kutaja kwenye Sheria kwa sababu ikiibuka nyingine ina maana tena tulete hapa Bungeni ili tuiweke kwenye hii orodha. Lakini kifungu namba 4(1)(d), Muswada huu unagusia pia Sheria nyingine. Suala hili litaangaliwa wakati wa kuwianisha na ku-*harmonise* Sheria nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya afya ya UKIMWI kupelekwe kwenye shule zetu, hilo nimeshalizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, anasema kuna migongano ya vifungu 15, 17, 46 na 48. Tulipoviangalia, kusema ukweli hakuna mgongano wowote. Kifungu cha 15 alishauri ifutwe, kifungu hiki kinabainisha maeneo ambayo mtu anaweza kupimwa bila hiari hususan maeneo yanayohitaji utoaji wa damu na viungo ama kosa la kujamiiana, kwa hiyo hatuwezi kukifuta kifungu hicho. Alisema

pia watu wanaojiambukiza kwa makusudi waadhibiwe na hili suala haliko kwenye maudhui ya Muswada huu lakini linazungumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unaweka usiri wa matokeo ya UKIMWI, lakini Kifungu cha 16(c) na (d) vinatoa usiri katika kutoa majibu ya vipimo kwa watu wengine lakini utoaji wa dawa hauzingatii usiri huu na hivyo basi, wasitengewe siku maalum za kuchukua dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matibabu yanatolewa kulingana na mpangilio wa huduma, kwa mfano magonjwa ya macho kwenye kliniki ya macho, meno kwenye kliniki ya meno, kifua kikuu kwenye kliniki ya kifua kikuu na kadhalika. Dawa za kupunguza makali ya UKIMWI hutolewa kwenye dirisha pamoja na dawa zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nyaulawa, alisema kwamba Kifungu cha 18 katika Muswada cha utoaji wa takwimu kitakuwa kinaondoa usiri. Utoaji wa takwimu hautaji jina la mhusika, kwa hiyo, hakuna usiri unaovunjwa hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 21(2), anasema pia kinavunja usiri, hapa tunasema kwamba anayetoa taarifa hiyo ni mhusika mwenyewe, kwa hiyo hakuna ukiukwaji wa taratibu zetu za kiafya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 32(1), kizungumzie ubora wa *condoms,* hilo nimelizungumzia.

Mheshimiwa Mbunge pia alishauri kwamba popote tunapokwenda tujue kwamba viongozi wa kimila wana ushawishi mkubwa tuwatumie, hilo tunalichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile alisema katika Kifungu cha 36(2), muundo wa Kamati uongezwe wajumbe kutoka sekta binafsi, hiyo ipo katika jedwali, tuliliona hilo na wenzetu wa sekta binafsi wamekuwa *captured* katika muundo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jenista Mhagama, alisema kwamba elimu izungumzie mambo zaidi ya kuwafahamisha watu UKIMWI ni nini pamoja na athari zake na namna ya kujikinga na hivi ndivyo tunavyofanya. Alisema pia kwamba jamii inayotoa mafunzo kwa wagonjwa wa UKIMWI ipewe taarifa kuhusu uambukizo wa UKIMWI kwa wagonjwa.

Taarifa kwa watoa huduma wote zitatolewa kwa kuzingatia maadili ya uganga. Inapendeza na inarahisisha pale mgonjwa mwenyewe atakapowaambia ndugu zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alizungumza kwamba, mikakati ya kudhibiti UKIMWI iziangalie sababu zinazosababisha UKIMWI katika mazingira ya Kitanzania kama vile mila potofu na hii iko katika kifungu cha 4(1)(d) na nguvu zielekezwe kwa asilimia 93 ya Watanzania, hilo nimeshalizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge amesema, sababu ya vifo vya wagonjwa zitangazwe, hili nimesema kwamba ni kinyume cha maadili na nje ya maudhui. Kuhusu kutolewa elimu ya matumizi ya dawa ya *ARV*, tutazingatia ushauri huo na kwamba, vifungo kama adhabu, visitolewe kwa watu binafsi tu na Mashariki pia yahusishwe, hii ipo katika kifungu husika.

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o amesema, suala la jinsia lizingatiwe katika utoaji wa elimu, tunauzingatia ushauri huo na kwamba, wanawake wajawazito wapimwe pamoja na waume zao, nilikwisha kulizungumza. Huduma za Misaada ya Kisheria zitolewe kwa watoto yatima; hapa tunasema Mashirika mengi yasiyo ya Kiserikali yapo na yanafanya kazi nzuri ya kutoa huduma hii. Alitupigia debe kwamba, vitendea kazi ni haba kwa sababu bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni finyu na kwamba, tujaribu kuifikisha asilimia 15 kama *Abuja Generation* ilivyosema. Mimi ningependa kumshukuru na kwamba wakati wa Bajeti, awe mstari mbele kutukingia kifua.

Mheshimiwa Yono Kevela alisema, iwepo adhabu kali kwa watu wanaoeneza UKIMWI kwa makusudi;; hiyo ipo katika kifungu namba 47. *CD4 machines* zipelekwe Njombe; tunasambaza mashine hizo kwa awamu, kulingana na uwezo wa fedha, mashine ni ghali, tumeweza kupeleka kila Mkoa na sasa hivi tumefika Wilaya 30. Waathirika wa Ugonjwa wa UKIMWI wapewe chakula; Serikali haina uwezo wa kutoa chakula. Tunachoweza kufanya ni kutoa ushauri wa chakula ambacho ni bora, hususan kwa wagonjwa ambao wameathirika.

Nchi ya Malawi walijaribu kutoa chakula kwa wagonjwa wote, lakini walishindwa kwa sababu bajeti ilikuwa kubwa, vilevile tukizingatia kwamba hao wagonjwa baada ya kuanza kutumia dawa na baada ya muda si mrefu wanaanza kujisikia hawajambo. Kwa hiyo, nia yetu ni kuwafundisha stadi waweze kujitegemea hapo watakapoanza kupona, wasiwe tegemezi kwa Serikali kupata chakula kila wakati. Alishauri kwamba, hoteli zitoe ruzuku ya chakula kwa mgonjwa wa UKIMWI akienda pale, ninadhani ajitambulishe halafu apewe ruzuku; hili limekuwa kidogo nje ya uwezo wa maudhui.

Mheshimiwa Peter Serukamba alisema kila mgonjwa aendaye hospitali apimwe, hilo limekwisha kulizungumza na kwamba Taasisi ya *Research Fellowship* isianzishwe bali NIMR iimarishwe nimekwisha kulitolea maelezo.

Mheshimiwa Pindi Chana, majibu yake tuliyatoa mchana. Mheshimiwa Rosemary Kirigini alisema, wagonjwa wote wa hospitalini wapimwe UKIMWI; tumekwisha kulizungumza. Wagonjwa wa UKIMWI wasitumie kadi maalum; tutauzingatia huo ushauri na fidia kwa wanaoambukizwa UKIMWI kazini ifafanuliwe. Viwango vya fidia kwa watu wanaoambukizwa UKIMWI kazini, vitaamuliwa na Mahakama kulingana na madai ya mhusika na adhabu ya maambukizi ya UKIMWI kwa makusudi ni ndogo; ninadhani hili linazungumzika. Katika rasimu ya kwanza ilikuwa inasema *life imprisonment*, lakini baada kuongea na wadau wengi ikaonekana kwamba, *experience* iliyopo ni kwamba, adhabu kali hazibadilishi mienendo. Wapo majambazi ukisema tutawaua, walijaribu Nigeria kuwapiga risasi hadharani, lakini ujambazi

ukaendelea tu. Kwa hiyo, ndiyo tuka-*balance* hapo miaka mitano hadi kumi kwa matumaini kwamba, watakuwa bado wako hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis amesema, dawa za UKIMWI zitolewe bure na zienezwe ili zikidhi haja. Mpango wa Tiba na Matunzo ya Usambazaji wa *ARV* ni bure, yaani kwa gharama ya Serikali kupitia Vituo vilivyoandaliwa kwa ajili ya wagonjwa. Mwaka 2005, tulikuwa na Vituo 98; mwisho wa mwaka 2006, tulikuwa na Vituo 200; na mwisho wa mwaka uliopita tulikuwa na Vituo 500. Kwa hiyo, tunajaribu kwenda haraka, tufikie sehemu zote wagonjwa wapate hizo dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vya tiba vya operesheni, chanjo na sindano, vitumike kwa kufuata taratibu na ndivyo inavyokuwa. Wagonjwa wapatiwe lishe na misaada ya wafadhili iwafikie, kusiwe na ubadhirifu, hili nimekwishaligusia.

Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi amesema, *NGOs* ikiwemo *AMREF* ilikuwa inatoa mafunzo ya vyeti kwa wale ambao walikuwa wanatoa huduma majumbani, yaani *Home Based Care;* kwa nini Serikali imezuia utoaji wa vyeti hivyo kwa Mashirika hayo; na kwa nini vyeti hivyo havitolewi na Serikali kwa wakati? Sisi tunasema kwamba, Wizara itatoa vyeti kwa wahitimu wote waliopata mafunzo kwa kutumia mitaala iliyoandaliwa na Wizara. Tungependa mitaala ijulikane na Wizara, siyo kila mmoja basi anainuka anatoa vyeti vyake ni vizuri tujue wanafundisha nini, kwa wakati gani na kwa muda gani na Wizara iwe ndiyo chombo pekee cha kutoa hivyo vyeti.

Mheshimiwa Felix Kijiko amesema, Serikali isitishe utoaji bure wa dawa za UKIMWI ili watu washindwe kununua dawa na kuacha ngono kwani itakuwa fundisho kwao. Serikali haina nia ya kuchukua maamuzi ya kusitisha utoaji bure wa dawa za *ARV* kwa kuwa imedhamiria kutoa huduma za tiba na matunzo kwa waathirika wote. Kusitisha utoaji wa dawa hizi ni kinyume cha maadili ya uganga.

Vilevile amesema kwamba, watu wote wanaoeneza UKIMWI kwa makusudi, wakijulikana washtakiwe ikiwa ni pamoja wakubwa Serikalini na katika Mashariki wanaowadanganya wanawake. Watu hao wapigwe picha na kutangazwa kwenye Vyombo vya Habari. Jibu ni kwamba, suala hili litashughulikiwa kwa mujibu wa kifungu cha 51 cha Muswada huu. Aidha, watakaobainika kueneza UKIMWI kwa makusudi, watashughulikiwa kwa kifungu namba 47 cha Muswada huu.

Mheshimiwa Felister Bura, ameuliza kifungu namba 47 kinawabana vipi watu wanaouza miili yao, yaani makahaba. Sheria ya Kanuni ya Adhabu *(Penal Code),* Sura Namba 16 inashughulikia watu hawa na sio kifungu cha 47 cha Muswada huu. Swali lingine ni kwamba; je, Serikali itawapima makahaba kujua walioathirika na ambao hawajaathirika?

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya kupima inatolewa kwa kila mtu. Kundi la makahaba halitambuliki Kiserikali, hakuna sheria inayowatambua, sasa kuanza kuwasaka inaweza ikawa kazi ngumu kidogo. Katika nchi ambazo wanatambulika, wanapima *regularly,* baada ya kila miezi kadhaa. Sasa sisi hatujafikia hapo mpaka Bunge

litakapopitisha kuhalalisha ukahaba na kuwaambia wapo kwenye orodha. Je, Serikali haioni kutowabana makahaba kifungu namba 47 hakitatekelezeka ipasavyo? Hili suala linashughulikiwa kwa mujibu wa Kanuni ya Adhabu Sura Namba 16.

Kifungu 29 kinazungumzia unyanyapaa, mbona Wizara inawanyanyapaa wenye UKIMWI kwa kupewa kadi tofauti za kuchukulia dawa. Jambo hili linaondoa usiri ambao Sheria inataka kuulinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa taarifa kwamba, Wizara inatoa huduma mbalimbali bila kutumia kadi za rangi maalum. Rangi ya kadi, hubadilika mara kwa mara kutoka tunakoagiza, leo wataleta kahawia, kesho wataleta bluu, lakini hakuna anayesema kwamba, wale wenye UKIMWI wapate rangi tofauti na wengine. Ametoa ushauri kwamba, matumizi ya fedha za Asasi zisizo za Kiserikali zijulikane na hivyo suala hili liongezwe kwenye kifungu.

Kifungu namba 35 kinazungumzia ufikishaji wa misaada kwa walengwa. Aidha, fedha zinazotolewa kwa Asasi hizi, hutangazwa kwenye magazeti na Mamlaka ya Serikali za Mitaa hupewa taarifa. Ameuliza vilevile kwamba, Ugonjwa wa UKIMWI ni sawa na magonjwa mengine, kwa nini majibu yawe siri; Serikali haioni usiri huo unawapa kiburi waathirika na kuambukiza watu wengine kwa makusudi? Jibu ni kwamba utaratibu wa usiri unatumika kwa magonjwa yote. Suala la usiri limesisitizwa kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hii. Amesema kwa nini baba wa mtoto habanwi na sheria ya kupima UKIMWI? Hilo nimekwisha kulizungumzia. Kwa nini wanaume wanaowapa mimba wanawake ambao wanagundulika kuwa wameambukizwa UKIMWI, hawabanwi na sheria hii? Kifungu namba 47 cha Muswada kinawabana.

Mheshimiwa Maria Hewa amesema, kifungu namba 9 kondom zitolewe kwa watu wote, si kwa wale wanaishi na Virusi peke yao; hilo nimekwisha kulizungumza. Waathirika wanaojitangaza wapangiwe bajeti; Serikali ina mpango maalum wa kuwahudumia wagonjwa hususan tiba na mafunzo na kwamba wanaoishi na virusi watangaziwe waende vituo gani au hospitali zao. Hapa tunasema wagonjwa wanapewa uhuru wanataka kwenda wapi.

Mheshimiwa Savelina Mwijage, amelalamikia misaada mingi haiwafikii walengwa; nimekwisha kulizungumza na kwamba, anaomba Wizara isaidie Kituo cha kulelea watoto yatima kilichopo Bukoba, hili tutalizungumza haliko kwenye Muswada. Jirani yake Mheshimiwa Meryce Emmanuel, anaomba wagonjwa wanaoishi na VVU wasaidiwe chakula na dawa; hilo nimelizungumza, kwa upande wa dawa zinatolewa bure na la chakula nimekwisha kulizungumza.

Vilevile amelalamika kwamba, wafanyakazi wa Serikali hawatunzi siri za watu wanaopimwa damu na wagonjwa, labda tulikuwa tunashindwa kuwabana vizuri kwa sababu hii sheria haikuwepo. Ingawa maadili pia yanakataza kutoa siri, lakini kwa nyongeza, kuwa na sheria nyingine, nina imani itasaidia kuwabana hao wanaotoa siri. Anaomba adhabu ya mtu anayesambaza UKIMWI kwa makusudi, ipunguzwe iwe miaka kumi. Nina imani hakusoma jedwali, kwa sababu sisi tunasema miaka mitano hadi kumi.

Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, amependekeza pia itolewe adhabu kali kwa wanaoeneza UKIMWI na ndivyo ilivyo. Jimboni kwake hakuna vifaa na *condoms* za kutosha hasa kwenye *guest houses*. Ameshauri *guests* za Ilembula, zifungwe mara moja kwani hazina kondom. Jibu ni kwamba, hatuna tatizo la upungufu wa kondom hivyo, Wizara inamshauri Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Mganga Mkuu wa Wilaya yake ili aagize kondom kutoka *MSD.* Aidha, nyumba za kulala wageni zipo kwenye sheria nyingine ya *Public Health,* ambayo karibu tutaileta hapa.

Mheshimiwa DR. Harrison Mwakyembe, aliomba katika tafsiri ya neno *court*, maneno *with exception to primary court* yafutwe na badala yake isomeke *with exception of primary court* na hili tutalitekeleza kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu. Amesema kifungu namba nne cha Muswada, kimsingi ni wajibu wa Serikali na vyombo vyake, kwa mujibu wa Ibara ya 9 na 14 ya Katiba; kulinda na kutoa huduma za jamii kwa watoto yatima na siyo wajibu wa Taasisi na watu binafsi; kwa sababu hiyo, anaona kifungu namba 4(c) cha Muswada kifutwe. Hivi vifungu havina mgongano na havina sababu ya kufutwa, hapa ni kutambua tu kwamba, kuna Taasisi, mbali na Serikali ambazo zinatusaidia katika hii kazi. Sasa kama tunajua wanafanya kazi hiyo ni lazima tuwatambue na pia kuweza kuwaratibu na kuangalia wanafanya nini?

Kifungu namba 25 kirekebishwe ili *counselling services* isitolewe tu kwa wanawake peke yao bali ihusishe na wanaume; nimekwisha kulisema hilo na kwamba, *scientific verification* iliyopo kifungu namba 27(1), kabla ya kutangaza tiba ya UKIMWI iwe na muda maalum ili tusiwakatishe tamaa watafiti wetu, kwa kukalia uvumbuzi wao miaka na miaka, kwa kisingizio cha *verification.* Suala hili ni muhimu kufanyika, hata hivyo, suala la muda litazingatiwa ili kuepuka ucheleweshaji.

Kifungu namba 28 maneno "*enact any law*" yaondolewe kwani hapana mtu mwenyewe madaraka hayo. Neno *person* kwa utaratibu wa Uandishi wa Sheria na yeye ni Mwanasheria, linajumuisha taarifa pamoja na mtu binafsi hivyo, hakuna sababu ya kukiondoa kile kifungu.

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo amesema, Wilaya ya Kilindi, haijafikiwa na elimu ya UKIMWI kama maeneo mengine. *TACAIDS* imetuahidi kutupa fedha kidogo mno, huo uhamasishaji umekuwa ni mgumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu kwamba, mipango ya elimu ya UKIMWI inafanywa na Halmashauri husika hivyo, tunashauri suala hili alipeleke kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kwa utekelezaji.

Vilevile amesema kwamba, pawekwe adhabu katika kifungu namba tisa kwa ajili ya kuwabana waajiri watakaokiuka kifungu hiki, hilo nimekwisha kulisema kwamba lipo kwenye jedwali la marekebisho.

Kifungu namba 35; *NGOs* zinazosajiliwa, maeneo mengine mfano, Tanga wakati kuna wengine wapo Kilindi watajuaje mgao wao? Je, hizi *briefcase NGOs*, zinabanwa

vipi na sheria hii, maana zinapewa fedha na kuishia hewani bila kuwafikia walengwa walioombewa fedha hizo? Aidha, kifungu hiki kizilazimishe *NGO*s wataje fedha walizopata na wawajulishe wafaidika wa fedha hizo na kuwa na *focal point* wa maeneo hayo. Hili limejibiwa tayari.

Mwisho amesema, akizingatia upasuaji tata wa Moi; je, Wizara haioni haja ya kuweka adhabu kali katika sheria hii ili kuhakikisha kuwa, wanakuwa makini sana kwenye maambukizi ya UKIMWI na hatua za wazi kuchukuliwa kwa atakayebainika? Tumezingatia adhabu kali na hii imetokana na wadau mbalimbali tuliokaa nao katika kipindi cha miaka mingi.

Mheshimiwa Elietta Switi amesema, kitendo cha usiri cha upimaji wa *HIV/AIDS* na utoaji majibu ni sehemu ya unyanyapaa, kwa sababu magonjwa mengine majibu hayafichwi. Majibu yatolewe kwa magonjwa mengine ila matibabu yawe chini ya kitengo maalum. Habari zote zinazohusu majibu yoyote ya ugonjwa wowote na vipimo vya wagonjwa ni siri na si *HIV* peke yake, hayatolewi kwa mtu mwingine isipokuwa muhusika.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya amesema, dawa za *ARV* hutolewa kwenye Vituo vya Afya vilivyopo Wilayani na Mikoani tu, ombi ni kwamba, huduma hii isogezwe hadi kwenye Zahanati, Kata na Vijiji vya jamii ya Watanzania. Hilo nimelizungumza, jinsi tunavyojaribu kusogeza hii huduma mpaka tufikie kila eneo ambalo tunatoa huduma ya afya. Serikali iwapatie chakula waathirika wa VVU, hilo nimelijibu. Sheria inawabana vipi wanaume wanaowabaka watoto na kuambukiza kwa makusudi; tuna sheria ya kujamiiana na huyo mwanaume mwenye tabia hiyo atabanwa na hiyo sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimegusia yote yaliyozungumzwa, lakini kabla sijaomba ruhusa ya kukaa, ninaomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge, ambao sikuwatambua wakati ninataja majina hapa. Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya na Mheshimiwa Juma Killimbah, kwa bahati mbaya majina yao yalisahaulika wakati tunaorodhesha. Vilevile jana wakati ninazishukuru Taasisi mbalimbali zilizotusaidia, nilipokuwa ninatoa hoja yangu niliisahau Taasisi muhimu ya Wabunge, yaani *TAPAC* kwamba na wao wamekuwa mstari wa mbele na tumesaidiana nao na tumefanya kazi nao kwa karibu. Tuna imani kwamba, tutafanya nao kazi kwa karibu katika utekelezaji wa sheria hii hapo mtakapoamua ipitishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisoma Mara ya Pili)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Said J. Nkumba.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mwongozo wako kutokana na maelezo ya MheshimiwaWaziri, alipokuwa anajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge; kwa kuwa Magereza yote wafungwa wote hutumikia kifungo kwa kukaa jinsia tofauti na moja ya kifungo ambacho anaadhibiwa mfungwa ni kutofanya tendo la ndoa akiwa gerezani; sasa Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hoja, amesema kwamba, Wizara itaangalia utaratibu wa kupeleka kondom magerezani nilivyomsikia; sasa ninaomba Mwongozo wako juu ya maelekezo haya kwa kumbukumbu sahihi za Bunge?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, Mwongozo wa Spika, unafuatana na mambo ya ki-*procedure* tunayosimama hapa. Sasa tutakapoingia kwenye Kamati ya Bunge Zima, kifungu kwa kifungu nitakupa nafasi, utafute kifungu kizuri uulize hayo. Mwongozo wa Spika ni kazi tu. Asante. *(Kicheko)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vya UKIMWI Nchini wa Mwaka 2007 *(The HIV and Aids (Prevention and Control) Bill, 2007*

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitazama marekebisho ambayo yamefanywa na Mheshimiwa Waziri, lakini nimeona katika sehemu ya ya pili, ukurasa wa 35, ambayo ni *interpretation,* pale katikati kuna neno limeandikwa *stigma,* sasa ukifuata ile kukiteremsha chini pale kuna sentensi ile ya pili inayosema; *person because one knows or suspect,* kwa sababu pale wametumia *singular;* ile *knows* na ile *suspect* isiwe *suspects*.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubali ni *oversight.*

**MWENYEKITI:** Ninaona ni Kiingereza na *typing error*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 4

**MHE. WILLIAM H. SHELLLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho cha 4(2) (a) ni kuboresha tu, lile neno limeandikwa pale *intergrate* ile "*r*" haihitajiki ni *Integrate*, kwa sababu Muswada huu ukipitishwa ni Sheria ya Bunge. Kwa hiyo, ni vizuri haya mambo madogo madogo haya tuyaangalie.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali.

**MWENYEKITI:** Ahaa! mbona kwa unyonge?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali.

**MWENYEKITI:** Hili ni suala pia la *typing error.*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisoma haya marekebisho, Ibara ya 6(1) ile sentensi ya pili kutoka chini, ninataka nipate uhakika kama neno lililopo pale kweli lilikuwa limedhamiriwa liwe hivyo, kwa sababu ukiisoma kidogo inaleta matatizo. Ukianzia pale "*and such plans shall be mainstreamed and implemented into the activities of such sector.*" Ninadhani hiyo *integrated into the activities* badala ya *implemented into the activities* haikunyooka vizuri hapa.

**MWENYEKITI:** Unasoma wapi; kwenye *Schedule of Amendments* au kwenye *main?*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, ninasoma kwenye Muswada wenyewe ukurasa wa 37.

**MWENYEKITI:** Ninaomba urudie.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasema, Ibara ya 6(1) hiyo sentensi ya nne au mstari huo wa nne, ukiusoma kuna neno pale ambalo kwa kiingereza halikai vizuri "*mainstreamed and implemented into the*

*activities.”* Ninadhani hapa walitaka *“mainstreamed and integrated or included in the activities of such sector.”*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti nipendekeza kwamba isomeke *“shall be mainstreamed and implemented within the activities of such sector.”*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ninaomba urudie tena.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, isomeke *“such plans shall be mainstreamed and implemented within the activities of such sector.”*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 7

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri akihimitisha hoja yake, alitamka kwamba, ninaitwa Dr. Binilith Mahanga, mimi ninaitwa Dr. Binilith Mahenge. Kwa hiyo, ninaomba kwa rekodi liwekwe sawasawa. Asante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, tupo kwenye Ibara ya 7 na kwenye Ibara ya 7 hakuna Mahenge. *(Kicheko)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 11

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii kuna neno pale lilikuwa limetumiwa, lakini nikawa na matatizo nikaenda kwenye *dictionary* nikaangalia kama labda ni la kitaalam au namna gani. Ibara ya 11(1); "*A person may on his own motion, volunteer to donate ...*" Sasa *motion* kwa mujibu wa *Oxford Advanced Dictionar*y ya mwaka 1995 ya *Oxford Press* inasema, *motion is a formal proposal to be discussed and voted on at a meeting*. *To be discussed* ni *proposal,* kwa hiyo, hajafanya *decision.* Nilikuwa ninadhani hapa tungetumia neno lingine na hili neno limetumika tena kwenye Ibara ya 15, hiyo *motion*. Kwa hiyo, ninapendekeza hapo tutumie *on his own decision or on his own willingness*, lakini siyo *motion*, *motion* ni kwamba, *decision* haijafanyika bado, *is open for discussion.*

**MWENYEKITI:** *On his own will;* sasa lipi tuandike *motion definitely* haifiti hapo.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru mtaalam wa Kiingereza ni kweli hapa haileti maana na hatukuliona. Ingeweza ikawa *decision or volition,* ninadhani ilikuwa *volition* toka huko mwanzo.

**MWENYEKITI:** Nini?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** *Volition.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri anapendekeza *volition.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga ni katika kifungu hiki hiki? *Okay!* Kwanza, tukubaliane kwamba, hiyo *volition* itakuwa badala yake. Tunaendelea Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara hii, ibara ndogo namba tano, inazungumzia *penalties* za ile *laboratory* au Ofisa ambaye atafanya makosa ya kumwekea mgonjwa kiungo au damu ambayo ina ugonjwa. Zimetolewa hukumu za yule atakayetenda kosa hilo.

Katika mchango wangu nilishauri kwamba, tuboreshe kifungu hiki kwa kuongeza sehemu ya *compensation* kwa mgonjwa atakayekuwa amefanyiwa hivyo kwamba, amewekewa damu au kiungo chenye ugonjwa sasa asihukumiwe tu yule aliyefanya tendo hilo; je na huyu aliyewekewa apate *compensation*?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika mchango wake alishauri hivyo na bahati mbaya, sikusoma tu majibu yetu. Masuala ya *compensation* yana sheria yake. Mtu anakuwa na madai kwa jambo alilotendewa na anaona hakutendewa haki, sio suala tena la hapa kuna mkondo wake ambao unakwenda kwenye Mahakama.

**MWENYEKITI:** Sawa, kwa sababu ukiangalia hapa tunatoa adhabu, sasa tena iingie na *compensation* hapa hapa vitagongana. Mheshimiwa William H. Shellukindo kifungu kipi?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Hicho hicho lakini kile cha 11(5) sehemu ndogo ya (5)(d) ni neno dogo tu

**MWENYEKITI:** *As amended* au?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Kuna neno limekosekana.

**MWENYEKITI:** *As amended?*

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO:** Haikuwa *amended*. Nimesoma haikufanyiwa *amendment* na nilikuwa nimalizie lakini akaingia Mheshimiwa Siraju Kaboyonga.

**MWENYEKITI:** Wewe hukuwa na haraka, basi haya.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Kwa hiyo, kwenye (d); *in case of a laboratory on an institution to a fine not less than of,* pale *not less than* ni ndogo tu ingeingia hapo inakaa vizuri tu.

**MWENYEKITI:** *Amendment* umeisoma pia?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Nimeisoma na nimei-*amend* hii huku. Nikiendelea hiyo sentensi kama mnataka niimalizie uhakikishe nimeisoma; *and not exceeding ten million shillings.* Ile *of* ndiyo haipo hapo.

**MWENYEKITI:** *Okay!* Ninadhani hakuna matatizo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 15

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Kwa kuwa tulikubali lile neno "*motion*" tukalibadili pale, kwa hiyo, ninamwomba Waziri ninadhani na hapa vilevile angetumia "*volition*" badala ya ile "*motion*".

**MWENYEKITI:** Sawa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 19

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilipokuwa ninachangia, nilizungumzia kwamba, watoto yatima na wagonjwa wa UKIMWI, wapewe msaada wa kisheria. Wakati Mheshimiwa Waziri akijibu, amesema kwamba, msaada wa kisheria, unaweza kutolewa na Taasisi zisizokuwa za Kiserikali zilizoko huko kwenye jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu, hakuna taasisi nyingi zisizokuwa za Kiserikali, zinazotoa msaada wa kisheria na ninajua kwamba, kuna kesi nyingi ambazo zimejitokeza; watoto kunyang'anywa haki zao na kukosa wa kuwatetea na ninaelewa kwamba kwenye Halmashauri kuna Wanasheria. Sasa kwa nini Serikali isiangalie uwezekano wa kuwasaidia hawa watoto, pamoja na wajane kuliko kuwaachia taasisi zilizokuwa za Kiserikali kufanya hiyo kazi na ambazo hazipo kila sehemu? Ninaomba nipate jibu Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o aliileta hiyo hoja.

**MWENYEKITI:** Ongeza sauti Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Ninakiri kwamba, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o aliileta hiyo hoja, lakini vilevile ningependa tuelewe kwamba, tuna utaratibu maalum wa kuangalia hawa waathirika; watoto yatima pamoja na wajane katika *set-up* tofauti na maudhui ya Muswada huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o kama hukuridhika, ungesimama mapema kwa sababu sasa ninaendelea na kazi yangu. Haya endelea.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijajibiwa itashughulikiwa na sekta nyingine, mimi ninataka nipate jibu tu nitaridhika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, rudia ulivyosema?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Nilikuwa ninasema kuna sheria na taratibu nyingine zinazoangalia masuala haya.

**MWENYEKITI:** Tumeelewana, hukusikia tena au kuna tatizo lingine?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya simama, maana yake hukuonekana.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa ninaomba nifahamu kwenye ibara ya 33, kuhusiana na haki za mgonjwa wa UKIMWI, kuweza kupata *access* wakati wa kupiga kura au kupigiwa kura. Sijui kama itakuwa inahusika hapa au kuna sheria nyingine ambayo itaweza kubeba suala hilo?

**MWENYEKITI:** Hebu rudia tena.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ninasema kwamba, kwenye ibara ya 33 nilikuwa naangalia pia haki ya mwathirika hasa yule ambaye ameshakuwa mgonjwa, kuweza kupata *access* ya kupiga kura au kupigiwa kura. Ninashindwa kuelewa kama inaweza ikawa hapa au kuna sheria nyingine ambayo itaweza kusaidia suala hilo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo mgonjwa kama ni Mtanzania aliyefikisha miaka 18 na hajawahi kufungwa, ana haki ya kupiga kura.

**MWENYEKITI:** Nilifikiri ni kama mgonjwa mwingine yeyote. Kama siku hiyo atakuwa na uwezo wa kupiga kura atapiga, kama ni hoi kabisa basi. Kwa sababu tukifanya hivyo tena, tunanyanyapaa watu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35
Ibara ya 36

Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39
Ibara ya 40

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 44
Ibara ya 45

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 46

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 47

**MHE. JUMA S. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ufafanuzi katika mambo mawili hapa; kwanza ninataka nirudie pale pale kwenye suala la *compensation* kwa yule atakayekuwa amembukizwa kwa makusudi. Hapa Ninataka nimwombe Mheshimiwa Waziri, afanye *cross reference* kwenye *section* 26(c). 26(c) ina-*allow compensation* kwa mfanyakazi ambaye atakuwa ameambukizwa UKIMWI *in the cause of* kufanya kazi yake.

Sasa huku kwenye 47 na pale ilipoanzia mwanzo ni mgonjwa, huyu sasa ni mtu mwingine tu ameambukizwa UKIMWI kwa makusudi na mtu mwingine. Tunamhukumu aliyeambukiza hatutaji *compensation* kwa aliyeambukizwa, tunasema sheria nyingine

itafanya kazi; kwa nini kule kwa wafanyakazi wa hospitali tumeiweka *compensation* kwenye sheria hii ndio ufafanuzi ninaohitaji?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Andrew Chenge anisaidie. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Ninaelewa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu hayupo hapa; kwenye kifungu cha 26 ambacho Mheshimwa Siraju Kaboyonga amekipeleka, ambacho kinatoa *compensation* ambayo inatokana *for any loss or pecuniary loss, directly resulting from affection on HIV.*

Sasa yeye anasema kama *concept* ile tumeiingiza kwenye sheria kupitia ibara hii ya 26; kwa nini dhana hiyo hiyo tusiingize katika kifungu cha 47; nilivyomwelewa mimi mwenyewe?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mimi ninadhani ushauri wangu kwa sababu 47 inalenga kwenye adhabu; dhana hii ya fidia kama tunataka tuikubali, hatuwezi kuiweka kwenye eneo la adhabu kwa sababu kule kunalenga atakayefanya hivyo, adhabu yake iwe ni nini, lakini kwa mwathirika, Sheria ya *Court* misingi yake inabaki pale pale, kwa sababu kuna hata kama haikuandikwa kwenye sheria hii, huna haki kabisa ya kwenda kuwasilisha madai yako kuhusu huyu ambaye unaamini amekuletea madhara au athari hizo. Yawezekana ama tungelipata kifungu kingine chenye dhana hii ambayo Mheshimiwa Siraju Kaboyonga ameileta, ambayo iko katika 47.

Unaweza ukakubali *for the purpose* ya kuisema kwamba, si vibaya kurudia rudia jambo, lakini haimnyimi, ninarudia tena, haimnyimi mwathirika haki yake ya kwenda Mahakamani na kudai fidia. Ningeishauri 47 ibaki kama adhabu, lakini itakapoonekana kuna kifungu kingine mbele ambacho hakijafika, basi dhana hiyo tuone kama inaweza ikaingia katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, hata ukisoma kifungu cha 47 ni kwamba; *"Any person who willfully and intentionally transmits HIV to another person commits an offence."* Kwa hiyo, anapewa, lakini huyu katika kufanya kazi zake, amemwekea mtu damu au kitu ambacho kina *infection* halafu inampata ni kama kesi hii waliyopasua watu ovyo. Ndugu zake wana haki ya kudai, kwa hiyo na hili nalo linakuwa kama watu ambao ni *careless* wana haki ya kudai. Ninadhani ni vitu viwili tofauti.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 48

Ibara ya 49

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 50

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, akubali kuongeza katika kifungu hicho cha 50, msitari wa nne pale mwisho kwenye ile faini au *imprisonment for a term not less* …, kuna ile *"of"* hapo inakosekana, ingeingia hapo ikanyoosha vizuri tu.

**MWENYEKITI:** Mmeipata hiyo? Sawa

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 51

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 52

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa vilevile kuna sahihisho dogo tu. Katika kifungu cha 52 kuanzia (a) mpaka (l), ile (l) ambayo kwa masahihisho ya Waziri sasa ni (m), kuna sentensi tatu pale. Ile sentensi ya tatu inasema *AIDS, orphan;* ukisoma kinakosekana kitu kimoja pale. Kwa mfano, ninadhani *orphan and their families should be orphans and their families*.

**MWENYEKITI:** Sawa sawa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 53
Ibara ya 54

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa William H. Shellukindo, amesoma kabisa hii sheria mpaka itakoma.

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vya UKIMWI Nchini wa Mwaka 2007 *(The HIV and AIDS (Prevention and Control) Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The HIV AIDS* **(***Prevention and Control) Act* ya Mwaka 2007, pamoja na mabadiliko yake, kifungu kwa kifungu na kuukubali. Hivyo basi, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada huo sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**Muswada wa Sheria ya Utalii wa mwaka 2007**
***(The Tourism Bill, 2007)***

*(Kusoma Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu tulitaka uingie Jumatatu, lakini walioomba ni wengi sana, kwa hiyo, afadhali tuanze leo halafu tutaendelea siku ya Jumatatu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda niungane na Wabunge wenzangu, kutoa pongezi nyingi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika au *African Union.* Hii ni heshima kubwa kwa nchi yetu, ambayo inatokana na utamaduni wetu uliotukuka wa demokrasia na hali ya amani na utulivu, iliyodumu tangu tupate uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeendelea kuwa nchi ya mfano katika Bara letu la Afrika hivyo basi, hatuna budi kujivunia heshima hii kubwa tuliyoipata na kuhakikisha kuwa demokrasia, amani na utulivu, vinadumu daima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dr. Getrude Pangalille Rwakatare, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum. Ninaomba kwa niaba ya watu wote wa Mwanga, kutoa salamu za rambirambi kwa

familia, kwako Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge wote, ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu Benedict Kiroya Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto, Mkoa wa Manyara. Aidha, ninachukua fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mbunge wa Mkuranga, kwa kufiwa na mke wake, ninamwomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. *(Amina)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii ni kati ya sekta zinazokua kwa kasi kubwa duniani na hivyo kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa ulimwengu. Takwimu za awali za Shirika la Utalii duniani, zinaonyesha kuwa, idadi ya watalii iliongezeka kutoka watalii 844 milioni mwaka 2006 hadi kufikia watalii 898 milioni mwaka 2007, ikiwa ni ongezeko la asilimia sita. Aidha, taarifa zinaonyesha kuwa, katika mwaka 2007 utalii wa Afrika ulikua kwa asilimia nane, ule wa Asia na Pacific, ulikua kwa asilimia 10 na ule wa Mashariki ya Kati kwa asilimia 13. Ukuaji huu mkubwa katika Mabara mengine ni changamoto kubwa kwa Bara la Afrika, ikizingatiwa kuwa Afrika ina urithi mkubwa wa vivutio vingi vya asili na vya kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini mchango wa sekta ya utalii katika Pato la Taifa umefikia asilimia 17.2 mwaka 2006, ikilinganishwa na asilimia 13 mwaka 2000. Katika kipindi hicho, idadi ya watalii iliongezeka kutoka 501,670 mwaka 2000 ikilinganishwa na watalii 644,120 mwaka 2006. Katika mwaka 2006, watalii hao waliliingizia Taifa dola za Kimarekani 862 milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu kwa sasa ni kupata watalii milioni moja ifikapo mwaka 2010. Lengo hili, litatuwezesha kupata jumla ya dola za Kimarekani takriban bilioni moja na nusu ifikapo mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii nchini, bado ina fursa kubwa ya kukua na kuchangia zaidi katika Pato la Taifa na kuondoa umaskini wa kipato kwa Watanzania walio wengi. Hadi sasa, aina ya utalii ulioendelezwa kwa kiasi kikubwa ni ule wa kutembelea mbuga za wanyamapori. Kati ya maeneo yenye sifa za kipekee duniani ambayo Tanzania inajivunia ni pamoja na Hifadhi ya Serengeti, Pori la Akiba la Selous na Hifadhi ya Ngorongoro. Sanjari na vivutio hivyo, Mlima Kilimanjaro na Mji Mkongwe wa Zanzibar, hupokea idadi kubwa sana ya watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bara la Afrika, Tanzania ni nchi ya pili kuwa na maeneo mengi yaliyoingizwa kwenye orodha ya urithi wa dunia *(World Heritage Sites).* Kwa hivi sasa nchi zinazoongoza kwa kuwa na maeneo mengi, ambayo yametangazwa kuwa ni urithi wa dunia ni Ethiopia na Morocco. Kila moja ya nchi hizi, ina maeneo manane. Nchi yetu ina jumla ya maeneo saba yaliyotangazwa kuwa urithi wa dunia. Kati ya hayo, maeneo manne ambayo ni Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, Hifadhi ya Ngorongoro, Pori la Akiba la Selous na Hifadhi ya Serengeti ni maeneo yaliyotangazwa kuwa urithi wa dunia wa asili *(Natural World Heritage Sites)*. Maeneo hayo ni kati ya Hifadhi za Taifa 15 tulizonazo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine matatu yameorodheshwa katika orodha ya urithi wa dunia wa kiutamaduni au *Cultural World Heritage Sites*. Maeneo hayo ni Mji Mkongwe wa Zanzibar, Kilwa Kisiwani, Songo Mnara na michoro ya miambani ya Kondoa. Vilevile maeneo mengine nchini mwetu, yako kwenye mchakato wa kuorodheshwa kwenye orodha ya urithi wa dunia.

Maeneo hayo ni njia kati ya biashara ya utumwa na vipusa, *the central slave and ivory traded route;* Olduvai, Milima ya Tao la Mashariki au *Eastern Arc Mountain Forest of Tanzania*, Oldonyo Mulraki, Hifadhi ya Gombe iliyoko Kigoma na Hifadhi ya Jozani, Chwaka iliyoko Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudi kubwa za kutangaza vivutio vyetu, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mlima wa Kilimanjaro na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, vimewekwa kwenye orodha ya vivutio vya utalii 50 vilivyo bora zaidi duniani kwa mwaka 2008 *(The Best 50 World Destinations for the year 2008)*. Matarajio yetu ni kuwa maeneo mengine katika nchi yetu ni kwamba, yataingia kwenye orodha hiyo na tutakapofika hapo, tutakuwa nchi iliyokuwa na vivutio vingi labda kupita zote katika Bara la Afrika. Pamoja na vivutio hivyo maarufu, bado yapo maeneo ambayo yakiendelezwa yanaweza kuchangia zaidi katika Pato la Taifa. Maeneo hayo ni pamoja na Ukanda wa Pwani wenye fukwe safi, ambao una urefu wa km 804. Aidha yapo maeneo ya kihistoria, mathalani Kilwa Masoko, Kilwa Kisiwani, Mafia, Bagamoyo, Kigoma, Rukwa, Lindi, Mtwara na Pangani, ambayo yakiendelezwa kikamilifu, yataweza kukuza utalii wetu kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakamilisha mpango maalum wa kuendeleza utalii, ikiwa ni pamoja na kuziendeleza sehemu hizo ili kuongeza uwezo wake wa kupokea na kuhudumia watalii vizuri. Nchi yetu inajivunia mambo matatu makubwa, ambayo ni mhimili wa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mambo hayo ni ukarimu wa Watanzania, utamaduni wa demokrasia, amani na utulivu. Mhimili wa utamaduni huu ni muhimu sana katika kujenga na kuendeleza utalii. Hivyo, ninaliomba Bunge lako Tukufu, kuendelea kuhakikisha kuwa, utamaduni huu hususan amani na utulivu wa nchi yetu, vinadumishwa kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada; kutokana na ubora wa vivutio vyetu na matarajio ya kukua haraka kwa utalii wetu ni muhimu kutunga sheria itakayosimamia utalii nchini katika mwanzo wa Karne ya 21. Lengo letu ni kuongeza mchango wa sekta hii katika uchumi wa taifa, kuongeza ushiriki wa Watanzania katika sekta hii, pamoja na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa watalii katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unaowasilishwa unakusudia kutungwa kwa Sheria ya Kusimamia Sekta ya Utalii nchini. Sera ya Utalii, inasisitiza uendelezaji utalii endelevu, jambo ambalo litatekelezwa kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira, kulinda mila na desturi zetu, pamoja na kudumisha mahusiano mema baina ya watalii na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kwa upande wa Tanzania Bara, masuala ya utalii ikiwa ni pamoja na hoteli na wakala wa utalii, yanashughulikiwa na sheria mbili tofauti. Sheria hizi ni Sheria za Mahoteli sura ya 105 na Sheria ya Wakala wa Utalii au Utoaji wa Leseni, Sura ya 65, zote zikiwa zimetungwa katika miaka ya 1960. Mabadiliko mengi yametokea katika nyanja ya utalii, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa sekta hii na utalii wenyewe hivyo, kusababisha Sheria zilizopo kutokidhi hali na mahitaji ya sasa.

Mhesimiwa Naibu Spika, Muswada huu, pamoja na mambo mengine, umezingatia mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Sera ya Taifa ya Utalii, kwa kuainisha wajibu na majukumu ya watendaji.

(b) Kuanzisha Kamati ya Ushauri ya Wataalam ikiwa ni pamoja na kubainisha wajumbe wa Kamati hiyo na kazi zake.

(c) Kuainisha shughuli za kitalii na uwekaji wa madaraja ya hoteli.

(d) Muswada umeweka taratibu za usajili na utoaji wa leseni za utalii, pamoja na kufuata usajili na haki ya kukata rufaa.

(e) Muswada unapendekeza kusimamia utoaji wa fidia kwa mali za watalii au wageni endapo kuna upotevu wa mali za watalii au wageni wanapokaa katika eneo la utalii.

(f) Muswada umeweka wazi wajibu wa kuweka na kutoa taarifa na takwimu za shughuli za kitalii na wageni wanaohudumiwa na kila sehemu ya utalii. Hatua hii imechukuliwa hasa kwa kuzingatia suala tete la usalama wa utalii na raia wa Tanzania, pamoja na kuhakikisha kwamba, wanaoendesha shughuli za kitalii, wanalipa kodi ya Serikali.

(g) Uchangiaji wa huduma za kijamii katika maeneo yanayozunguka vivutio vya utalii.

(h) Unaainisha makosa na adhabu mbalimbali zitakazotolewa chini ya Sheria itakapopitishwa na Bunge.

(i) Umeainisha baadhi ya shughuli za kitalii zitakazofanywa au kuendeshwa na Watanzania peke yao.

(j) Unaweka masharti kwa ajili ya maafisa na watu mbalimbali wanaosimamia au kushiriki katika shughuli za utalii, ukizingatia kanuni za maadili ya utalii duniani au *The Global Code of Ethics of Tourism*.

(k) Unaainisha na kuweka masharti ya waongoza watalii au *tour guards*, pamoja na hayo, Waziri pia amepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni kwa ajili ya kuweka utaratibu wa usimamizi wa shughuli za *tour guards.*

(l) Umeainisha kwa kifupi, masharti na utaratibu wa upigaji picha na kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya utalii, kutengeneza kanuni zitakazosimamia masharti na utaratibu wote utakaohusu uendeshaji wa shughuli hiyo hapa nchini.

(m) Umeweka masharti na taratibu mbalimbali zitakazofuatwa katika kutambua, kusajili na kutoa leseni kwa shughuli zote za utalii zitakazoendeshwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mambo muhimu yaliyojumuishwa kwenye Muswada huu; Muswada umegawanyika katika sehemu tisa:-

Sehemu ya kwanza, inahusu masuala ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria na kuanza kutumika kwa sheria hii. Pia inatoa tafsiri kwa baadhi ya misamiati na maneno muhimu yaliyotumika kwenye Muswada unaopendekezwa. Sehemu hii pia inasisitiza, uzingatiaji wa Sera ya Taifa ya Utalii na Kanuni za Maadili Duniani, kwa watu mbalimbali wanaotekeleza majukumu chini ya sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya pili, inaweka masharti yanayohusu uanzishwaji wa Kamati ya Ushauri ya Wataalam, kazi zake na wajumbe wake. Pia inatoa masharti ya Mkurugenzi wa Utalii, kazi za Idara ya Maofisa wa Utalii. Sehemu hii pia inaweka taratibu nyingine zinazohusu utawala.

Sehemu ya tatu, inahusu masuala yanayohusu uteuzi *(designated of tourism facilities and activities)*, uwekaji wa madaraja ya hoteli na shughuli za kitalii.

Sehemu ya nne, inahusu uanzishwaji wa Bodi ya Leseni, masuala yanayohusu kazi za Bodi ya Leseni na uanzishwaji wa Mamlaka ya Rufaa, yameanishwa katika sehemu hii.

Sehemu ya tano, inahusu utoaji leseni za utalii. Sehemu hii inaweka mchakato wa utaratibu wa uombaji, utoaji na ufuatiliaji wa leseni za utalii. Pia inaweka masharti yanayohusu haki na wajibu wa wamiliki wa shughuli za utalii na za watalii.

Sehemu ya Sita, inahusu watu wanaoendesha shughuli za utalii au *tourism facilities operators.* Sehemu hii inaweka utaratibu wa utoaji wa leseni za haki na wajibu wao chini ya sheria inayopendekezwa, pamoja na utangazaji wa orodha yao kama ilivyoainishwa kwenye sehemu hii.

Sehemu ya saba, inahusu waongoza watalii au *tour guards*. Sehemu hii inaainisha masharti na sifa za waongoza watalii. Vilevile inaainisha usajili wa waongoza watalii au *tour guards* na kuonyesha kazi zao na mambo gani yatakayokuwemo kwenye daftari la usajili wa waongoza watalii.

Sehemu ya nane, inaainisha makosa na adhabu mbalimbali ambazo zinaweza kutolewa chini ya Sheria hii, pindi ukiukwaji wa sheria inayopendekezwa utakapotokea.

Sehemu ya Tisa, inahusu masuala ya jumla yanayohusu utayarishaji wa Kanuni, mafunzo, utoaji wa takwimu na habari, pamoja na kuweka utaratibu wa kuwapa kipaumbele, Wananchi wa Tanzania katika baadhi ya utalii na kuona namna gani wanaweza kufaidika na vivutio vya utalii vilivyoko nchini. Sehemu hii pia inafuta Sheria ya Hoteli, Sura ya 105 na Sheria ya Mawakala wa Utalii au Utoaji Leseni, Sura ya 65.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nikushukuru sana na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua Kanuni mpya bado hatujapewa, lakini kimsingi zimeanza kutumika, ndiyo sababu tumeona hata baadhi ya mavazi ambayo yalikuwa yanakataliwa chini ya Kanuni za Toleo la Mwaka 2004, sasa yanatumika.

Kinachonishangaza ambacho ninaomba Mwongozo wako; kwenye Kanuni hizi mpya, tulipokuwa tunapitisha kuna kifungu ambacho ninakumbuka tulikisoma na hakikupingwa; ilikubalika kwamba, salamu za pongezi au rambirambi zikishatolewa na Spika au Naibu Spika, basi ziwe zinatolewa kwa niaba ya Bunge zima, lakini bado ninaona zinaendelea kutolewa. Kwa hiyo, ninaomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, upo sahihi kabisa kwamba, kama kuna pongezi ama kuna salamu za rambirambi, zitatolewa aidha na Spika au Kiongozi wa Serikali Bungeni au Kambi ya Upinzani; baada ya hapo, wengine tunaendelea kusudi tutumie muda wetu kwa mambo yale ambayo ni ya maendeleo. Kifungu chenyewe nitakwambia kesho, ninakijua kwa sababu nimeshiriki sana. Zaidi zaidi kwa maswali asubuhi, Waziri anatakiwa kujibu swali na sisi wenzenu katika dakika kumi na tano wakati wa Bunge la kawaida maana yake kila swali ni dakika tano tu. Sasa wewe ukitumia kwa pongezi na rambirambi kwenye swali, kwa kweli umeshavuruga ratiba ya kiti.

Hivyo hivyo, Mheshimiwa Mbunge anapouliza swali anasema kabla ya kuuliza swali, nina habari sijui kuhusu kitu fulani; anatakiwa kusema Mheshimiwa Spika, ninaomba swali langu fulani lijibiwe, isipokuwa labda kama kuna *amendment* tu basi. Kwa hiyo, tunaomba *strictly* hiyo ifuatwe, kwa sababu inavuruga mwenendo mzima wa kuuliza maswali. Asante kwa ku-*pay attention*. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *spirit* hiyo hiyo, kwa sababu muda wa Bunge hili ni adimu sana, baada ya kipindi cha maswali, ninadhani Bunge hili kupitia kwako, tupate Mwongozo kwa sababu tunatumia muda mwingi sana ambao tungeutumia vizuri kwa shughuli za nyumba hii kwa uchache.

**NAIBU SPIKA:** *Comment* yako *noted*, lakini ninadhani katika Kanuni pia imetoa utaratibu wa aina hiyo, tutatoa maelezo siku ya Jumatatu. Sasa ninamwita Msemaji wa Kamati, Mheshimiwa Halima M. Mamuya, kwa niaba ya Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA M. MAMUYA (K.N.Y. MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, kuhusu Muswada wa Sheria ya Utalii wa Mwaka 2008 *(The Tourism Act, 2007).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata fursa hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, kuhusu Muswada wa Sheria ya Utalii wa mwaka 2007 *(The Tourism Act, 2007)*, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(5), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kwa Mkutano huu wa Kumi wa Bunge, Kamati yangu ilipewa kazi ya kuupitia na kuujadili, Muswada wa Sheria ya Utalii wa Mwaka 2007, ambao unafuta Sheria ya Hoteli, Sura ya 105 na Sheria ya Mawakala wa Hoteli (Leseni) Sura ya 65 kwa dhamira ya kuweka utaratibu mzuri zaidi katika kusimamia na kukuza biashara ya Utalii Tanzania Bara. Ninapenda kuchukua fursa hii, kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati yangu ilitekeleza kazi hiyo kikamilifu, kwa kushirikiana na Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na Watendaji wa Wizara yake na Wanasheria toka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau husika wa Muswada wa Sheria ya Utalii, 2007 na kupata maoni na mapendekezo yao. Maoni ya Wadau hao yaliwasilishwa mbele ya Kamati tarehe 15 Januari, 2008 katika kikao kilichofanyika katika Ukumbi wa *Courtyard* katika Hoteli ya Protea, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawapongeza na kuwashukuru kwa dhati, wadau wote muhimu, kwa ushiriki wao katika kuandaa Muswada huu, ambao walitoka Sekta na Taasisi mbalimbali za Kiserikali na zisizo za Kiserikali kama vile *Hotel Association of Tanzania (HAT),* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(UDSM*), Chuo cha Kilimo cha Sokoine *(SUA),* Chuo cha Utalii Tanzania *(NCT),* Jumuiko la Maliasili Tanzania *(TNRF), Tanzania Operators Association (TATO), Tanzania Hunting Operators Association (TAHOA),Tanzania Professional Hunters Association (TPHA), Tanzania Society of Travel Agents (TASOTA), Intra-Africa and Tourism Association (ITTA), Tanzania Tour Guide Association (TTGA), Tanzania Air Operators Association (TAOA), Zanzibar Tourism Investors Association (ZATI)* na Washirika wa Sekta ya Utalii, pamoja na wengineo wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati kwa kutambua umuhimu wa kushirikisha Wizara katika maandalizi ya Muswada huu, chini ya Wizara husika ya Maliasili na Utalii, tumeshirikiana kikamilifu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika kufikia muafaka, ambao tunauleta mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao utawezesha kuwepo kwa sheria mahususi itakayokidhi mahitaji yaliyopo katika kukuza Sekta ya Utalii Tanzania. Aidha, Sheria hii inakusudia kuimarisha, kuboresha usimamizi wa Utalii na kukuza biashara ya Utalii ndani na nje ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kutungwa kwa sheria hii, ambayo imeenda sambamba na kasi iliyopo sasa ya utangazaji wa utalii nje ya nchi. Vilevile imezingatia kwa kiasi fulani, Sera ya Taifa ya Utalii, Usimamizi wa Wanyamapori na miongozo mbalimbali inayohusu Utalii na Wanyamapori. Sheria hii italeta ufanisi katika ukuzaji wa sekta hii, hasa kwa kuzingatia ushindani wa kibiashara na nchi jirani pia kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Muswada huu ni mazuri kwa manufaa na maslahi ya maendeleo ya Taifa letu na kukuza uchumi wa Nchi yetu. Kamati inashauri Serikali kuwa na mtiririko mzuri wa Sera na Sheria nzuri hasa za Utalii na Wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kutungwa kwa Sheria hii ya Utalii. Sheria zilizopo ambazo zinagusa maeneo ya utalii, hazitoshelezi hasa katika kuhakikisha Serikali inapata mapato sahihi kutokana na shughuli hii ya utalii. Kutungwa kwa Sheria hii, kutasaidia kujua idadi kamili ya watalii waingiao nchini kwa mwaka na itasaidia kujua pato kamili linalotokana na shughuli za utalii nchini kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni kitovu cha utalii Duniani; imejaliwa kila aina ya vivutio vya utalii, lakini mapato ya Serikali kutoka kwenye sekta hii, hayalingani na utalii uliopo. Shughuli nyingi zinafanywa pasipo kuzingatia taratibu za leseni au kutokuwa na leseni kabisa. Kwa kuwa sheria hii inaweka mchakato wa utaratibu wa uombaji, utoaji na ufutaji wa leseni ya utalii, Kamati inaishauri Serikali kuwabana ipasavyo wale wote wanaokiuka masharti ya shughuli za utalii nchini.

Kwa kuwa Tanzania ina vivutio vingi vya utalii sehemu za vijijini, ikiwa ni pamoja na utamaduni na mazingira, Kamati inashauri Serikali kutangaza utalii wa vijijini *(Rural Tourism Development),* kupitia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Wakiwezeshwa wanaweza kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko vijijini kwa urahisi zaidi. Pamoja na kwamba, Sheria hii inakusudia kusimamia, kukuza na kuboresha utalii nchini, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia suala la utunzaji wa mazingira hasa katika ujenzi wa hoteli za kitalii zitakazojengwa na zinazojengwa katika maeneo yenye vivutio vya utalii.

Kwa kutambua nafasi muhimu waliyonayo wadau katika kuchangia kukua, kutangaza na kuimarisha shughuli za utalii ndani na nje ya nchi, Kamati inaishauri Serikali iweke utaratibu maalum, utakaowawezesha wadau wengi zaidi kushiriki wakati wa kutengeneza Kanuni za Sheria hii. Ushirikishwaji wa wataalam, washauri waelekezi na wadau wengine, utaleta ufanisi katika Sekta ya Utalii. Muswada huu umeainisha vyema masuala ya makosa na adhabu mbalimbali ambazo zinaweza kutolewa chini ya Sheria hii. Kamati inasisitiza na kutoa wito kuwa, hatua kali zichukuliwe kwa wale ambao watakiuka sheria na taratibu zitakazowekwa. Kamati inasisitiza na kutoa wito kwa vyombo husika, wasimamie sheria ipasavyo na kuwachukulia hatua kali, wanaohusika kukiuka sheria na taratibu zinazohusu utalii. Kamati inaishauri Serikali, kuongeza adhabu zilizopo chini ya sheria hii ili kupunguza mianya ya uvunjaji wa sheria hii kwa makusudi.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa mstari wa mbele katika kutangaza, kusimamia na kukuza biashara ya utalii ndani na nje ya nchi. Kamati inatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote kwa ujumla, kuwa na mwamko wa kutangaza utalii wetu na kutembelea maeneo mbalimbali yenye vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zabein Mhita, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Katibu Mkuu, Wataalam na Watendaji wote wa Wizara hii, walioshirikiana na Kamati katika kuandaa na kutoa maelezo ya kina pale yalipohitajika. Ninapenda kutoa shukrani za pekee kwa Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kutoa ufafanuzi wa vipengele mbalimbali vya Sheria hii kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawashukuru wadau wote niliokwisha wataja hapo awali, kwa ushiriki wao katika *public hearing* na kutoa maoni yao, ambayo kwa kiasi kikubwa, yamesaidia katika kukamilisha na kuuboresha Muswada huu. Kwa ushirikiano na kazi nzuri ya wadau hao, Muswada umeandaliwa na kuwasilishwa kwa ufasaha na kufanya kazi ya Kamati kuwa rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, ambao walishiriki kikamilifu katika kuujadili kwa ufasaha na kuuboresha Muswada huu. Ninaomba niwatambue kwa

majina Wajumbe hao kama ifuatavyo: Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Emanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, Mheshimiwa Aziza S. Ally na Mheshimiwa Ali Khamis Seif. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Salim Khamis Salim, Mheshimiwa Abdukarim E. Shah, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. L. Foka, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, ninapenda kuwashukuru Ndugu Michael Kadebe na Ndugu Elieka Saanya; Makatibu wa Kamati hii; kwa kuweza kuihudumia vyema Kamati na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono kwa dhati, kuwasilishwa kwa Muswada huu na kujadiliwa Bungeni. Kwa niaba ya Kamati ya Maliasili na Mazingira, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, NInaomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya na kuniwezesha kumaliza na kuingia salama katika mwaka mpya wa 2008. Pia natoa salaam za heri ya mwaka mpya, kwa Waheshimiwa Wabunge wote, pamoja na Wananchi wa Mkoa wa Tabora, hususan Wananchi wote wa Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani zangu kwako binafsim kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzanim kuhusu Muswada wa Sheria ya Utalii wa mwaka *2008 (The Tourism Bill, 2008)*, kwa mujibu wa Kanuni ya 52(6)(c) na 85(6), Toleo la 2007 la Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Naibu wake, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, pamoja na watendaji wake wote, kwa kuandaa na kuuleta hapa Bungeni Muswada huu, wenye lengo la kuboresha Sekta ya Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii hapa nchini, imekuwa kwa kipindi kirefu ikinufaisha baadhi ya makundi fulani ya jamii na kuacha jamii kubwa ya Watanzania ikiwa hainufaiki na utalii kwa ujumla wake. Kambi ya Upinzani inaona kwamba, kama sheria hii itasimamiwa vizuri, basi Sekta ya Utalii itaongeza Pato kubwa la Taifa na hivyom itakuwa na manufaa makubwa kwa nchi na wananchi wake, kwani utalii ni biashara pekee ambayo Watanzania tunaweza kupanga bei sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii ni moja kati ya mambo ambayo yanapewa mstari wa mbele katika kuondoa umaskini kwa wananchi. Sekta hii kuhodhiwa na makundi fulani katika jamii ni makosa makubwa na inasababisha utalii usionekane kama ndio kiashiria kikubwa cha kupunguza/kuondoa umaskini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umejikita sana katika utalii wa nchi kavu na kusahau utalii wa pwani. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri, aliangalie suala hili la utalii wa pwani. Hii inatokana na ukweli kuwa, wanamiliki mahoteli makubwa, wamehodhi huduma zinazoweza kutolewa na wananchi, kama vile matumizi ya boti ndogo ndogo kwa shughuli za baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu, Serikali Kuu imekuwa ndio muhusika mkuu katika suala zima la kuendeleza utalii na hivyo, Serikali za Mitaa kutokushirikishwa kikamilifu katika suala zima la kukuza na kuendeleza utalii. Muswada huu pia haujamfikiria mwananchi ambaye anajihusisha na utalii wa kiutamaduni *(Cultural Tourism or Community Based Tourism).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina makabila yasiyopungua 120 na kila kabila lina mila na tamaduni zake, kwa maana nyingine mila na tamaduni hizo ni sehemu ya utalii katika jamii hizo, mfano mzuri ni mila katika jamii za Wamasai, Wahadzabe, Wamang'ati na kadhalika. Bidhaa zozote za kiasili katika makabila yetu, zinaweza kuwa za kibiashara na walengwa wakuu ni wale walio nje ya jamii hizo.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya pili ya Muswada, Kifungu cha 4(3) kinachoongelea muundo wa Kamati ya Kishauri ya Ufundi, kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la kwanza, karibu wajumbe wote ni watendaji katika mamlaka au asasi nyengine. Kambi ya Upinzani, inaliona hili kuwa linaweza kuwa ni kikwazo katika utendaji kazi wa jumla kwa wajumbe hao, kutokana na majukumu waliyonayo katika asasi/taasisi zao au inawezekana kabisa kila mjumbe katika kamati hiyo, kutoa ushauri ambao unaweza kulenga kunufaisha upande wa asasi anayoiongoza. Kambi ya Upinzani, vilevile inapendekeza kuwa, wajumbe wa kamati ya ushauri wawe ni wale wasiokuwa na maslahi katika asasi yoyote ile, lakini wawe ni watu wenye sifa na uwezo wa kumudu majukumu yalivyo ainishwa kwenye Muswada wa Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya (iv) ya Muswada, ukurasa wa 13 inayohusu uundwaji wa Bodi ya Leseni, kifungu cha 18(2)(a) kuhusu Mheshimiwa Waziri kuwa ndiye mwenye mamlaka ya uteuzi wa Mwenyekiti. Kambi ya Upinzani, inaona ni bora sifa za Mwenyekiti zikawekwa wazi, kwani kumekuwepo na mazoea ya Wenyeviti wa Bodi mbalimbali, kuteuliwa wanasiasa wasiokuwa na uelewa wa kutosha katika fani

husika, jambo linalosababisha kuwepo kwa utendaji mbovu katika sekta husika. Pia tunapendekeza sifa za wajumbe 11 wa Bodi hiyo, ziainishwe wazi ili kupata watu wenye sifa watakaokidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri, atoe ufafanuzi wa kimajukumu kati ya Kamati ya Ushauri wa Kiufundi kama inavyoonyeshwa katika kifungu cha 4(2)(a)(i) na Bodi ya Leseni iliyo katika kifungu cha 19(1)(c) cha Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika Muswada, haionyeshi kuwa ardhi ambayo imetengwa kwa ajili ya kuweka miundombinu ya utalii kama vile barabara na mahoteli. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuzingatia utunzaji wa mazingira na kuhifadhi uhalisia wa hifadhi zetu na vivutio vilivyopo, wawekezaji washauriwe kujenga mahoteli ya kitalii nje ya hifadhi, badala ya kushinikiza kujenga ndani wanavyotaka wao, jambo linaloleta msongamano katika eneo moja na kuharibu mandhari ya mbuga zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo lingine katika Sekta ya Utalii kuhusiana na huduma zinazowekwa ndani ya vivutio vya kitalii, kutofaidisha kikamilifu, hifadhi husika kupitia ada zinazotolewa; mfano, *camping fee*-inakuwa *$50* na *concession fee $5.* iki ni kiasi kidogo sana, kulinganisha na kiasi wanachokipata kutoka kwa mtalii mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali iangalie Muswada wa Sheria hii upya, kuhusiana na viwango vya ada, sambamba na leseni kwa wale wote wanaojishughulisha na shughuli za utalii, kwa lengo la kuweka mazingira bora kwa wananchi kunufaika na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kifungu 21(i) kinasema, mtu yeyote atakayeendesha shughuli za kitalii, awe na leseni. Kifungu 21(3), mtu yeyote atakayefanya shughuli hiyo bila ya leseni, atakuwa amefanya kosa. Kifungu 46(1) kinasema, yeyote atakayefanya makosa kwa makosa yaliyotajwa katika kifungu hicho, atahukumiwa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kufungwa jela miaka isiyozidi miwili au adhabu zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kifungu 49, kinatoa adhabu kwa mtu yeyote aliyekiuka sheria hii kwa makosa ambayo adhabu yake haikutajwa, itabidi atoe faini isiyopungua milioni mbili au kifungo cha miezi sita au vyote viwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wajasiriamali wadogo wadogo, kwa mfano, wachonga vinyago, ambao pia wamo katika shughuli za utalii; itakuwa hatukuwatendea haki wanapopatikana na kosa la kutokuwa na leseni, wakaadhibiwa chini ya vifungu 46 na 49 vya sheria hii. Kwa kutumia adhabu hizo, hatuoni kama kutakuwa na matabaka kwa watu fulani kujishughulisha na shughuli za kitalii na wengine kushindwa, kwa sababu ya uwezo wao mdogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, juu ya wajasiriamali wadogo ambao hata uwezo wa kukata leseni hawana, watakapopatikana na makosa watashughulikiwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 50, kinamlinda Mkurugenzi na Watendaji wake, wasiwajibishwe kwa matendo ambayo watakuwa wametenda katika majukumu yao ya kiutendaji. Kambi ya Upinzani, inaona hapa bila ya kuweka *standards* zinazotakiwa za kuwadhibiti Mkurugenzi na Watendaji wake, kifungu kinatoa mwanya mkubwa wa uonevu na unyanyasaji toka kwa Watendaji wa Serikali, kwa wale wanaopata matatizo katika sekta nzima ya utalii, kwa kuwa sheria hii inatoa mwanya kwa watendaji kufanya wanavyotaka. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta kabisa kifungu hiki ili kuondoa kabisa uwezekano wa kuwepo unyanyasaji wa aina yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 51, kinahusu rufaa zote zinahususiana na leseni kwenda kwa Mheshimiwa Waziri, pale ambapo mhusika hakuridhika na hatua zilizochukuliwa dhidi yake. Kambi ya Upinzani, inaona itakuwa ni busara kwa rufaa zote kupelekwa kwa Mamlaka ya Rufaa *(Appeal Authority)*, kifungu cha 20, kwani mamlaka hiyo ina watendaji ambao wamejumuisha wanasheria na wataalam kwenye Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukuza Sekta ya Utalii katika maeneo yote yenye vivutio, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuharakisha kuyapatia hadhi maeneo yote ya Hifadhi za Jamii *(Wildlife Management Areas)*, ili vivutio vilivyopo kwenye maeneo hayo, viweze kutumiwa kikamilifu kuingiza kipato kwa jamii zinazozunguka maeneo hayo na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, nizungumzie suala zima la matumizi ya fedha za kigeni katika kuendeshea shughuli za utalii hapa nchini; hiki ni kikwazo kikubwa kinachochangia fedha yetu kuporomoka mara kwa mara na hivyo, uchumi wetu kuyumba. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa, shilingi ya Kitanzania inatumika katika maeneo yote ya utalii, kwa lengo la kuipa nguvu fedha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo machache, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante. Kama nilivyoeleza, mpaka hivi sasa wachangiaji wamefika 23 na kwa utaratibu wetu, hiyo ni idadi kubwa, kwa hiyo, tutaendelea mpaka siku ya Jumatatu. Nitaanza na wale ambao hawajazungumza, kwa sasa ninamwona Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni na Mheshimiwa James Lembeli. Hawa wanatosha kwa leo.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha Muswada huu ambao umekuja katika muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu, mimi nimeguswa na mambo kadhaa. Mheshimiwa Waziri, amekiri hapa kwamba, kupitia Muswada huu, kukua kwa Sekta ya Utalii hapa nchini, mapato yameongezeka kufikia Dola milioni 898 au asilimia 17.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2006/2007 na kwamba, tayari Wizara imeshaweka *projection* ya kuongezeka kwa mapato haya kufikia bilioni 1.5 mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu, ninaona kidogo Mheshimiwa Waziri labda katika maelezo yake hakueleza sana, kwa sababu hakuweka haja kubwa ya kupanua wigo wa utalii katika nchi hii. Amezungumzia sana sana utalii wa wanyamapori na utalii wa Mlima Kilimanjaro, lakini kuna maeneo mengi ambayo hakujaribu kuyagusia, kwa mfano, utalii wa pwani na katika Ziwa Victoria ambao ni muhimu sana. Sasa ninapenda nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, katika Muswada wake huu ni vyema ajaribu kuainisha maeneo ambayo ni mbadala kwa ajili ya kutanua wigo wa utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu sasa tunazidi kukusanya fedha nyingi ili tuweze kuboresha maisha ya Watanzania na utalii ni moja kati ya sekta zinazoingiza pato kubwa sana kwa nchi hii. Katika Muswada huu, ukiangalia kuna maeneo ambayo leo hii Watanzania tungekuwa tumejivunia sana kufuatia machafuko ya Kenya, kwa sababu Kenya walikuwa wame-*plan* kuwa na watalii wengi ambao wameshindwa kuja. Tungekuwa tumejiandaa hapa nchini, ina maana tungeweza kupata *opportunity* ya kuweza ku-*host* na kuongeza mapato yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiingia katika sehemu ya pili, ile ibara ya 6(1) inazungumzia kuhusu suala la ku-*classify* na ku-*grade facilities* ambazo ziko kwenye *tourism*. Ningependa kumwomba Mheshimiwa Waziri hapa, kwa vile Muswada umesema kutakuwa na Idara ya Utalii, Idara hii ingeongozwa na watu ambao ni *Professionals* na ikawa *independent body* ili ifanye kazi ambayo haitakuwa na ile *element* ya Serikali kuinguilia kufanya maamuzi yake. Kwa hiyo, ninashauri sana katika Muswada huu, Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia haja ya kuwa na *independent body* ambayo itakuwa inafanya *grading* na *classification* ya *tourism facilities*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sura ya (4), kuna suala zima la *Appeal Authority*; hapa tunaona kuna *appeal* mbili; kuna moja kwenye *Licensing Board* na nyingine kwenye *Tourism Division*. Ninafikiri kwa sababu Muswada huu ni mmoja ni vyema angeweza ku-*harmonize*, *Appeal Board* ikawa moja badala ya kuwa na *Appeal Board* mbili ili haya masuala yote yanayohusu mambo ya *Licensing* na mambo ya *Tourism,* yafanyike kwenye *Appeal Board* moja. Vilevile ukiangalia kiutendaji na hata kiutawala bora, inarahisisha zaidi utendaji kazi na kupunguza gharama za kuwa na *Board* mbili tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi ukizungumzia utalii katika nchi hii, kuna baadhi ya maeneo yanasahaulika sana. Sielewi kwa nini Serengeti na Mlima Kilimanjaro

inakuwa *pledged* zaidi kwa utalii wa Kanda ya Kaskazini, lakini kwa Kanda ya Ziwa, Mwanza inasahaulika kila wakati? Ukiangalia Mwanza, kuna *Airport* ambayo miaka yote haijengwi, kunakuwa na ahadi ya kujengwa lakini haijengwi. Mimi ningeshauri kwamba, Ukanda wa *Western Corridor* ambao unahusisha na Mwanza *Airport* ni vyema ungeweza kuboreshwa ili watalii sasa wasizidi kwenda zaidi Kilimanjaro na Arusha au Ngorongoro, wafike na kwenye Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu ni vyema Mheshimiwa Waziri, akaweka mkakati mahususi ambao utahusisha suala zima la miundombinu. Hatuwezi kupanua utalii katika nchi hii, bila kuhusisha suala la miundombinu na hii ni moja kati ya changamoto ambazo ni muhimu sana kwa Waziri wa Utalii kuweza kuweka msukumo wa kipekee. Ninaamini kabisa kwamba, maeneo ambayo yamezungukwa na Ziwa Victoria, yana nafasi kubwa sana ya kuongeza Utalii katika mambo ya *Eco-tourism*, *fishing* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Muswada huu, haijaelezwa suala la kuwa na vyuo vya kutosha vya kufundisha wataalam katika Sekta ya Utalii. Kitu kimoja katika Tanzania leo hii ni kwamba, *hospitality industry* bado iko chini sana. Huduma kwa watu wanaotoa huduma bado ziko chini sana. Kwa vile tunaenda katika soko ambalo ushindani ni mkubwa ni vyema Wizara ingewekeza na kuweka kipaumbele katika suala la huduma. Huduma hii unaanza kui-*track* kutoka kwenye kitu kinachoitwa *Value Chain Analysis* kwamba, mtalii anaponunua tiketi yake kule nje anakuja Tanzania, analipa *Visa* kama ni Ubalozini au *upon arrival* akifika Dar es salaam mpaka anapokuwa ameenda Hotelini amelala, ametoka hotelini, amezunguka kwenye Mbuga za Wanyama au maeneo mbalimbali ya kitalii mpaka anaporudi nyumbani. Sasa Tanzania tunapata nini katika *component* hiyo?

Wenzangu ambao wanaweza wakanisaidia, watu wa Visiwa vya Unguja na Pemba, kuna mahoteli mengi sana yako kule, ambayo yanamilikiwa na wageni. Hawa watu wana kitu kinachoitwa *package tourism*, hao watalii wanalipa hela zao kule nje, wanakuja hapa na senti kidogo tu za kutumia hapa nchini. Sasa hoja inayokuja ni kwamba ni kiwango gani cha mapato ambacho tunapata sisi Watanzania, kutokana na utalii wa namna hiyo. Ninadhani hii ni kero kubwa sana na kama tunataka kuweza kuivutia na tuweze kuongeza mapato yetu, lazima tuangalie, hapa ipo shughuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi Watanzania tunakuwa *taken for the ride*, lakini nchi nyingine hata kama mtu anamiliki hoteli hapa nchini kama ni *foreigner*, lazima kuna utaratibu ambao *income* yake inakuwa *properly declared* ili tuweze kumtoza kodi na kupata mapato ya kutosha. Sasa unakuta mtu anaye-*own hotel* ni wa kutoka nje, akaunti inayolipiwa pesa hizi iko nje, watalii wanatoka nje, pato linalokuja hapa nchini ni kidogo sana. Kwa hiyo, ninaomba sana katika Muswada huu, Mheshimiwa Waziri ajaribu kuliangalia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ninapenda kuongelea ni Ibara ya (4) kuhusu suala la ku-*register tour guides*. Kwa mtazamo wa haraka haraka, nilidhani

kwamba, *tour-guides* ni *sub-set* ya *tourism operation or operators,* kwa sababu umemzungumzia *tour-guide* peke yake, lakini huyu ni sehemu ndogo tu, kuna watu wengine katika *line* hiyo ya biashara; kwa nini tuongelee *tour-guide* peke yake (mwongoza watalii), vipi kuhusu watu wanaotoa huduma nyingine? Mtalii ataongozwa kama kuna watu wanatoa huduma nyingine na ndiyo maana tunasema utalii inakuwa ni *package*.

Kwa hiyo, ningeshauri kwamba, hii *tour-guides* isingeingia kwenye Muswada hapa, ingeingia labda kwenye *regulations* badala ya kwenye Muswada, kwa sababu kama ni Muswada na baadaye ikawa sheria, kubadilisha kitu chochote lazima ije hapa Bungeni, iwe tena *amendments*, kitu ambacho ninafikiri itachukua muda mrefu na kadhalika. Kwa hiyo, ninamshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, hiki kipengele ajaribu kukiangalia kwa sababu ukizungumzia *tour-guide* ni *sub-set* ya *tour operation*. Sasa ni vyema zaidi akajaribu kuiangalia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu ninamsifu kitu kimoja hapa kwamba, baadhi ya shughuli zimekuwa ni kwa ajili ya Watanzania, hii ni safi kabisa kwa sababu tufike mahali, tujaribu kuweka misingi ambayo Watanzania wapewe kipaumbele na kweli kazi ifanywe na Watanzania. Hatuhitaji kuleta *tour-guide* afanye kazi hapa, waache Watanzania wafanye kazi hizi za *travel*, mambo ya *tour operations, scuba diving* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nilikuwa na haja ya kusema kwamba, Wizara hii vilevile inahitaji kuangalia suala zima la *section 44(1) and (2),* kuhusu malalamiko mbalimbali. Anasema kwamba, ninaomba ni-*quote: "Complaints against a tour-guide, the Act is silent on the appeal and mechanism for tour-guide, should he/she not be satisfied by the complaints raised by client of tourism having used his services."* Kunapotokea kwamba, *tour-guide* ametoa *poor service* kwa mteja, bado yule mteja anaweza kulalamika, lakini haitoshi, kwamba huyu ambaye amelalamikiwa ni yupi. Kwa hiyo, kuna haja ya sheria kidogo kujaribu kuainisha suala hili ili liweze kuwa sahihi zaidi. Lazima iwe *very clearly stated* na *procedure* ambazo kama *tour-guide* amefanya makosa, basi aweze kurekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili ninapenda kusisitiza kwamba, Muswada huu umekuja katika muda ambao kweli tunauhitaji, lakini bado kuna haja ya kuwa na *coordination* muhimu sana ya suala zima la utalii hapa nchini. Hatima ya Uwanja wa Ndege wa Mwanza, ninaomba ipewe kipaumbele na tuweze ku-*balance* utalii. Pili, kuna suala ambalo sisi kama Watanzania, tufike mahali sasa tuanze kudhibiti mapato yetu. Mapato kuwa yanavujavuja, ninadhani ni chanzo kibaya sana, tunahitaji fedha hii kwa ajili ya Watanzania. Wizara yako imekuwa na sifa nzuri toka umekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii; uendeleze mkakati huo na ujaribu kupunguza rushwa ndani ya Wizara yako. Watu wanapeana vitalu kiholela, biashara hii iishe. Vilevile na mambo ya kupeana viwanja hivi hivi yaishe, mambo ya kupeleka mbao nje kinyemela yaishe na mambo ya kupeleka meno ya tembo nje yaishe.

Mheshimiwa Waziri, nina imani kubwa na wewe, pamoja na Naibu wako na ningependa nimpongeze Katibu Mkuu wako kwamba, Wizara hii sasa imepata watendaji shupavu. Sasa ni vyema Watanzania tuwategemee sana kwamba, Wizara hii ni chanzo kikubwa sana cha mapato na ni vyema sasa muweze kufanikisha hilo litendeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninapenda kuunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kutoa taarifa kwamba, idadi ya Waheshimiwa Wabunge, mliyoomba ni wengi na inawezekana hata Jumatatu wengine wasifikiwe. Kwa hiyo, muache kukataa ninapowaambia mzungumze msiseme Jumatatu, mnaweza msifikiwe. Kwa hiyo, Mheshimiwa James Lembeli anasema Jumatatu, sasa labda Mheshimiwa Gosbrt B. Blandes kama uko tayari? Mnaoomba Jumatatu, mnaweza msifikiwe na mimi nitawaweka mtakuwa wa mwisho, maana orodha itakuwa inakwenda chini, waliotangulia ndio wale, kwa hiyo, mjue hivyo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada huu. Nami nichukue nafasi, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu wake na Watendaji wenzake, kwa kazi nzuri ambayo mmeileta hapa. Binafsi, nimefurahishwa sana kuona Muswada huu unatajwa kwa uwazi kwamba, shughuli hizi sharti zifanywe na Watanzania na si mtu mwingine. Katika hili, ninataka niiombe Serikali ihakikishe kwamba, sheria hii inafuatwa kwa umakini, isije ikatokea mwanya, kuna watu wengine wanatumia mwanya wa kutumia Watanzania wengine wakati wao siyo Watanzania, kwa kufanya shughuli ambazo kisheria wamepewa Watanzania kuzifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninayo machache ya kuongezea yanayoweza kuboresha Muswada huu. Kwanza kabisa, nianze na kifungu cha (4) cha Muswada ambacho kinaeleza kuwa, itakuwepo Kamati ya Ushauri na kifungu cha 4(3) kinatoa muda wa Kamati hii ya Ushauri *(Advisory Committee)* kufanya kazi zake. Ukiangalia kwenye Muswada huu, unaeleza katika jedwali la kwanza *(first schedule)*, kipengele cha 6(1) kuwa, Kamati hii ambayo ni muhimu sana, itafanya kazi zake ndani ya miaka mitatu na pia Wajumbe wa Kamati hii wanaweza kuteuliwa na Mheshimiwa Waziri, wakaendelea kufanya kazi hiyo kwa kipindi cha miaka mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, *concern* yangu ninataka nifahamu, hawa watu watateuliwa mpaka lini ni mpaka milele? Ninataka nishauri kwamba, kama itawezekana, ninapendekeza Wajumbe wa Kamati hii wakae kwenye madaraka kwa kipindi cha miaka mitatu, ikiisha kama huyo mtu anafaa, aweze kuteuliwa tena mara ya pili kipindi cha miaka mitatu na kama wanafaa tena, wateuliwe tena katika kipindi kingine cha miaka mitatu, yaani miaka tisa katika vipindi vitatu, baada ya hapo, tuwape nafasi Watanzania wengine nao watoe michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nikiwa hapo hapo, ninapendekeza Ibara ya 18, hii ni *Board Tenure*, muda wa Wajumbe wa Bodi kukaa madarakani; Muswada haujaonyesha watakaa kwa muda gani? Wameeleza ni miaka mitatu na baadaye

wanaweza wakateuliwa tena. Pia *Appeals Authorty Board* nayo katika *section 20(1),* imepewa muda huo huo kwamba, watakaa katika uongozi huo kwa kipindi cha miaka mitatu na bado wanaweza kuendelea kuchaguliwa na kuchaguliwa bila kufikia mwisho. Ninapendekeza sheria hii ikae vizuri, hawa wenzetu wakae kwenye madaraka katika vipindi ambavyo havizidi vitatu vya miaka mitatu mitatu. Hayo ni mapendekezo yangu na ninadhani yatasaidia sana kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye kifungu 5(1), kinahusiana na *Director of Tourism* na amaeonyeshwa kwamba, atakuwepo Mkurugenzi wa Utalii na sifa zake zimeelezwa kwamba, lazima awe na taaluma ya utalii. Ninadhani na vigezo vingine vingewekwa. Ninakubaliana na haya mapendekezo, isipokuwa nina ushauri mmoja tu kwamba, mtu huyu awe na taaluma ya utalii, lakini pia awe na taaluma ya masoko *(marketing),* aweze kutangaza utalii wetu nje na ndani ya nchi *properly*. Taaluma ya utalii peke yake, kwangu mimi ninaona kama haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 ya Muswada huu, inazungumzia *registration and grading of tourism facilities and activities*, inaelezea ni jinsi gani *Director* anavyoweza kukataa maombi ya mtu yeyote, anayetaka ku-*register facility* ya *tourism.* Hii ni sahihi kwamba, Mkurugenzi anayo haki ya kukubali au kukataa maombi hayo, lakini ninataka Muswada vilevile uboreshwe kwa kuweka vizuri kwamba, baada ya Mkurugenzi kukataa maombi ya mtu, je, ndiyo mwisho. Ningeshauri huyu mtu apewe nafasi ya kufanya marekebisho ya yale ambayo Mkurugenzi ameona kwamba hayafai, halafu aruhusiwe kuomba tena ili kuondoa mwingine anayeweza akawa *dictator*. Tunaweza tukawa na *Director* ambaye ni *dictator,* atawabana watu au kwa chuki binafsi aka-*reject application* ya mtu, basi ikawa ndiyo mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine kwa leo ni kuhusiana na kifungu cha 24(1), kinachohusiana na *cancellation of license.* Muswada unaeleza kuwa, mmiliki yeyote atafutiwa leseni kama itathibitika kuwa, amevunja masharti ya sheria hii. Hii ni sahihi kabisa, lakini ninataka nishauri kwamba, Muswada uwe na adhabu mbalimbali, si kwamba makosa yote yanafaa kufutiwa leseni. Katika Muswada huu, basi ikiwezekana tuweke faini mbalimbali kwamba, kuna kosa fulani dogo, litozwe faini labda ya shilingi 500,000, faini kubwa zaidi itozwe labda shilingi 1,000,000 na kosa kubwa zaidi mara mbili au mara tatu ndiyo leseni iweze kufutwa. Ikifutwa, ninashauri pia mtu huyu isiwe mwisho, kama imefutwa akajirekebisha, apewe nafasi tena ya kuomba leseni upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninaomba nirudi kwenye eneo langu la Jimbo la Karagwe. Jimbo la Karagwe ni kati ya majimbo ambayo Mwenyezi Mungu, ameyapendelea sana; lina wanyama wengi sana na vivutio kwa watalii. Wanyama maaufu tulionao, jana tumeambiwa tuseme ndovu, lakini kule kwangu hilo neno hawalitambui vizuri, wao wanajua kwamba ni tembo. Hawa tembo wa Karagwe, wakitumika vizuri ni kivutio kikubwa sana cha watalii. Kwa bahati nzuri, wameweza kuzaliana sana, lakini sijaona watalii wengi wanaokuja Karagwe kutembelea huko. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, atutengenezee utaratibu mzuri wa tembo wetu na sisi waonekane kwa watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa hapa hapa kwenye tembo, badala ya kuwa kivutio kwa watalii na Watanzania, wamebadilika kuwa kero kubwa sana kwa Wananchi wa Jimbo la Karagwe. Juzi nikiwa kwenye ziara yangu, nikitoka kijiji kimoja kinachoitwa Nyakakika nikielekea Kijiji cha Nyakasimbi, nilipishana barabarani na tembo wapatao 300, ilibidi nisimame pale kwa muda kama wa dakika 40 ili niweze kupishana nao. Kesho yake nilipoenda kwenye Kata nyingine, nikakuta wamelala kijiji hicho. Sasa tembo kwa Karagwe wamezagaa, wamekuwa kama mbuzi ni jambo la kawaida kupishana na tembo mahali popote unapotembea. Tembo hawa wamekuwa waharibifu, wanaharibu mashamba ya migomba na miti ya matunda.

Kwenye kikao cha bajeti, nilizungumza na nilimwomba sana Mheshimiwa Zabein Mhita, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, tupange safari ya kuongozana pamoja kwenda Karagwe, naye aliniahidi kwamba, mwezi Novemba, 2007, angekuwa mgeni wangu Karagwe. Kwa masikitiko makubwa ni kwamba, hajafika na kuweza kunisaidia tatizo hili. Niombe kabisa kwa mara nyingine na pengine ya mwisho, kumwomba Mheshimiwa Waziri mwenyewe kama Naibu imeshindikana, afike anisaidie, tembo kwa Karagwe imekuwa ni kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja hii. Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana. Ninaona kama nilivyosema, orodha yetu kusema kweli ni kubwa sana, siku ya Jumatatu tutaendelea nayo. Tunakusudia pia kesho baada ya semina itakayokuwepo, ninaomba Kamati ya Uongozi, kutakuwa na kikao cha dharura. Kesho tutakwenda *Nyerere Square* kwa ajili ya shughuli ile ya kuzindua Mpango wa Pili wa UKIMWI, asubuhi saa tatu, Wabunge wote wamekaribishwa. Baada ya hapo, tutakuwa na semina ile ya Waziri wa Fedha na baada ya hapo ndipo Kamati ya Uongozi, tukutane kwa muda mfupi, tuna jambo la kuweka sawa.

Wakati tunaanza kujadili Muswada huu, kulijitokeza kutaka mwongozo wa Spika, kwa mambo ninafikiri mawili; la kwanza lilikuwa kuhusu salamu. Hizi kanuni zitagawiwa mapema wiki ijayo. Kwa hiyo, kifungu cha 150(1)(2) mpaka (4) kinasema; “Endapo litatokea jambo lolote ambalo mhusika wake au mwathirika wa jambo hilo anastahili kupewa pongezi au pole na Wabunge, basi Spika atatoa pongezi au pole kwa muhusika au mwathirika wa jambo hilo kwa niaba ya Wabunge wote.” Kanuni ya 151(2) inasema; “Baada ya Spika, kutoa pongezi au pole kwa muhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Mbunge yeyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa muhusika au mwathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni.”

Kanuni 151(3); “Kwa upande wa Serikali, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni atatoa pole au pongezi kwa muhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa niaba ya Serikali.” Kifungu 151(4) kinasema; “Baada ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kutoa pongezi au pole kwa muhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa ajili

ya kuokoa muda wa majadiliano, Waziri yeyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa muhusika au mwathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni." Kwa hiyo, hiyo ndiyo Kanuni tulivyoiandika.

Kuhusu kutambulisha wageni, kifungu 139 cha kwanza na cha pili, kinasema; "Spika anaweza kuwatambulisha wageni wote wa Kitaifa na Kimataifa waliomo katika Ukumbi wa Bunge." Kifungu kidogo cha pili kinasema; "Spika vilevile anaweza kuwatambulisha wageni wengine waliomo katika Ukumbi wa Bunge ambao; (a) wanahusika moja kwa moja na shughuli za majimbo; (b) wanatembelea Bunge kwa ajili ya ziara za mafunzo; na (c) wametoa mchango wa kitaifa unaohitajika kuenziwa." Hiyo ndiyo tafsiri ya kutambulisha wageni.

Tafsiri ya maswali, kifungu 42(2) kinasema; "Mbunge atakayeitwa atasimama na kuuliza swali pamoja na masahihisho kama yapo kwa kutamka maneno yafutayo bila kuongeza jambo lingine lolote: "Ninaomba swali langu ….. (atataja namba ya swali lake lililopo kwenye *Order Paper*) sasa lijibiwe. Vivyo hivyo, Waziri atajibu kikamilifu."

Kwa sababu kile kifungu kingine kimesema hakuna pongezi au salamu au nini, basi ataendelea moja kwa moja kujibu maswali. Kwa hiyo, huu ni ufafanuzi wa yale maswali yalioomba Mwongozo wa Spika. Waheshimiwa Wabunge, Kanuni hizi zitatolewa mapema wiki ijayo, kwa sababu ya mabadiliko madogo tuliyofanya jana, basi inabidi tutoe wiki ijayo mapema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyokubaliana, kesho asubuhi tunaenda kwa ajili ya Uzinduzi wa Mpango wa Pili wa Kupambana na UKIMWI. Tutakuwa na Semina kuhusu Muswada ule wa Wizara ya Fedha kesho. Halafu Jumapili pia tutakuwa na semina juu ya Muswada wa mambo ya Umeme, *TANESCO* na Muswada wa *Petroleum*.

Jumapili tutaanza saa tano; kesho kwenye uwanja saa tatu na semina saa tano. Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru kwa wiki yote hii tuliyofanya kazi nzuri. Tumefanya kazi kubwa, kwa hiyo, twende tukapumzike *weekend*. Ninawatakieni *weekend* njema.

Sasa ninaahirisha Kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu Tarehe 4 Februari, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*